ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
3. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
4. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
5.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
6. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
7. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
8. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge

9. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
10. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
11. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
12.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
14. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
15. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
17. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
18. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
20. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
21. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
22. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
23. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
24. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
26. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
27. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
28. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
29. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
30. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
31. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
32. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
33. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
34. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani

35. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
36. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
37. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
39. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
40. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
42. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
43. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
44. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
45. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
46. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
47. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
48. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
49. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
50. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
51. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
52. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
53. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
54. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
55. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
56. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
57. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
58. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Jimbo la Chukwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Pili - Tarehe 23 Mei, 2016

(*Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Machano Othman Said (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Wenyeviti Kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2016/2017.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 32

Wahalifu Kutopelekwa Mahakamani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana asubuhi hii kupata fursa ya mwanzo, lakini hivi juzi tulipewa semina na katibu wetu Mussa Kombo Bakary namna gani mtu anaweza kuondosha swali kwa *theory* leo anataka kuondosha kwa *practical* baadhi ya wajumbe wajue namna gani kuondosha swali.

Mhe. Spika, nakuja katika hoja. Kwa hiyo, naomba serikali isijibu swali hili naliondosha.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, umeliondoa? Sijafahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, juzi tulipewa semina na Wajumbe wetu wengi ni wageni, nawaonesha mfano namna gani unaweza kuondosha swali, kwa sababu juzi tulipewa *theory* leo naonesha kwa *practical*. Naondosha swali langu Nam. 32.

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondowa)

Nam. 12

Stahiki na Maslahi kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:-

Kwa kuwa wafanyakazi wa Serikali za Mitaa wana kazi kubwa sana za kufanya usafi, lakini ndio wafanyakazi ambao hawapati stahiki zao kwa wakati wanapokwenda likizo na pesa za "*overtime*". Na kwa kuwa kuna wafanyakazi ambao ni wazee hawajafika umri wa kumaliza kazi na wanafanya kazi katika mitaro kwa muda mrefu wakati wapo vijana ambao wameajiriwa kwa muda.

(a) Je serikali haioni kuwa kutokuwalipa haki zao wafanyakazi hawa hatuwatendei haki.

(b) Kwa nini wazee hao wasibadilishwe wakapewa angalau kazi nyepesi ili kumaliza muda wao na vijana wakaajiriwa kabisa ili kuepusha uhaba wa wafanyakazi katika Mabaraza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 12 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Baraza la Manispaa Zanzibar ni taasisi ya serikali kama taasisi nyingine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hivyo, Baraza linatekeleza wajibu wa kuwalipa wafanyakazi wake stahiki zao zikiwemo "pesa za likizo" na malipo ya baada ya saa za kazi "*overtime*".

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi 72 walilipwa fedha za likizo na jumla ya Shilingi 30,467,300/- zilitumika kulipia malipo ya baada ya saa za kazi "*overtime*" za wafanyakazi kwa mwaka 2015/2016.

Wafanyakazi walioajiriwa katika shughuli za usafi wa mazingira ni wa mkataba, hivyo, malipo na stahiki zao zote zimelipwa na zinaendelea kulipwa kwa wakati husika kama tulivyokubaliana kwa mujibu wa mikataba hiyo. Aidha, Baraza halina deni la malimbikizo hayo.

b) Mhe. Spika, Baraza la Manispaa limeingia mkataba na vikundi 12 vya kijamii vya usafi ili kushika nafasi ya

wafanyakazi wazee, kati ya vikundi hivyo vikundi vitano vinafanya usafi wa barabara kwa kuzoa michanga, vikundi vinne vinafanya usafi wa taka kwenye masoko na maeneo ya Mji Mkongwe, kikundi kimoja kinafanya kazi ya bustani na vikundi viwili vinafanya kazi ya kusafisha misingi ya maji ya mvua na maji machafu.

Mhe. Spika, aidha, Baraza limetuma maombi kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kuajiri vijana kwa lengo la kufanikisha utendaji bora wa kazi za Baraza. Vile vile, Baraza la Manispaa litahakikisha kuwa kila anayeajiriwa anaendana na aina ya kazi na uwezo aliokuwanao. Aidha, ofisi yangu na taasisi zake itaendelea kuchukua hatua za kuwapima afya wafanyakazi wake ili kujua maendeleo ya afya zao.

Vile vile, vijana wengi bado hawajawa na muamko wa kufanya kazi za usafi, hivyo, wanapopatiwa kazi hiyo hawafanyi kwa ufanisi na wengine huondoka bila ya kutoa taarifa kwa muajiri wake. Kwa mnasaba huo serikali itaendelea kuwahamasisha na kuwaelimisha vijana kuona fursa za ajira ziliopo kupitia usafi na utunzaji wa mazingira sambamba na kuwawezesha katika shughuli hizo.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kisiwa chetu za Zanzibar ni kisiwa ambacho kinapendwa na watalii kutoka sehemu mbali mbali za nchi, lakini ukiangalia katika kisiwa hiki bustani nyingi zimepungua katika barabara zetu.

Je, Mhe. Waziri, amejipanga vipi kuziimarisha bustani hizo katika mji wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, nataka nikubaliane naye kwamba visiwa vyetu vya Zanzibar ni miongoni mwa visiwa vinavyopendwa na watalii na watu wengi duniani. Hivyo, serikali kupitia Baraza la Manispaa katika awamu hii ya saba imejipanga kwanza kurejesha nidhamu ndani ya mji wetu wa Zanzibar na kazi hiyo tutaifanya si muda mrefu kutoka sasa. Hivi sasa Baraza la Manispaa tayari limeanza kuimarisha bustani katika maeneo yake mbali mbali, hivyo, kazi hiyo itaendelea kufanyika ili kuufanya mji wa Zanzibar uweze kupendeza na kuendelea kupendwa na watu wengi duniani.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, nikiri kwamba wizara yetu hii ina majukumu mazito kuliko wizara nyingi katika nchi yetu, lakini pia ni wizara ambayo imebeba mambo mengi ya jamii. Mara nyingi wafanyabiashara na wananchi kwa jumla huwa hawana uzoefu au hawajali kutekeleza maagizo ya Halmashauri zetu juu ya usafi wa mazingira na hili ndio chanzo cha maradhi ya kipindupindu kutokea katika baadhi ya sehemu.

Je, Mhe. Waziri, kwa kuwa janga hili kubwa limetokea kwa baadhi ya wananchi kukosa makaro katika maeneo yao, kukosa vyoo na hata katika baadhi ya maeneo ya mkusanyiko wa watu kukosa vyoo vya serikali, haoni kwamba hii ndio sababu inayosababisha uchafu katika maeneo yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ: Mhe. Spika, ni kweli kabisa wananchi kujenga katika maeneo yasiostahiki kujengwa na yaliyopangwa kwa mujibu wa mipangomiji na yalioruhusiwa kisheria, ni moja kati ya sababu inayosababisha matatizo mengi ya huduma za kijamii hasa za usafi wa mazingira. Kwa hiyo, serikali kama nilivyokuwa nikijibu swali mama, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ; Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira; Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa pamoja zitashirikiana kuhakikisha kwamba tunayapitia maeneo yote yaliyojengwa kinyume na mipango miji na kinyume na taratibu au matumizi ya ardhi na kuweza kuchukua hatua ili kurejesha nidhamu ndani ya nchi yetu.

Jengine serikali tutaendelea kuwafahamisha wananchi wetu wa Zanzibar waweze kufuata sheria, kufuata taratibu ambazo sisi wenyewe tumejiwekea ili kujiepusha na matukio na majanga mbali mbali ambayo yanaweza kujitokeza, hasa kama yale Mhe. Mwakilishi, aliyoyataja ya maradhi ya mripuko wa kipindupindu. Serikali itafanya kazi hiyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Mhe. Waziri, alipokuwa akijibu swali la msingi Baraza la Manispaa linatekeleza wajibu wake kuwalipa wafanyakazi stahiki zikiwemo pesa baada ya saa za kazi, *weekend*. Lakini Mhe. Waziri kuna wazee mpaka hivi sasa mimi ninawajua wanfanya kazi siku za *holiday,* baada ya saa za kazi na mpaka sasa hivi hawajalipwa haki zao. Ni lini nikuletee ili wapate haki zao ukizingatia ni watu wazima.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu mpaka

mwezi wa Machi, Baraza la Manispaa kwa mji wa Zanzibar hakuna mfanyakazi yeyote ambaye anadai *overtime*, anadai pesa zake za likizo. Suala la kuwalipa *overtime* na fedha za likizo wafanyakazi ni jambo endelevu na sisi tunakwenda kwa mujibu wa utaratibu wa kiserikali wa malipo. Sasa kama wafanyakazi hao wapo hana haja yeye ya kuniletea, wanaowajibika wakuu wa utumishi katika sehemu hizo na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa atawajua, atawatambua na haki zao watalipwa iwapo watakuwa wanastahiki, lakini mpaka naondoka leo asubuhi ofisini kwangu hakuna mfanyakazi yeyote yule wa Baraza la Manispaa anayedai fedha zake za *overtime* au fedha za likizo.

Kwa taarifa yake Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tumeamua kuweka utaratibu maalum, lazima mfanyakazi yeyote na tunawazingatia zaidi wale wafanyakazi wa chini wanaofanya kazi za usafi kwanza kuwalipa haki zao kuliko wale wafanyakazi wanaofanya kazi sehemu zao za ofisini. Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru.

Nam. 6

Mikakati ya Kukuza na Kuondoa Migogoro Sekta ya Michezo

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Sekta ya michezo ni muhimu sana kwa kuwaunganisha vijana na pia michezo ni sehemu ya ajira kwa vijana.

a) Je, serikali imepanga vipi kuhakikisha kwamba sekta ya michezo inakua nchini kwa faida ya vijana wetu na nchi kwa ujumla.

b) Je, serikali ina mikakati gani ya kuondoa migogoro kwa baadhi ya vyama vya michezo ili kuondoa tatizo la kuanguka kwa kiwango cha michezo Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 6 lenye vipengele (a) na (b), kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein imejipanga vyema ili kuhakikisha kuwa sekta ya michezo

inakua nchini. Ni vyema tukarejea kumbukumbu za hotuba yake aliyoitoa siku ya ufunguzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi.

Mhe. Spika, ushahidi wa haya umejionesha wazi pale ambapo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuonyesha kwa vitendo alipotoa vifaa kadhaa katika fani tofauti za michezo ili kuthibitisha jinsi gani anavyoithamini michezo ili vijana wetu waweze kutumia michezo kwa faida yao kiafya, kijamii, kiuchumi, kisiasa na nchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye kipengele a na b kama ifuatavyo:-

a) Ni kweli kuwa sekta ya michezo ni muhimu sana kwa kuwaunganisha vijana na pia michezo ni sehemu ya ajira kwa vijana.

Serikali kupitia Wizara Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ikishirikiana na taasisi zilizopo chini yake hasa Baraza la Taifa la Michezo limejipanga kuhakikisha kwamba sekta hii inakua nchini kwa faida ya vijana na nchi kwa ujumla kwa kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili. Serikali imeanza kutekeleza yafuatayo:-

1) Kuwapatia vifaa vya michezo, kuwapatia mafunzo mbali mbali ya ualimu, uamuzi na uongozi wa michezo ndani na nje ya nchi.

2) Kutatoa tatizo la upungufu wa viwanja, serikali imeanza kujenga viwanja vya michezo kwa baadhi ya wilaya na serikali na dhamira yake ni kufanya hivyo kwa kila wilaya Unguja na Pemba kwa kadri ya hali itakavyoruhusu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la migogoro kwa baadhi ya vyama michezo, napenda nieleze kuwa migogoro mingi ya vyama vya michezo inatokana na viongozi wanaoviongoza vyama hivyo huongoza kwa utashi wao baada ya kuleta maendeleo ya vyama hivyo.Wengi huweka mbele maslahi binafsi baada ya maslahi ya chama husika na Taifa.

Mhe. Spika, aidha, wapo wanaojiweza kiuwezo pamoja na madaraka waliyonayo. Tatizo jengine linasababisha migogoro ni kutojitosheleza kwa Katiba za vyama vya michezo kwa mujibu wa mazingira ya nchi yenyewe. Baadhi ya Katiba nyingi zimetengenezwa kwa lengo la kujijengea wigo na hatimae wagombea wenye uwezo wa kufanya kazi kushindwa kupata nafasi za kuongoza.

Mhe. Spika, aidha, serikali inachukizwa sana na inachukuwa fursa hii kukemea ipasavyo migogoro ya mara kwa mara inayojitokeza kwenye michezo kwani mogororo hiyo haileti tija kwa wana michezo na wapenzi wananchi na wadau wa nje na ndani ya Zanzibar.

Mhe. Nassor Salum Ali: Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, lakini Mhe. Naibu Waziri, alipokuwa akijibu maswali yake amekiri kwamba migogoro mingi ya vyama vya michezo inatokana na viongozi wanavyoviongoza vyama hivyo.

(a) Ni vyama vingapi ambavyo vinaongoza kwa migogoro Zanzibar.

(b) Baadhi ya Katiba inayotengenezwa kwa lengo la kujijengea wigo na hatimae viongozi kuweza kushinda na wale ambao hawana uwezo kutopata nafasi ya kushinda. Je, ni chama gani Zanzibar kinachoongoza kwa kutengeneza Katiba ambayo inaweka wigo ambao unaozungumza hii.

Mhe. Waziri wa Habari Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli kama tulivyoeleza kwenye suala mama vipo vyama ambavyo vinaonekana kwamba vinaongozwa na vinaleta migogoro. Kama inavyoeleweka kwamba vyama vya mpira vingi na duniani kote ni vyama visivyoundwa na serikali moja kwa moja, lakini huwa ni vyama vinavyoungana na sekta binafsi, mfano wa chama hicho ambacho kinaleta migogoro ni kimoja tu kwa Zanzibar hivi sasa ni *ZFA*. Nataka nithibitishe wazi kwamba kwa kipindi cha muda wa miaka miwili iliyopita mpira wetu hapa ikiwa ni sehemu kubwa inahyounganishwa wana michezo haukuchezwa kikamilifu. Hii ilitokana na migogoro ya chama hicho.

(a) Kwa hivi sasa ndani ya Zanzibar ni chama kimoja na jina la chama chenyewe ni chama cha *ZFA*.

(b) Napenda nimjulishe kwamba Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, ni kweli Katiba zetu ndizo zinazosababisha kuwa na migogoro ndani ya vyama na vile vinavyoundwa vyote na kuendeleza michezo.

Hii inaonesha wazi kwamba pale panapotokea migogoro inayokwenda kinyume na Katiba mfano chama cha *ZFA* kinaeleza katika vipengele vyale vya Katiba haviruhusu wale viongozi kupelekeana kwenye Mahakama. Lakini ndani ya uongozi

wamethubutu kupelekana kwenye Mahakama. Tunaishukuru sana serikali imeweza kusimamia hayo kupitia wizara yetu ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imesitisha mambo yote ya kupelekeana Mahakamani na hivi sasa hakuna kesi za Mahakamani na suala la mipira na michezo yote kwa ujumla iko sawa na vyama vyengine vyote vya michezo viko sawa na sasa *football* kama alivyoeleza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iko juu na inaendelea kukua na itaendelea kukua. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri ya suala mama ambalo ameulizwa. Lakini pamoja na majibu hayo mazuri nielekee mimi katika suala zima la ukuaji wa michezo. Huwezi ukawa na ukuwaji mzuri wa michezo katika nchi yoyote bila ya kuona kwamba vijana wadogo wanapata mafunzo hayo na mafunzo hayo huwa yanaanzia katika skuli. Skuli zetu za Zanzibar ufundishaji wa somo la michezo umedorora kwa kiasi kikubwa na wizara yako ni wizara mama.

Je, ina uhusiano gani wa karibu na Wizara ya Elimu kuweza kuona kwamba mafunzo wa Elimu kwa Michezo kwa wanafunzi wetu wanakuwa na ufanisi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kama inavyojulikana kwamba kitu chochote huanza katika msingi wake wa awali na kweli vijana wetu wanategemea sana kufanya michezo vizuri endapo watapata misingi mizuri mashuleni ambako ndio chanzo cha michezo inapotokea. Katika awamu hii ya saba serikali imejipanga vizuri mawaziri wote kufanyakazi kwa pamoja.

Hivyo, Wizara ya Habari, Utalii na Utamaduni na Michezo iko karibu sana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na tayari tu hivi juzi tumeonesha baada ya kufungua kongamano la michezo la Vyuo Vikuu ambalo limefunguliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Mo'hd Shein katika siku hiyo tumeonesha wazi jinsi gani wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imeshirikiana na Wizara ya Elimu, kazi hiyo itakuwa endelevu, itaendelezwa kwa juhudi zote na sasa tusahau tafauti zetu katika michezo Zanzabar na itakuwa kuanzia watoto wa chini na wilaya hadi kufikia Taifa. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri, amekiri kwamba kuna migogoro katika Chama cha *ZFA* katika majibu yake ya nyongeza.

(a) Je serikali imechukuwa hatua gani ya kutatua migogoro hiyo.

(b) Kwa kuwa vyama vingi vya michezo vinakuwa havifanikiwi katika lengo lake ambalo limekusudiwa kutokana na ukosefu au ukata wa bajeti fedha. Je, serikali imejipanga vipi kuvipatia vyama hivyo vya michezo fedha ili viweze kujiendesha wenyewe. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kama tulivyoleza katika suala mama kwamba hapa Zanzibar ipo migogoro mingi kwa vyama vya michezo. Lakini serikali imechukuwa hatua kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kusimamia migogoro hii na ndio maana kwa sasa hivi migogoro ile yote imeondoka na hakuna kesi Mahakamani na sasa hivi michezo inaendelea kuchezwa kama kawaida.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Mwakilishi, arudie swali lake la (b).

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, kwa kuwa vyama vingi vya michezo vinakuwa havifikii malengo yake yaliyojiwekea kutokana na ukata wa bajeti au fedha. Je, serikali imejipanga vipi kuhakikisha vyama hivyo vinawapatia fedha ili ziweze kujiendesha wenyewe.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, napenda kuchukuwa nafasi hii kujibu suali ya nyongeza la Mheshimiwa wa Jimbo la Fuoni.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kwamba ukata wa fedha unaweza ukasababisha suala lolote kutokwenda mbele, nakiri hivyo. Kwa hivyo, serikali kila itakapopata fedha za kutosha tunahakikisha kwamba tutavisaidia vyama vile na kuiwezesha michezo yote iweze kufanikiwa. Mfano mzuri ni wachezaji wa *Athletic* wiki mbili zilizopita serikali imeweza kujipiga na kuwasaidia na hatimae wakaja na medali mbili za dhahabu, tatu za shaba na nne za fedha, wametokea washindi wa nne na kuwashinda mahiri wa mashindano wa michezo wa *Athletic*. Hizo

ndio jitihada za serikali na tutaendelea kufanya jitihada kadri fedha zinaporuhusu kupatikana. Ahsante sana Mhe.Spika. (*Makofi*)

Nam. 8

Matatizo ya maji Chambani

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Chambani bado kuna tatizo la maji katika baadhi ya Shehia ukilinganisha na wakati huu tulionao.

Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia kupata maji wananchi wa Wambaa kwa Azani na Tangi la maji Chambani na Mteng'ombe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 8 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Kijiji cha Azani kilichoko Wambaa hakikufaidika na Mradi wa Maji Vijijini kutokana na mradi huo kupunguzwa eneo la ujenzi *rescoping*. Hata hivyo, hivi sasa wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji na kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo tayari tumeleza mabomba ya maji ambayo yatatumia katika maeneo hayo na maeneo jirani. Aidha, timu ya *ZAWA* itakuwepo kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kuunga maji katika majumba yao.

Mhe. Spika, tangi la maji Chambani yapo maji ya kutosha na hii inatokana na kukamilika kisima chengine ambacho kimezinduliwa hivi karibuni tarehe 08/05/2016 na kiongozi wa mbio za mwenge kitaifa ndugu George Jakson. Mhe. Spika, kijiji cha Mteng'ombe ni miongoni mwa vijiji vilivyopata huduma za maji kupitia kisima cha maji cha ukutini, hapo awali kisima hicho kilikuwa kikifanya kazi vizuri na kuhudumia maeneo yote yaliyokusudiwa.

Hata hivyo, kutokana na uwezo mdogo wa kuzalisha maji katika kisima hicho sambamba na ongezeko la mahitaji ya matumizi mbali mbali ya maji, baadhi ya vijiji vilianza kukosa kabisa huduma ya maji, kikiwemo kijiji cha Mteng'ombe. Kutokana na tatizo hilo la uhaba wa maji, Mamlaka ya Maji tayari imeshachimba kisima ambacho kitaongeza wingi wa maji na kuyafanya maeneo yote yaweze kufikiwa na huduma hio muhimu kupitia msaada kutoka

Mtawala wa Serikali ya *Ras al Khaimah*. Mara kazi za ujenzi wa kituo katika kisima hicho utakapokamilika, wananchi wa Mteng'ombe watafaidika vizuri na huduma ya maji. Ahsante sana.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Spika, katika Shehia ya Ukutini kimechimbwa kisima cha kwanza mimefeli, kimechimbwa kisima cha pili maji hayatoshi, kimechimbwa kisima cha tatu bado hakijaunganishwa mabomba na wananchi bado wanaendelea kupata tabu ya maji.

Je, Mhe. Waziri, kichimbwa visima vitatu katika sehemu moja hatuoni kwamba serikali tunaitia hasara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, Serikali haiogopi hasara kwa kuwanufaisha wananchi wake. Tutafanya hivyo hata mara kumi kuhakikisha tu maji safi na salama yanawafikia wananchi. Tulifanya hivyo Chambani na ndio maana Chambani Tangi la maji kuna chengine sasa kinahudumia Chambani mote na hii inatokana labda aidha katika maeneo kuzuka chumvi au mchanga hatuwezi tukatumia kisima ambacho hakiko safi, si salama kwa wananchi wetu. Tutatafuta maeneo mengine hata kama kumi katika jimbo moja tutachimba. (*Makofi*)

Mhe. Omar Seif Abeid:

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo la maji ni kubwa katika jimbo langu hasa kwa baadhi ya maeneo kutokana na *Geographia* iliyopo katika jimbo langu la Konde. Je, serikali imejipanga vipi kuwapatia maji hasa kwenye mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ambalo ni tatizo sugu, wananchi wa vijiji vya Konde Misufini, Kifundi, Mkia wa Ng'ombe, Bandari Kuu na Vijiji vya Shehia ya Makangale hasa maeneo ya Msuka.

(b) Je, wizara kupitia mamlaka yake ya maji ina mpango gani wa kurejesha mashine iliyokuwepo zamani kwenye kisiwa cha Skuli ya Konde ambacho kisima hicho ndicho kilichokuwa kikisaidia sana kugawa maji kwa wananchi wa Msuka na Konde wakati sasa uzalishaji huo umepungua kwa asilimia hamsini. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ni vyema akawasiliana na sisi kujua tatizo la Shehia ni nini. Kilio kisiwe mashine, mashine inawezekana isiwe tatizo; unaweza ukawa na mashine lakini maji

huyapati, tunachokitaka huduma ya maji safi na salama. Sasa sijampata vizuri tatizo ni nini hasa lakini nimwambie kwamba awasiliane na sisi tutajitahidi kadri Mwenyezi Mungu atakavyotuwezesha kuhakikisha kwamba kabla ya mwezi mtukufu wa Ramaadhani maeneo yake yote yanapata maji.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri, amekiri ni kweli serikali imechimba visima vitatu katika Jimbo la Chambani na bado wananchi wanaendelea kupata shida ya kupata maji safi na salama. Na kwa kuwa Mhe. Waziri, ameendelea kusema kwamba serikali itachimba hata kama visima kumi, lakini ihakikishe kwamba wananchi wanapata maji safi na salama.

a) Je, Mhe. Waziri, haoni kwamba kuchimba vitatu hivyo na bado wananchi wanashindwa kupata maji, ni kwamba wizara yake inashindwa kupanga mipango thabiti na kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuchimba visima hivyo.

b) Mhe. Waziri, haoni kwamba ni vyema wakaelekeza pesa hizo katika mambo mengine kuwanufaisha wananchi kuliko kuchimba visima ambavyo haviwanufaishi wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Shida kwenye maji. Kwa hivyo, wizara yangu ina-*concern* na maji. Na mambo mengine ambayo yanajitokeza ni mambo ambayo yapo nje ya uwezo wetu. Yanapotokea haya hatuwezi kununa, ni lazima tufanye njia nyengine ya kuchimba kisima chengine kusudi wananchi wetu wapate maji. (*Makofi*)

Sasa kufanya hivyo, serikali haioni kwamba inapoteza na wala sio sababu ya kwamba kufanya upembuzi yakinifu, tunajitahidi kufanya lakini yanapotokea ya Mwenyezi Mungu hakuna wa kuzuia.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Nam. 2

Kukaa Maji Eneo la Barabara ya Mwanakwerekwe

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Kutokana na mvua zinazonyesha mara nyingi hutokea kujaa maji mengi katika bwawa la Mwanakwerekwe Shelimpya, kunasababisha usumbufu mkubwa wa usafiri katika njia hiyo. Kwa kuwa tatizo hilo limekuwa la muda mrefu na hadi leo linaendelea.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja katika barabara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 2 kama ifuatavyo:-

Tatizo la kujaa kwa maji kwenye barabara ya Mwanakwerekwe Shelimpya linatokana na kuwepo kwa bwawa la maji pembezoni mwa barabara hiyo ambapo kwa miaka ya nyuma maji yalikuwa hayajai mpaka kufunika barabara tofauti na hivi sasa. Sababu kubwa na ya msingi inayosababisha kufurika kwa maji mpaka barabarani na kufanya barabara ya Mwanakwerekwe kutopitika na kuleta usumbufu kwa watumiaji wa barabara hiyo wakati wa mvua inatokana na utupaji wa taka na kufinywa kwa njia za asili za maji zinazotokana na ujenzi holela wa nyumba kwenye maeneo hayo. Kuna njia za asili zinazopitisha maji kutoka kwenye ziwa la Mwanakwerekwe hadi ziwa Maboga ambazo baada ya ujenzi holela ama zimefinywa au kuzibwa kabisa na kuwa chanzo cha kuleta maafa kwenye maeneo hayo.

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na mambo mengine, iliunda Kamati ya Wataalamu kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali, wakiwemo Wahandisi wa Wizara yangu, kwa ajili ya kutafuta vyanzo vya matatizo na kupendekeza suluhisho la kuyaondoa matatizo yanayosababisha maafa ya mara kwa mara kwenye maeneo mbali mbali likiwemo hilo la Mwanakwerekwe Shelimpya. Taarifa ya mapendekezo ya Kamati imeshawasilisha kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na naamini kabisa hatua zilizopendekezwa zitafanyiwa kazi baada ya kufanyiwa mapitio na Serikali Kuu.

Aidha, Wizara yangu inatizama uwezekano wa kulipanua daraja la barabara ya Nyumba Mbili ili kuliwezesha magari kupishana kwa wakati wowote ule. Mbali na juhudi hizo Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ tutaangalia uwezekano wa kuimarisha barabara inayotoka Kwamabata kupitia kwa Kinyang'unya hadi kufikia Mwanakwerekwe Makaburini ili iwe ni njia mbadala wa kwenda Fuoni na maeneo mengine kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara ya Mwanakwerekwe Nyumbambili.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Naomba tuwe wazi kabisa. Hivi sasa tunaamini kwamba barabara yetu hii ni barabara kuu kulinganisha na barabara zote, ukiacha barabara ya Mkokotoni na kwengineko, ina ruti zinafika nane au kumi. Makunduchi, Kizimkazi, Jambiani, Michamvi, Bwejuu, Unguja-Ukuu na kwengineko. Inapotokea mvua kama hii huwa ni athari kubwa kwa wananchi wetu wanaotoka shamba kuja mjini au wanaotoka mjini kwenda shamba.

Je, swali langu lipo pale pale. Pamoja na kuwa kuna mpango umepangwa huko kwa Mhe. Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini ujenzi wa barabara unakwenda na madaraja. Pamoja na kuangalia na utaalamu huo, Wizara ina mpango gani kuhakikisha angalau kujenga daraja japo ndogo, siyo kwamba kama ya Kivukoni ambayo hatuiwezi. Haioni kwamba ipo haja ya kujengwa daraja kwa ajili ya kuokoa muda huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ahsante, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri, naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Ni kweli kabisa tunajua kwamba ile barabara inatumia ruti nyingi sana na zaidi ya kumi kama alivyosema yeye. Ni barabara muhimu sana. Ndiyo maana katika swali lake la pili, tutaelezea kwa nini sisi tunataka ile barabara kuhakikisha inakuwa barabara nzuri na ya kisasa kabisa.

Na hilo suala la kutaka kujengwa daraja ni vyema mapendekezo ambayo tunawakilisha kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, na kama alivyosema mwanzo kuna *alternatives* nyingi tu. Kwa hivyo, moja wapo wa *alternative* hiyo ni ile ya kuonesha kwamba zile njia za asili za kupisha maji, zitakuwa

zinapita maji kama kawaida na hapo itabidi tuchukue maamuzi magumu. Na nitamuomba Mhe. Mwakilishi awe tayari kushirikiana na sisi kulitekeleza hilo. Ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri, nimekuona Mhe. Shamata Shaame Khamis, halafu atamalizia Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba na mimi nichukue fursa hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Jimbo la Micheweni ni sehemu ambayo kwa kiasi fulani au kwa asilimia kubwa ya barabara zinazojengwa katika Kisiwa cha Pemba zinatokana na maliasili inayotoka kwenye jimbo langu. Lakini kwa sasa hivi ni muda mrefu mno wananchi wa Jimbo la Micheweni wanakuwa wakilalamika sana kuhusu barabara ambazo zinatumika kuchimbwa kifusi cha kutengeneza barabara, lakini wao wananchi wa Jimbo la Micheweni hadi hii leo hawajapata barabara au barabara zao ni mbovu na hazipitiki hususan katika kipindi cha mvua zinazoendelea.

Ninamuomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri. Ni lini sasa atachukua hatua ya kuona kwamba sasa wananchi wa Jimbo la Micheweni ikiwa wao maliasili yao inapotoa, lakini wao hawafaidiki na mpango huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mimi mwenyewe juzi nilikuwa ziarani Pemba, nikaweza kuangalia maeneo yote likiwemo eneo la Micheweni. Zipo barabara ambazo ni barabara za ndani. Barabara hizi ambazo tunaziita barabara za mlisho *(feeder road).* Hizi zipo chini ya Halmashauri za Wilaya husika. Sisi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika tupo tayari kutoa mashirikiano ya kutosha kwamba kuhakikisha na nia yetu hiyo, barabara zote zile muhimu katika kipindi chetu hichi cha Ilani ya Uchaguzi wa CCM wa 2015/2020, zinapitika ili kuwaondoshea wananchi wetu shida na kero hizo.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Nassor Salim Ali, kwa swali la nyongeza na la mwisho kwa swali hili.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo la barabara hii ya Fuoni linaendelea na kuendelea siku hadi siku na hasa Mhe. Ali Suleiman Ali, alipoeleza kuhusu ujenzi wa daraja pale. Lakini mbali na hilo, serikali ilikuwa na mpango wa kujenga barabara kutoka Kwarara kwenda Kisauni ambayo ingesaidia sana kuondoa msongamano hususan linapotokea tatizo la maji katika maeneo ya barabara hii ya Fuoni/Mwanakwerekwe.

Je, mpango huo upo na kama upo. Ni lini utaanza kujengwa barabara hii ya Kwarara/Kisauni. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Ni kweli barabara hii ni barabara muhimu katika kupunguza msongamano na ipo katika mipango ya Halmashauri ya Wilaya husika. Na kwa kushirikiana na wizara, sisi tutahakikisha kwamba barabara hii na siyo hii tu, ni barabara zote kama nilivyosema tunahakikisha kwamba zinapitika kwa urahisi ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo na abiria. (*Makofi*)

Kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu atusubiri na nina imani kabisa chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein basi hiyo kazi itafanyika *inshaallah.* (*Makofi*)

Nam. 3

Malipo ya Fidia kwa Wananchi Waliobomolewa Nyumba zao Mwanakwerekwe

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa ujenzi wa barabara ya Kwerekwe – Fuoni, ambayo ujenzi wake unaendelea vizuri, kwa kuwa ujenzi huo wa barabara umeenda sambamba na ubomowaji wa nyumba ziliopo karibu ya barabara hiyo.

a) Je, Mhe. Waziri, wananchi waliokumbwa na ubomowaji huo wamelipwa fidia.

b) Ni kiasi gani cha fedha kimetumika kwa malipo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 3 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi naomba nitoe maelezo mafupi juu ya mradi wa ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe – Tunguu (12.6*km*) ambao unajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kwa kiwango cha lami na unatekelezwa kwa awamu. Mradi huu umekusudia kujengwa barabara mbili (*Dual carriageway*) ambazo zitajumuisha na sehemu za waendao kwa miguu, wapanda baskeli, eneo la kugawa barabara (*medium*) ambalo baadae patawekwa taa (*street lights*), eneo la mitaro na eneo la kupanda miti.

Kutokana na mahitaji yote hayo na kwa kuzingatia ukuaji wa Mji wetu wa Zanzibar, ongezeko la gari na umuhimu wa taasisi zilizopo Tunguu pamoja na makaazi ya watu, Serikali iliamua kulitumia eneo lote la akiba lenye upana wa mita 30 (mita 15 kila sehemu kutoka katikati ya barabara ya asili) kwa mujibu wa Sheria ya Marekebisho ya barabara *(Decree Cap 134* ya mwaka 1927) ya mwaka 2012. Aidha, kumbukumbu za Kamisheni ya Ardhi zinaonesha kwamba eneo la barabara hiyo kutoka kwenye makutano ya barabara Mwanakwerekwe (*round about*) hadi Kituo cha Polisi Fuoni ni sehemu ya eneo lililotangazwa kuwa ni eneo la mji tokea mwaka 1982 *(Zanzibar Master Plan, 1982).*

Baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo:-

a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi sasa haijalipa fidia ya nyumba ya mtu yeyote kutokana na ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe – Fuoni na baadae Tunguu.

b) Kwa kuwa hakuna aliyelipwa fidia hadi sasa maana yake hakuna fedha zilizolipwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwanza kwa dhati kabisa ninampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ninaamini wananchi wote wanaotumia barabara hiyo na wengineo wameridhika na maendeleo ya ujenzi siku hadi siku. Lakini nina swali dogo tu Mhe. Spika.

Pamoja na uzuri wa barabara hii ambayo itakuwa ni ya mfano maeneo yetu au barabara zetu kwa sifa zake alizozitangaza Mhe. Naibu Waziri. Je, kwa kuwa

tunakwenda na wakati, tunaona sasa hivi barabara kutoka Amani mpaka Uwanja wa Ndege zinatiwa taa barabarani, kutoka Amani mpaka Mwembeladu, kutoka Magomeni na kwengineko tunakwenda na wakati.

Je, wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba barabara hii kwa kuwa inajengwa ni mpya ili kuondoa ubomoaji na baadae kula hasara, ina mpango gani wa kutia taa kabisa ili barabara ile iende sambamba na uzuri wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako ninapenda kulijibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Ni kweli kabisa hivi sasa mji wetu unang'ara sana na hii tunatoa pongezi kwa Wizara ya Nchi (AR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, kupitia mradi wao *ZUSP* ambao unasema *Zanzibar Urban Service Programme.* (*Makofi*)

Kusema la ukweli mradi huu umeonesha kwamba Zanzibar hivi sasa inaelekea kule ambapo wenyewe wanasema Zanzibar ni ya kisasa kabisa.

Mhe. Spika, kuhusu suala lake hilo, ninataka kumuhakikishia kwamba hiyo ni mipango yetu na hii vile vile tunataka iwe barabara ya mfano. Kwa hivyo, kadri uwezo utakavyotuwezesha kuweza kujenga hiyo barabara, vile vile, tunamuomba Mwenyezi Mungu tunamuhakikishia kwamba tutatia taa kwenye barabara hiyo, tutakuja kumuonesha baadae ili watu wetu wajue nini tunataka kukusudia; ni barabara ya mfano kusema la ukweli na itakuwa ya kimataifa kwa *standard* zake, ikiwemo kujengwa bustani pamoja na mitaro na hizo taa anazosema Mhe. Mwakilishi. Kwa hivyo, ninamwambia Mhe. Mwakilishi kwamba, taa zitatiwa na asiwe na wasi wasi asubiri muda utakapofika *inshaallah*. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri, nilimuona Mhe. Zulfa Mmaka, halafu atamalizia Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri, nijue ni muda gani unatarajiwa kumalizika kwa ujenzi huo wa barabara ya Mwanakwerekwe/Tunguu, kwa sababu kutokumalizika kwa barabara hii imeshakuwa kero kwa wananchi. Kwa hivyo, naomba nijue muda gani utachukua hadi kumalizika kwa ujenzi wa barabara hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako ninapenda kujibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi.

Kwa mujibu tulivyopanga na mkandarasi tunatarajia barabara hii kumalizika ujenzi wake ifikapo Disemba mwaka huu 2016. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri na swali la mwisho kwa Wizara hii ni Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwa vile suala moja limeshajibiwa, naomba nimalizie kwa suala hili.
Je, ni fedha kiasi gani zinakusudiwa kutumika katika barabara hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ahsante. Swali lake hili baadae nitamjibu kwa maandishi kwa sababu mwanzo tulivyokusudia kujenga hizi, kumekuja kujitokeza baadhi ya matatizo. Matatizo yenyewe ambayo sasa hivi tumekaa na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kuhakikisha kwamba tatizo hilo tunalitatua na kujua gharama zake. Kwa sababu kama munavyojua barabara ile ina miundo ya taa za zamani na vile vile kulikuwa na bomba la maji kubwa lililopita pale. Sasa tutakaa na wataalamu ili kujua gharama zote, baada ya kujua gharama hizo zitaongezeka katika barabara hii. (*Makofi*)

Na vile vile ninapenda kufahamisha tu kwamba hii barabara tumeipanua zaidi. Kwa hivyo, kutakuwa na gharama za nyongeza ambazo tutamjibu kwa maandishi kama atayataka. (*Makofi*)

Nam. 14

Kuimarisha Sekta ya Uvuvi

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:-

Wananchi wanahitaji kupewa elimu ya kutosha ili wasiharibu mazao ya baharini na pia wasitumie nyavu za kukokota ambazo hazifai kutumika. Pia, wapewe mafunzo na wasaidiwe vifaa vya uvuvi wa kisasa pamoja na zana za uokozi katika mabadiliko hayo.

Je, Serikali imejipanga vipi kutimiza malengo yake ya kuimarisha sekta ya uvuvi kwa kuzingatia mambo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo machache kuhusiana na suala la wananchi kupewa elimu ya mazao ya bahari. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi itaendelea kusimamia mpango Mkakati pamoja na kutoa elimu juu ya uhifadhi kwa wavuvi na Kamati Tendaji zote kufuatia programu ya maendeleo ya uvuvi na uhifadhi wa bahari, ambao imekwishafunza wavuvi na kuwapatia vifaa mbali mbali vya uvuvi kupitia mradi wa *MACEMP*.

Mhe. Naibu Spika, ili uvuvi haramu usifanyike mbali ya elimu ya mafunzo na vitendo inayotolewa kwa wananchi hao, pia tutaendelea kufanya doria za baharini ili kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu. Wito wangu kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili, ni kuwa tushirikiane kwa pamoja ili wavuvi wavuwe kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo. Serikali kupitia wizara imeandaa mkakati wa utekelezaji mipango maalum ya kuwawezesha wavuvi, ili kuondokana na uvuvi mdogo mdogo na kuwapelekea kwenye kina kirefu cha maji. Mpango huo utaanza kwa kuwapatia elimu na ujuzi kivitendo na hatimaye kuandaa utaratibu utakaowahusisha sekta binafsi, yaani *deep sea fishing* na kuendeleza ufugaji wa samaki ambao ndio ufunguzi wa kuongeza kupata na kupambana na uvuvi haramu.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, wavuvi wetu wa shamba ni wavuvi ambao bado hawajaelewa uvuvi ulio halali na wananchi hawa hawataelewa kama hawatokopeshwa angalau nyavu, mashine za kuvulia na wakapewa utaratibu ulio madhubuti.

Je, Mhe. Naibu Waziri, umejipanga vipi na hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, imejipanga katika kuwasomesha wavuvi na tutaanza na wavuvi 60, wavuvi 30 kutoka Unguja na 30 kutoka Pemba, ili kuweza kuwafundisha mafunzo hayo ya uvuvi wa bahari kuu ambapo utawawezesha kuvua katika kina kirefu zaidi cha maji. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nimekuona Mhe. Simai Mohammed Said na tutamalizia na Mhe. Amina Iddi Mabrouk.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri, kuhusiana na uvuvi haramu unaofanyika kwenye bahari. Nataka kumuuliza swali moja kuhusiana na uvuvi unaofanyika kwa kutumia mabomu, ambayo ni *fishing using dynamite.* Ni muda mrefu sasa katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na visiwa vyetu tatizo hili linakuwa linaendelea, hasa upande wa Magharibi mwa Pemba, ambayo ndio inaitwa Peka na kwa upande wa Kisiwa chetu cha Unguja hapa Zanzibar eneo la Minai mpaka Kizimkazi na Makunduchi kwenda chini.

Ni hatua zipi za kisheria ambazo zimetumika katika wizara yako katika kulikabili janga hili ambalo linataka kutuumiza na vizazi vinavyokuja kwa nchi yetu. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe.Spika, kuhusu suala la uvuvi haramu wa mabomu unaofanyika eneo la hifadhi. Kwanza maeneo ya hifadhi tuna mpango wa kuongeza doria zaidi ili kuweza kulinda yale maeneo ya hifadhi. Pia, sijui kama nimemuelewa vizuri, kasema sijui kuhusu kusimamia sheria?

Mhe. Spika: Mhe. Simai Mohammed, weka sawa swali lako kidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Lakini naomba lingekuja swali, maelezo yake nimemuelewa.

Mhe. Spika: Atakuwekea sawa tu, tafadhali. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika. Swali langu lilikuwa ni jepesi kabisa, kama maelezo yangu yamemtosheleza Mhe. Naibu Waziri. Swali ni kwamba, hili janga limekuwa ni sugu Mhe. Naibu Waziri na yamekuwa yanaandikwa kwa sifa mbaya nchi yetu, lakini pia yanahatarisha maisha ya vizazi vya watoto wetu wanaokuja kwa *generation* za mbele.

Je, wizara yako imechukua hatua gani za kisheria kulikabili janga hili katika maeneo haya, au kwa lugha nyepesi kabisa, ni watu wangapi wamekamatwa katika muda wa miaka miwili, mitatu. Sitaki kusikia masuala ya elimu, ni hatua za kisheria zilizochukuliwa, ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante. Mhe. Mjumbe, nadhani Mhe. Naibu Waziri, atakuwa hawezi kukujibu idadi ya watu, yaani masuala yale ya kitakwimu, lakini nafikiri kimsingi ngoja tumuachie waziri mwenyewe asaidie hili swali. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Naibu Waziri, kwa kujibu kiufasaha swali la msingi na swali la nyongeza aliyoulizwa. Vile vile, nimshukuru sana Mhe. Simai Mohammed, kwa kuuliza swali lake la nyongeza, ambalo kama alivyosema kweli ni tatizo la msingi kabisa katika Taifa letu. Pamoja na taaluma nyingi inayotolewa kwa wavuvi juu ya athari zinazopatikana kwa kutumia mabomu, kutumia nyavu ambazo hazistahiki, mazingira ya bahari zetu zote zimeharibika sana. Ndio maana tukaanzisha mradi wa uhifadhi angalau watu waelewe pale ambapo tumeweka hifadhi ya kiasi gani cha samaki wanapatikana na kiasi gani watalii wanapata fursa ya kuona aina za samaki ambao tunao katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wito wetu kwa wananchi na kwa Watanzania wote, kwa sababu bahari yote inakwenda mpaka Bara huko, ni kwamba lazima tuheshimu sheria za kutumia nyavu zinazotakiwa katika kuvua, lakini pia kuwaondoshea tatizo ambalo wavuvi wanalo. Tumeanzisha programu ya kuhakikisha tunazalisha samaki sasa wa kufuga, kwa sababu unaweza ukakazia sheria, lakini kama huwapi watu *alternative*, yaani njia mbadala basi uharamia utaendelea. Sasa njia mbadala tutakayoitoa ni kuhakikisha kabisa tunafuga samaki, na kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi, hivi sasa tuna mradi ambao juzi tulisaini na *FILO* wa dola milioni 4, ili kuwasaidia wavuvi sasa kuweza kufuga samaki na kuzalisha vifaranga vya samaki ili tuhakikishe samaki wanapatikana. *(Makofi)*

Lakini kuna wananchi ambao bado wanapenda kuvua uvuvi wa haramu, lazima sheria zichukuwe mkono wake, naomba tawala za mikoa, wenzetu wamekutana wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya na masheha tuwa-*identify* hawa watu ambao wanafanya uvuvi haramu. Nimekutana na wavuvi nimewaeleza, wao wanajuana nani anafanya uvuvi haramu, tuwadhibiti, tuwakamate na tuwachukulie hatua. Wakati tumewapa uhuru kama kuna mtu ana tatizo aje wizarani tumsaidie tumpe *alternative* ya kufanya, asiendelee na uvuvi ule, sasa akikaidi ni lazima tuchukuwe hatua za kisheria, ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Waziri, amekiri kwamba uvuvi haramu bado upo na unaendele siku hadi siku. Kwa kuwa Mhe. Waziri, amesema kwamba wanafanya doria katika kudhibiti uvuvi huu haramu. Je, Mhe. Waziri, kwa kuwa bado unahitajika udhibiti mkubwa wa uvuvi huu haramu, wizara yako inafanya doria kwa mwezi mara ngapi?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inafanya doria kila siku kwa ufupi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, maswali yamekwisha. Sasa kabla hatujaendelea na shughuli nyengine, naomba nitowe matangazo ya wageni wetu waliotufikia hapa. Kwanza kabisa naomba niwatangaze wageni waliopo ni wageni wa Mhe. Maudline Cyrus Castico Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Wageni hao ni wazee wanaolelewa katika Kituo cha Sebleni, jumla yao ni wanne na majina yao ni kama ifuatavyo. Mzee Asaa Ali Issa, Bi Asha Rajab Shaa, Bwana Omar Said Machenge na Ali Khamis Takadiri wakiongozwa na mlezi wao ndugu Tahiya Abdalla, naomba msimame ili tuwaone. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi kutoka Skuli ya *SOS*, jumla yao ni saba na kiongozi wao ni Badru Suleiman Badru, naomba mnyanyuke kwa pamoja. Ahsanteni, hayo ni matangazo ya wageni. Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea na shughuli inayoendelea basi nitamuomba Mhe. Naibu Spika, aje achukuwe kiti, lakini nitapenda kuwatajieni wajumbe watano ambao watakuwa wanaanza hii leo asubuhi katika michango, baada ya kusikiliza mchango wa Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kuhusiana na bajeti. Mpaka sasa hivi jumla ya wajumbe ambao wameshaleta maombi ni wajumbe tisa tu, lakini wajumbe watano watakaochangia wa mwanzo ni Mhe. Ali Suleiman Ali, atafuatiwa na Mhe. Mohammedraza Hassanali, Mhe. Simai Mohammed Said, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy na mjumbe wa tano atakuwa Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Baada ya hapo sasa naomba nimuombe Mhe. Naibu Spika, aje achukuwe usukani wa Baraza ili aendelee na huu mchango. Mhe. Naibu Spika, tafadhali.

(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali na Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mhe. Machano Othman Said: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu): Mhe. Naibu Spika, naomba niwasilishe ripoti au hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti na ninaiwasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti wetu Mhe. Hamza Hassan Juma, ambaye amepata dharura.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba tumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema, katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na wananchi wetu. Pia, kukutana tena katika Baraza letu tukufu katika Mkutano huu wa Bajeti ili tuweze kujadili, kushauri na hatimae kupitisha bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, pongezi zetu za dhati zimwendee Mheshimiwa Dkt. Ali Muhammed Shein Rais wetu kipenzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuchaguliwa tena kwa kishindo na wananchi wa Zanzibar kwa asilimia 91.4. Tunamuomba Mwenyenzi Mungu azidi kumpa hekma na busara katika maamuzi yake anayoyafanya.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza inamuomba Mheshimiwa Dkt. Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuyatekeleza na kuyasimamia kwa dhati yale yote aliyoyaahidi kwa manufaa ya Chama chetu cha Mapinduzi na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla. Miongoni mwa mambo ambayo Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein ameyaahidi, ni pamoja na kuwachukulia hatua wale wote ambao kwa namna moja au nyengine watakwenda kinyume na maadili ya kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuchaguliwa na wananchi wa Tanzania kushika nafasi hiyo. Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, inazithamini juhudi kubwa zinazochukuliwa na Rais wetu huyu kwa lengo la kuhakikisha kuwa hakuna matabaka ndani ya Tanzania. Tunamuomba Mwenyenzi Mungu azidi kumjaalia nguvu, afya njema pamoja na kumuwezesha kuwabaini wale wote wenye nia mbaya na nchi hii ya Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, tunamuomba *Allah Subhanahuwataala* aendelee kumlinda na hasadi yoyote iliyopo dhidi yake kiongozi wetu huyu. Mhe. Naibu Spika, tunayaomba haya kwa kuwa bila shaka wapo baadhi ya Watanzania ambao hawayaungi mkono yale maamuzi yanayofanywa na Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli kwa maslahi ya Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, napenda pia kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa ujumla wale wote waliopata uteuzi wa Mheshimiwa Rais katika nyadhifa mbali mbali wakiwemo Makamo wa Pili wa Rais, Mawaziri, Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wote wa serikali. Kamati ya Wenyeviti inawaahidi itaendelea kushirikiana nao kwa karibu katika kuhakikisha

tunatekeleza wajibu wetu wa kikatiba katika kutumikia wananchi na Taifa kwa ujumla, ili malengo ya nchi yetu yaliyopangwa yaweze kufikiwa kwa ufanisi mkubwa pia kwa wakati uliopangwa.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaenda moja kwa moja na kuanza kutoa maoni ya kamati kuhusiana na Mapendekezo ya Bajati, Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/2017. Nitakuwa mchoyo wa shukurani kama sijampongeza Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed, pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndg. Khamis Mussa, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuandaa nyaraka zote tatu ambazo ndio zilikuwa nyezo kuu katika kuipitia bajeti nzima ya serikali na kuhakikisha bajeti hiyo inaendana na malengo ya kitaifa.

Pia, shukrani za dhati kabisa ziwaendee Makatibu Wakuu wa wizara mbali mbali, wakurugenzi na jopo zima lililoandamana na Waziri wa Fedha, kwa ajili ya kutoa ufafanunuzi wakati wa kujadili na kamati maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Wahusika wote yaani "*stake holders"* kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyaonesha, katika hatua za kuyapitia mapendekekezo ya Bajeti na Mpango wa Maendeleo katika hatua ya Kamati. Mashirikiano yao yamekuwa na msaada muhimu sana katika kuiwezesha Kamati yetu kukamilisha jukumu hili kikanuni.

Mhe. Naibu Spika, pia, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati hii, naomba shukurani zangu maalum ziende kwa wananchi wa Jimbo la Shaurimoyo kwa kuendelea kumuamini na kumpa kura za ndio. Naomba pia na mimi nichukuwe nafasi hii kama mjumbe wa kamati, kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mfenesini ambao walinichagua kwa kura nyingi za ndio. Ni matarajio yangu kwamba tutaendelea kushirikiana katika kuleta maendeleo ya jimbo letu, na kwa ujumla kuwasaidia wananchi wa Zanzibar katika maendeleo yao.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutumia fursa hii napenda pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ambao ni Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, pamoja na makatibu kamati kwa kutumia muda wao mwingi kuipitia na kuifanyia uchambuzi bajeti hii katika kipindi kifupi ambacho bajeti iliwasilishwa. Kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame	-	M/Mwenyekiti

3.	Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Mjumbe
4.	Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Mjumbe
5.	Mhe. Machano Othman Said	-	Mjumbe
6.	Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Mjumbe
7.	Mhe. Omar Seif Abeid	-	Mjumbe
8.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
9.	Ndg. Abdalla Ali Shauri	-	Katibu
10.	Ndg. Kassim Tafana Kassim	-	Katibu

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 88, moja kati ya majukumu ya msingi ya Baraza la Wawakilishi ni kuidhinisha na kusimamia mipango ya Serikali katika njia ile ile ambayo bajeti ya mwaka iliidhinishwa. Aidha, Kanuni za Baraza la Wawakilishi, kanuni ya 117(2)(a) imeipa jukumu Kamati ya Wenyeviti kuchambua mapendekezo ya jumla ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi. Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu imeifanya kazi ya kuipitia na kuichambua bajeti ya Serikali pamoja na Mpango wa Maendeleo kwa ufanisi mkubwa na ni matarajio yetu kwamba Wajumbe wa Baraza lako tukufu, wengi wao ni wapya watapata fursa ya kuchambua na kuishauri vyema Serikali ili bajeti hii iwe bora na iwe na manufaa kwa wananchi wote.

Mhe. Naibu Spika, sote tunakumbuka ni hivi karibuni nchi yetu imetoka katika harakati za uchaguzi ambao umetoa fursa ya kupata Baraza jipya ambalo lina idadi kubwa ya wajumbe wapya. Hata hivyo, pamoja na uwepo huo wa idadi kubwa ya Wajumbe wapya naamini kwamba Wajumbe watafanya kazi zao kwa umakini na uhodari mkubwa na dalili za hayo tayari zimekwishaonekana.

Mhe. Naibu Spika, tunaishukuru sana Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuwapatia Mafunzo Wajumbe wa Baraza kuhusu Majukumu yao pamoja na mambo mbali mbali ya msingi yanayohusu Baraza, ikiwemo Itifaki ya Baraza, Kanuni za Msingi za Baraza, na Mafunzo ya Uchambuzi wa Bajeti. Tunatumai kwamba mafunzo hayo yaliyoanza kutolewa yatasaidia sana katika kuwawezesha Wajumbe kutekeleza vyema majukumu yao likiwemo hili lilo mbele yetu la kuidhinisha Bajeti Kuu ya Serikali. Pamoja na hayo lakini bado iko haja ya kuendelea kutoa mafunzo ya ziada kwa wajumbe hawa, kwani jukumu walilokuwa nalo ni kubwa kwa Taifa, kwa hiyo, ni lazima kufanya maamuzi kwa uelewa na umakini mkubwa, kwani sheria watakazozitunga hapa ndio zitakazokua dira na muongozo na misingi ya Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, Bajeti ya Serikali ni waraka muhimu sana katika mustakbali wa Taifa lolote lile, ni nyenzo kuu inayootarajiwa kuakisi utekelezaji wa

Mipango ya Kitaifa na Kimataifa ambayo inalengo la kuliendeleza Taifa katika maendeleo endelevu kwa mujibu wa shabaha na matarajio yaliyowekwa katika Mipango ya nchi yetu. Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni chombo cha utekelezaji wa Mpango Mpya wa Maendeleo wa mwaka 2016-2020, ambao ni mrithi wa Mpango wa zamani wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini MKUZA II, ambao umemaliza muda wake mwaka 2015. Aidha, ni chombo cha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 pamoja na Dira ya Maendeleo ya 2020 na Malengo Endelevu ya Dunia "*Sustainable Development Goals".*

Hivyo, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba siku zote inakuwa makini katika kupanga bajeti na mipango inayokwenda sambamba na Mipango hiyo ya Kitaifa na Kimatifa. Kwa upande mwengine, Wajumbe wa Baraza pia kwa niaba ya Wananchi wana jukumu zito la kuhakikisha wanaisimamia Serikali ipasavyo ili kuhakikisha kwamba rasilimali za Taifa zinatumika ipasavyo na kuyafikia matarajio ya wananchi. Pia, kuwa tayari kuwachukulia hatua kwa mtu yeyote ambae atakwenda kinyume na malengo yaliyopitishwa na Baraza hili kupitia Ilani ya Uchaguzi na malengo ya Milenia na muongozo wa Mheshimiwa Rais alioutoa wakati wa uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na ukweli kwamba bajeti yoyote lazima iwe na vipaumbele kwa mujibu wa malengo ya nchi na uwezo wa mapato, hata hivyo, bajeti lazima izingatie kwa kiasi gani itaweza kuwanufaisha wananchi wake, kwa kuwafikishia mahitaji ya msingi zikiwemo huduma muhimu za kimaisha. Hivyo, ni matarajio ya wananchi kwamba bajeti hii itaweza kuwandolea kero hizo na kufikia matarajio yao. Pamoja na kwamba wananchi wote wa Zanzibar wamejenga matumaini makubwa ya maendeleo ya haraka kupitia Serikali yao hii ya Awamu ya Saba.

Lakini cha kusikitisha ni kwamba kumeanza kujitokeza baadhi ya watu wachache ambao kwa roho zao mbaya wameanza kufanya vitendo vya hujuma na kuwasusia wananchi wenzao kuwapatia huduma kama vile huduma za usafiri, kuwauzia bidhaa, kuwatenga kwenye ibada na hata baadhi yao kuisusia misaada inayopelekwa na viongozi wao wa majimbo. Hii ni dalili mbaya kwa nchi yetu, kwa hiyo, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa umoja wetu tunalaani vitendo hivyo na tunaitaka Serikali kuvikemea na mtu yeyote atakaehusika na vitendo hivyo Serikali iwachukulie hatua kali za kisheria ili iwe funzo kwa wengine.

Aidha, kamati yetu inalaani wale wote wanaohamasisha wananchi wasusie ulipaji wa kodi, tunasema kwamba hakuna nchi inayoweza kuendelea bila ya

wananchi wake kulipa kodi, inashangaza zaidi kwamba miongoni mwa hao wanaowashawishi wananchi kususia ulipaji wa kodi ndio ambao wananufaika na mafao yao kuliko wana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Naiomba Serikali iwaangalie kwa jicho kali ili hatua za haraka zichukuliwe dhidi yao.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo mfupi naomba sasa nianze kutoa maoni ya Kamati kuhusiana na Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Uchumi wa mwaka 2016/2017.

Ukuaji wa Uchumi

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa juhudi inazozichukuwa ambazo zimepelekea kukuwa kwa uchumi kwa asilimia 6.6 kwa mwaka 2015. Taarifa ya Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 inaonyesha uchumi wa Zanzibar unaendelea kuimarika ukilinganisha na wastani wa ukuaji wa uchumi wa nchi zinazoendelea, nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na nchi zilizo katika Kanda ya Afrika Mashariki, ingawaje kuna upungufu kidogo ukilinganishwa na wastani wa ukuaji wa uchumi kwa asilimia 7.0 kwa mwaka 2014. Aidha, Kamati yangu inaishauri Serikali iongeze mikakati kuhakikisha kwa mwaka wa fedha 2016/2017 asilimia ya ukuaji uchumi inaongezeka zaidi ili kuweza kufukia lengo la Dira ya Maendeleo ya 2020 ya kufikia ukuaji wa uchumi endelevu wa asilimia 8 hadi 10 na kuweza kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi.

Pato la Taifa na Pato la Mtu mmoja mmoja

Mhe. Spika, Waraka wa Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016/2017 unaonyesha pato la mwananchi mmoja mmoja limekuwa licha ya kutoakisi hali halisi ya kiuchumi kwa wananchi wa kawaida. Kwa uchambuzi mdogo uliofanywa na Kamati yangu, imebainika kuwa hali hii inasababishwa na bajeti nyingi zinazoidhinishwa na Baraza hili tukufu kuwa na fedha chache zilizotengwa kwa shughuli za maendeleo ambazo zinawagusa wananchi moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, takwimu za Mapitio ya Hali ya Uchumi zinaonyesha Pato halisi la Taifa kwa mwaka 2015 limeongezeka hadi kufikia Tsh. 2,308 bilioni ukilinganisha na thamani ya Tsh. 2,133.5 bilioni kwa mwaka 2014. Wastani wa pato la mtu binafsi limeongezeka kufikia Tsh 1,632,000 sawa na Dola za kimarekani 817 kwa mwaka 2015 kutoka Tsh. 1,552,000 sawa na Dola za

Kimarekani 939 kwa mwaka 2014. Pamoja na ukuaji ambao unaonekana katika takwimu hizi bado tuko mbali kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020 ambayo imelenga kufikia Dola 995 ifikapo mwaka 2015 na Dola 3000 ifikapo mwaka 2020. Aidha, kutokana na kupanda thamani ya Dola pato hilo limeonekana kushuka katika uhalisia wake. Suala hili ni lazima Serikali zetu hizi mbili zikae kuangalia namna ya kudhibiti upandaji wa thamani wa Dola na kutafuta namna ya kudhibiti hali hiyo.

Mfumko wa Bei

Mhe. Naibu Spika, Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali mfumko wa bei wa dunia umeshuka kutoka asilimia 3.5 mwaka 2014 hadi 3.3 mwaka 2015. Aidha, mfumko wa bei wa nchi zinazoendelea ulishuka kufikia wastani wa asilimia 0.3 mwaka 2015 kutoka asilimia 1.4 mwaka 2014. Kwa upande wa Mfumko wa bei wa Zanzibar umepanda kwa wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2015 kutoka asilimia 5.6 mwaka 2014.

Mhe. Naibu Spika, mbali na kupanda kwa asilimia ndogo sana, bado Zanzibar hatujafanya vizuri katika eneo hilo ukilinganisha na mfumko wa bei wa dunia pamoja na nchi zinazoendelea ambao unaonyesha kushuka zaidi. Aidha, hatujaweza kufikia malengo ya *MKUZA II* ambayo yalilenga hadi mwaka 2015 tuwe na mfuko wa bei wa asilimia 5.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mfumko wa bei wa Zanzibar kwa kiasi kikubwa unaathiriwa na kupanda kwa bei za bidhaa za chakula, Kamati yangu inaishauri Serikali kuweka mkakati madhubuti ili kuhakikisha inakuza uzalishaji wa ndani kwa lengo la kupunguza mahitaji ya bidhaa hizo kutoka nje ya kisiwa cha Zanzibar.

Thamani ya Sarafu

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Serikali thamani ya Sarafu ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani iliendelea kushuka kwa asilimia 20.8 mwaka 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2014. Ambapo kwa mwaka 2014 Dola ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa TSh. 1,653 na kwa mwaka 2015 Dola ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa TSh. 1,997. Miongoni mwa sababu zinazotajwa kusababisha kushuka kwa sarafu ya Tanzania ni kuwepo kwa mahitaji makubwa ya Dola kutokana na kupungua misaada ya kibajeti *(GBS),* kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya biashara

ambayo yamepelekea kuagiza bidhaa zaidi kutoka nje ya nchi kuliko bidhaa ambazo tunauza nje ya nchi, na kuimarika kwa Dola ya Marekani dhidi ya sarafu ya nchi nyengine duniani.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaishauri Serikali kuweka mikakati imara ili kuweza kukabiliana na baadhi ya sababu zinazopelekea kushuka kwa sarafu ya Shillingi ikiwemo kukuza uzalishaji wa bidhaa za ndani na kudhibiti matumzi ya Dola yasiyo ya lazima kwa miamala ya ndani ya nchi. Pia, kutokana na funzo kutoka kwa wahisani kuendelea kupunguza kwa kiasi kikubwa misaada kutoka kwao. Kamati yangu inaishauri Serikali kuandaa mikakati ya kuwajenga na kuwawezesha wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani kwa kuweka mfuko maalum wa wawekezaji kwa lengo la kuwajenga kimitaji ili waweze kuanzisha na kuimarisha miradi yao ambayo itaweza kusaidia kutoa ajira na kulipa kodi mbali mbali ambazo zitapunguza nakisi ya utegemezi wa misaada kutoka nje. Na mfano mzuri ni kwa nchi ya Rwanda ambayo imeweka mfumo mzuri kwa wawekezaji ambapo imesaidia sana kuongeza mapato lao la ndani ya ndani.

Mhe. Naibu Spika, ili kupunguza utegemezi kutoka nje, Serikali ni lazima ifanye utafiti mkubwa kwa wawekezaji wenye Mahoteli ya kitalii, kwani kuna tuhuma nyingi kwamba wageni wao hufanya malipo nje ya nchi na kuisababishia Serikali kukosa kodi yake. Hivyo, tunaishauri Serikali imtafute Mshauri Elekezi ‘Consultant’ ili afanye utafiti na kutuletea taarifa sahihi kuhusu malipo ya wageni wanaokuja nchini na kukaa kwenye mahoteli ya kitalii ili kujuwa utalii wetu unatusaidia vipi isiwe tunalalamika tu eti mapato yanapotea. Kwani kuna baadhi ya nchi za visiwa kama sisi wanapata mapato makubwa sana kupitia utalii na yamesaidia sana kuimarisha kuinua nchi zao kulinganisha na sisi.

Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini MKUZA II

Mhe. Naibu Spika, tukiwa tumekamilisha muda wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini MKUZA II wa mwaka (2010-2015). Serikali imo katika hatua za mwisho za matayarisho ya Mpango Mpya wa Maendeleo wa Miaka mitano 2016-2020 ambao ni mrithi wa MKUZA II. Ni vyema Serikali ikatueleza ni kwa kiasi gani utekelezaji wa MKUZA II umefanikiwa, na changamoto gani ambazo zilikwamisha utekelezaji wa MKUZA II kwa maeneo ambayo malengo hayakufikiwa, na changamoto ambazo zitazingatiwa na kutatuliwa katika Mpango Mpya wa Maendeleo ambao baadhi ya Wajumbe wako bado hatujauelewa. Hasa tukizingatia kwamba Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/2017 umezingatia Mkakati huo mpya wa Maendeleo wa mwaka 2016-2020.

Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana

Mhe. Naibu Spika, katika taarifa ya Serikali ya Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka wa fedha 2015/2016, moja kati ya maeneo ya vipaumbele ni Kuendeleza Programu za Kukuza Ajira kwa Vijana, hata hivyo, hadi mwezi Machi 2016 programu hii haikuweza kupatiwa fedha. Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa suala la ajira katika maendeleo ya nchi, lakini pia kwakuwa ni eneo la kipaumbele, Kamati yangu inashauri Serikali kuweka mikakati imara kwa yale maeneo ambayo wameyatenga kuwa vipaumbele kuhakikisha yanapatiwa fedha kwanza, kwani kuyakosesha fedha ni kwenda kinyume na mipango yake iliyojiwekea wenyewe. Moja katika suala la kuongeza ajira kwa vijana ni kuwawezesha wawekezaji wa ndani.

Mhe. Naibu Spika, Taarifa ya Serikali haijaelezea kwa kiasi gani tumeweza kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa mujibu Malengo *ya* MKUZA II na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020 kiasi ambacho tunashindwa kupima ufanisi wa utekelezaji wake. Hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri, alieleze Baraza hili ni kwa kiwango gani tumeweza kutatua tatizo la ajira kwa mujibu wa MKUZA II na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020.

Sekta ya uvuvi

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa sekta ya uvuvi Kamati inaipongeza Wizara husika na Serikali kwa ujumla kuhusiana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa katika kuimarisha uvuvi wa bahari kuu kwa kuwapatia mafunzo baadhi ya wavuvi kuhusiana na uvuvi huo, licha ya changamoto za kitaaluma zinazotokana na kiwango cha elimu cha wavuvi hao. Katika bajeti hii na mipango ya Serikali, uvuvi bado hauonekani kupewa kipaumbele kutokana na uhalisia wa kijografia wa Zanzibar wa kuzungukwa na bahari, kama nchi ambayo uchumi wake mkubwa unategemea rasilimali hiyo ya bahari.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwajali wavuvi waliopo nchini ilianza zoezi la kutoa maboti kwa wavuvi hao. Kamati ya Wenyeviti inataka kujua ni jambo gani lililokwamisha zoezi lile muhimu kwa maendeleo ya wavuvi wetu? Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, Kamati yangu inataka kujua yamefikia wapi kiutekelezaji mazungumzo kuhusiana na masuala ya uvuvi kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Vietnam?

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaitaka Serikali pia katika eneo hili la uvuvi kumtafuta mshauri elekezi atakaetushauri vizuri namna ya kuimarisha uvuvi hapa Zanzibar ikiwemo kuvua katika bahari kuu pamoja na kuanzisha viwanda vya kusindika samaki. Kwani eneo hili likiimarishwa litaweza kuipatia Zanzibar samaki wa kutosha na wengine kuuza nje ili kuongeza mapato, lakini pia kupata fedha za kigeni na kuongeza ajira kwa vijana wetu.

Sekta ya Kilimo

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi sio tu kwa Zanzibar lakini kwa nchi nyingi hususan nchi zinazoendelea. Uzalishaji wa bidhaa hususan mazao ya chakula katika nchi yetu umeshuka. Hali hii itachangia nchi yetu kuzidi kutegemea uagizaji wa mazao ya chakula kutoka nje ya nchi, hali ambayo sio nzuri sana kiuchumi lakini pia kiusalama wa nchi. Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuwepo na sababu nyingi zinazoweza kuhusiana na upungufu huo, ukiacha wizi wa mazao ambao hurejesha nyuma sana jitihada za wakulima. Kamati yangu inaamini bado nchi yetu haijaweka mikakati imara ya kudhibiti maeneo ya kilimo ambapo maeneo mengi ya kilimo ambayo kwa miaka mingi yamekuwa yakitoa mazao mengi ya kilimo, hivi sasa yamevamiwa na kugeuzwa makaazi ya watu kwa ujenzi wa nyumba holela, na Serikali imekaa kimya.

Kwa hivi sasa hata maeneo yaliyokuwa mabonde ya mpunga hususan katika Mkoa wa Mjini na Magharibi pia yamejengwa nyumba za kuishi na miongoni mwao nyakati za mvua hujaa maji na kuathiri maisha na mali za watu, Kamati yangu inaishauri Serikali kuweka mikakati imara kuyalinda maeneo ya kilimo yakiwemo maeneo ya eka. Aidha, Serikali ihamasishe zaidi wananchi kulima mazao ya chakula pamoja na kuwaandalia masoko ili waweze kuwa na uhakika wa kuuza mazao yao ili tija ya nguvu zao wanazozitumia ipatikane.

Pia, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo iwahamasishe na kuwa karibu na wakulima wa mazao ya mboga mboga kwani zimekuwa na soko kubwa katika mahoteli ya kitalii, na kupunguza uagiziaji wa mboga mboga kutoka Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, ningependa pia nigusie suala la kilimo cha mwani ambacho kiuhalisia kimetoa ajira kwa wananchi wengi hususan kina mama wanaoishi karibu na maeneo ya ufukwe. Mhe. Naibu Spika, kwa sasa kilimo cha mwani kimeshuka thamani kwa kiasi cha kuwavunja moyo wakulima wa kilimo hicho, kutokana na bei ya mwani kushuka kutoka shilingi 700 hadi 300 kwa kilo moja kwa sasa. Katika kuimarisha zao hili na uchumi kwa ujumla, Kamati yangu,

inashauri Serikali kuwekeza kwa kuanzisha kiwanda ambacho kitasarifu mwani ili kuengeza thamani ya zao hilo na kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika**,** Changamoto nyengine iliyobainika na Kamati ni udanganyifu unaofanywa na wanunuzi wa mwani katika usafirishaji wa mwani huo, kwa kutaja idadi pungufu ya kilo za mwani wanaosafirisha. Hali hii inasababishwa kwa kukosekana kwa kifaa maalum cha kupimia uzito huo na kuwapa mwanya wanunuzi hao kuendelea kujinufaisha zaidi. Kamati yangu katika kuondoa tatizo hili, inaomba kinunuliwe kifaa hicho pamoja na kuitaka Serikali kupitia Shirika la Taifa la Biashara - *ZSTC* kununua mwani huo kutoka kwa wakulima kama ilivyo kwa zao la karafuu ambalo kwa sasa angalau wananchi wameanza kufaidika nalo.

Mhe. Naibu Spika, tunafahamu kwamba Serikali kupitia Shirika la Biashara la Taifa - *ZSTC* inatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya ununuzi wa zao la Karafuu. Ambapo ilitarajiwa mzunguko wa fedha hizo urejee katika benki za ndani hususan Benki ya Watu wa Zanzibar - *PBZ*, lakini pia manufaa yake yaonekane katika maeneo ya jamii ikiwemo ujenzi wa majengo ya kisasa hasa katika maeneo ambayo fedha hizo zimetumika zaidi.

Hata hivyo, kutokana na fedha ambazo zimetumika bado mafanikio yake katika Benki ya *PBZ* pamoja na maendeleo ya majengo ni madogo sana. Jambo hili huenda likachangiwa na wananchi wengi kuhifadhi au kuwekeza fedha zao nje ya Zanzibar. Kamati yangu inaishauri serikali kulifanyia utafiti suala hili, na kuwahamisisha wananchi kuwa wazalendo kwa kuitumia Benki ya Watu wa Zanzibar pamoja na kuwekeza ndani ya nchi kwa kuwawekea mazingira rafiki ili mzunguko wa fedha hizo unufaishe nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, tunalipongeza Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*) kwa juhudi iliyochukua la kuzuia magendo ya karafuu. Hata hivyo, tunaliomba shirika hili lizidishe juhudi hizo kwani baadhi ya wananchi wasiopenda maendeleo ya nchi hii wanaendelea na harakati za kusafirisha karafuu kinyume na utaratibu.

Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaipongeza Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar - *ZIPA* kwa jitihada zao wanazozichukuwa katika kuhamasisha wawekezaji hususan katika Sekta ya Utalii. Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaisisitiza mamlaka hayo na serikali kwa ujumla kufanya jitihada zaidi kuwawekea mazingira rafiki wawekezaji ikiwemo kuwawekea

miundombinu ya uhakika pamoja na kujitangaza zaidi kibiashara ili kuwavutia wawekezaji, hususan kwa miradi yenye thamani kubwa ambayo itaipatia serikali mapato mengi na kutoa nafasi kubwa ya ajira kwa wananchi. Aidha, uwepo wa miradi mikubwa itaijengea sifa na kuitangaza nchi yetu zaidi kibiashara, mfano hoteli kubwa za nyota tano, "*Five Stars Hotel*".

Mhe. Naibu Spika, kwa kusisitiza hilo ni vyema kuangalia uwezo wa mitaji ya wawekezaji wanaokuja na kuwapa maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Kwani kuna ardhi nyingi ambayo walipewa madalali ambao imekaa bure bila ya kuekezwa kwa miaka mingi jambo ambalo limeinyima fursa Zanzibar ya kupata mapato zaidi. Kamati yangu inaitaka *ZIPA* pamoja na Idara ya Ardhi kuyarejesha serikalini maeneo yote waliyopewa wanaojifanya wawekezaji ambao hadi leo wameshindwa kuwekeza na kuwapa wengine wenye uwezo wa kuwekeza ili nchi yetu iongeze mapato na kuongeza ajira.

Mhe. Naibu Spika, tunaipongeza serikali na mikakati yake madhubuti ya kuanzisha mradi wa kijiji katika eneo la Fumba. Pamoja na pongezi hizo, tunaiomba serikali isimamie vyema mikakati hiyo ili iweze kuleta tija iliyokusudiwa.

Ukusanywaji wa Kodi ya Ardhi

Mhe. Naibu Spika, katika Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za SMZ kwa mwaka wa fedha 2011/2012, pamoja na Ripoti ya Ukodishwaji wa Ardhi kwa Wawekezaji ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuanzia ukurasa wa 56 hadi 77 wa ripoti hiyo iliorodheshwa miradi iliyopatiwa ardhi ambayo haijafanyiwa mapitio. Vile vile, katika ukurasa wa 78 hadi 84 iliorodheshwa miradi ambayo imesajiliwa lakini hailipi kodi ya ardhi. Aidha, kutoka ukurasa wa 107 hadi 113 yameorodheshwa maeneo ya wawekezaji ambayo hayajaingizwa katika mtandao wa ulipaji kodi ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, Kamati ya *PAC* katika ripoti yake ya mwaka 2013/2014 iliyowasilishwa mbele ya Baraza hili mnamo mwezi wa Januari, 2014 ilieleza kuwa yapo maeneo ya ardhi ambayo yamekodishwa kwa wawekezaji lakini wawekezaji hao hawakuyaendeleza maeneo hayo kama walivyoomba, vile vile, wawekezaji hao hawalipi kodi yoyote ingawa wanaendelea kuyatumia maeneo hayo kwa matumizi mengine.

Mhe. Naibu Spika, mfano wa mwekezaji huyo aliyetajwa na kamati hiyo ni Kampuni ya Mpapindi *Holiday and Diving* iliyopo Pemba ambayo ilipatiwa ardhi tangu mwaka 2004 lakini hadi Kamati ya *PAC* imefanya uchunguzi wake

mnamo mwaka 2013 Kampuni hii haijaendeleza eneo hilo kwa madhumuni iliyoomba na badala yake inatekeleza shughuli nyengine pasipo kulipa kodi yoyote. Kwa ujumla Kamati ya *PAC* ilieleza kuwa hadi mwaka 2013 Kampuni hiyo ya Mpapindi inadaiwa *USD* 391,352.00 pamoja na adhabu.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo utaungana na kauli iliyotolewa na Kamati ya Wenyeviti kuwa zipo baadhi ya Taasisi za Serikali zinashindwa kusimamia vyema majukumu yake hususan kwenye upande wa ukusanyaji wa mapato. Kitendo ambacho huikosesha mapato nchi yetu na kuendelea kutegemea misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo wakati endapo watendaji wetu wangesimamia vyema majukumu yao tungeondokana kabisa na mfumo huo. Kwa msingi huo, kamati yangu inataka kujua hatua zilizochukuliwa na serikali kupitia Mamlaka ya Vitega Uchumi na Wizara inayohusiana na mambo ya ardhi baada ya Mdhibiti kuzibaini kasoro hizo pamoja na maoni mbali mbali yaliyotolewa na Kamati ya *PAC* kuhusiana na hoja hizo.

Huduma ya Maji Safi na Salama

Mhe. Naibu Spika, huduma ya maji safi ni muhimu sana katika afya na usalama wa wananchi, tunaipongeza serikali kupitia Mamlaka ya Maji, *ZAWA* kwa jitihada zao wanazozichukuwa za kuwafikishia huduma hii wananchi. Kamati yangu inashauri Mamlaka ya Maji kuendeleza juhudi hizo za kuwafikishia wananchi huduma hiyo kwa yale maeneo ambayo bado hayajafikiwa na huduma hiyo hususan katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaamini bado *ZAWA* haijaweka mkakati na mazingira rafiki katika utaratibu wao wa ukusanyaji wa malipo ya maji. Hivyo, tunaishauri mamlaka hiyo kuchukua jitihada za kuwahamasisha wananchi kulipia huduma hiyo ili iwe endelevu, pamoja na kuongeza vituo vya malipo ya maji, sambamba na kufanya mazungumzo na kampuni za simu ili huduma hiyo iweze kulipwa kwa njia ya mtandao.

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa wananchi wanalazimika kufuata vituo vya malipo masafa marefu ambayo mbali ya usumbufu wa muda, pia gharama wanazotumia ni kubwa ukilinganisha na fedha wanayokwenda kulipia ankara (*bill*) ya maji. Pia, kamati yangu inaitaka Mamlaka ya Maji kuendelea na utaratibu wa kuyabadilisha mabomba ya maji ya zamani (*asbestos*), kwani mabomba hayo mengi yameanza kuwa mabovu na kusababisha maji mengi kuvuja na kupotea njiani bila ya kuwafikia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaitaka Mamlaka ya Maji kuendelea na zoezi la kufunga mita za maji kwa maeneo ya biashara ili wateja hao waweze kulipia gharama ya maji kwa mujibu wa matumizi yao. Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Wenyeviti imebaini kuwa zoezi la ufungaji wa mita za maji limesita siku nyingi. Hivyo, kamati hii inataka kujua ni jambo gani limekwamisha zoezi hilo muhimu kwa maendeleo ya mamlaka hii.

Sekta ya Afya

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nigeukia upande wa sekta ya afya ambayo kwa ujumla kamati inaipongeza Wizara ya Afya na Serikali kwa ujumla, kwa kujitahidi kufanya kwa kuyafanyia ukarabati majengo ya hospitali na kuongeza majengo mapya, dawa na vifaa tiba, japo kwa ujumla bado havijakidhi mahitaji ya hospitali zetu. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja wapo wataalamu wanaofanya matengenezo ya vifaa vya watu wenye ulemavu kama vile miguu ya bandia na kadhalika. Kwa vile vifaa hivi vinahitajika kwa asilimia kubwa, na kwa kuwa watu wenye ulemavu hutumia gharama kubwa kuvitafuta vifaa hivi zaidi Tanzania Bara. Kamati ya Wenyeviti inaishauri serikali kuanzisha kitengo maalum cha kuandaa vifaa hivi badala ya kuvifanyia matengenezo pekee ili kuwaondoshea usumbufu watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na mripuko wa maradhi ya kipindupindu kamati pia inachukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Afya kwa jitihada wanazochukua za kupambana na maradhi haya, kwani kiuchumi sio tu yamepunguza nguvu kazi ya Taifa lakini pia imezorotesha sekta ya elimu na sekta ya utalii ambazo idadi yao imepungua kutokana na mripuko wa maradhi haya. Aidha, kamati inashauri kuwa imefikia wakati sasa wizara kuanzisha kambi mpya ya wagonjwa wa kipindupindu ambayo itakuwa kubwa, ya kisasa na ambayo itakayokuwa mbali na makaazi ya watu, kwani kwa sasa kambi ya wagonjwa wa kipindupindu iliyopo katika Jimbo la Chumbuni inahatarisha usalama wa afya ya wakaazi wa eneo hilo na wanaoishi jirani.

Mhe. Naibu Spika, tunashauri hili kwa kuwa Kituo cha Afya cha Chumbuni kilichokuwa kinatoa huduma kwa wananchi wa maeneo ya Karakana, Chumbuni, Mwembemakumbi, Maruhubi, Mtopepo, Mtoni Kidatu, Masumbani, Bamita, *Kotex* kinavyopangiwa kuhudumia wagonjwa wa kipindupindu huwa hakitowi tena huduma za afya za kawaida. Kitendo ambacho kinawapa mzigo mkubwa wananchi wa maeneo niliyoyataja kufuata huduma ya afya katika vituo vyengine vya mbali na makaazi yao.

Mhe. Naibu Spika, licha ya kuongezeka kwa hospitali za watu binafsi, na kuongezeka kwa madaktari kama tulivyoelezwa na Mhe. Waziri, bado tuna changamoto ya kuongezeka kwa wagonjwa wanaohitaji kupelekwa nje ya nchi kila mwaka, kwa ajili ya kupatiwa matibabu zaidi, wakiwemo viongozi wa kitaifa, jambo hili huilazimu serikali kutumia gharama kubwa. Mhe. Naibu Spika, hadi tunawasilisha taarifa hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakadiriwa kudaiwa jumla ya *USD* 1 milioni zimetumika kwa ajili ya gharama za matibabu ya nje ambapo fedha hizi zinaweza kuongezeka maradufu kwani baadhi ya wagonjwa wanaendelea kupatiwa matibabu kwa mkopo.

Mhe. Naibu Spika, katika kuongeza wigo wa sekta ya afya ambao pia utaongeza pato la taifa, kuipunguzia serikali gharama na kupunguza tatizo la ajira. Kamati inaishauri serikali kwa kushirikiana na Kitengo cha *PPP* kutafuta muwekezeji mkubwa ambae atakuwa tayari kujenga hospitali kubwa ya kimataifa ambayo itakuwa na uwezo wa kupokea wagonjwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya "*Medical Tourism*" na kutoa huduma ambazo zitakuwa nafuu hata kwa wananchi wa kawaida. Mhe. Naibu Spika, hili linawezekana iwapo muekezaji huyo atapatiwa msamaha wa kodi kwa baadhi ya maeneo kama uingizaji wa vifaa ikiwezekana hata kodi ya ardhi.

Sekta ya Elimu

Mhe. Naibu Spika, katika mapendekezo ya kamati ya mwaka 2016/2017, suala la kuimarisha huduma za kijamii limewekwa kipaumbele, ikiwemo upatikanaji wa elimu bora. Kwa kuwa kumekuwa na tatizo kubwa katika upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wanaosoma masomo ya elimu ya juu kutokana na wingi wa mahitaji usiokwenda sambamba na fedha inayotengwa kwa ajili ya mikopo hiyo. Sambamba na urejeshwaji mdogo sana wa mikopo iliyotolewa, ambapo kamati yangu iliarifiwa kwamba kuanzia mwaka 2011 hadi 2015 jumla ya Tsh 25.2 bilioni zimetolewa mikopo kwa wanafunzi, ambapo kuanzia mwaka 2013 mikopo iliyorejeshwa ni Tsh 1.4 bilioni tu.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, kamati yangu inaishauri Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar, ishirikiane na taasisi nyengine katika kufanikisha urejeshaji wa mikopo hiyo. Ili fedha hizo ziweze kuwasaidia na wanafunzi wengine pamoja na kuifanyia marekebisho Sheria ya Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu Nam. 3 ya mwaka 2011, hususan kwenye kifungu cha 24(2) kinachotoa mamlaka kwa bodi kutoa maelekezo ya namna ya kurejeshwa mkopo baada ya mkopeshwaji kuajiriwa.

Mhe. Naibu Spika, kamati hii inapendekeza muda huo iwe mwaka mmoja tu bila ya kujali kama mkopeshwaji ameshaajiriwa au la. Hapa tunamaanisha kuwa endapo mkopeshwaji atakuwa hajaajiriwa hadi mwaka mmoja unamalizika, jukumu la kulipiwa fedha hizo lichukuliwe na mdhamini wake. Tunashauri hili kwa kuwa fedha hizi zinatengwa kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi wote wanaohitaji kusoma na imebainika kuwa kwa utaratibu uliopo hivi sasa baadhi ya wakopeshwaji wa fedha hizi wataendelea kulipa mkopo huo hadi wanastaafu kazi.

Sambamba na hilo, tunaishauri Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu kufanya ziara ya mafunzo katika Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kujua mbinu ambazo bodi hiyo inazitumia kwa lengo la kuwabana wakopeshwaji ili kulipa mikopo yao kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi, Kamati yangu inaishauri Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*), kuendelea na azma yake ya kuwapatia mikopo wanafunzi wanaohitaji huduma hiyo. Vile vile, serikali ichukue jukumu la kuwahamasisha mabenki mengine kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanafunzi, ili kuweza kuendelea na mafunzo yao ya elimu ya juu.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine inayoikabili wizara hii kupitia suala la mikopo ni kuwanyima baadhi ya wanafunzi mikopo hiyo kwa kigezo cha fani wanazosoma, ambapo kwa sasa sayansi tu ndio imekuwa kipaumbele kikubwa katika kupatiwa mikopo hiyo. Kamati yangu katika hili ina mtazamo tofauti kidogo, kwani kwa sasa ulimwengu unakoelekea unahitaji wataalamu wa fani tofauti na sio sayansi pekee. Kamati inaishauri mamlaka husika kuliangalia suala la uhitaji wa wataalamu kuwa ni suala la kiulimwengu na sio la nchi moja tu.

Hivyo, hata kama wataalamu hao watafanyakazi nje ya nchi bado faida za kiuchumi zitapatikana katika nchi yetu kupitia kwa wataalamu hao. Sambamba na kuvitia moyo vyuo vya hapa nchini kwani vinaendelea kufundisha masomo tofauti, kwa hiyo, ni lazima kuwe na mkakati maalum wa kuwapa mikopo wote wanaohitaji. Hatua hii itawatia moyo wale wanafunzi wanaosoma masomo ambayo sio ya sayansi.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni Wizara ya Elimu imeanzisha mfumo mpya wa elimu ambapo mwanafunzi anaemaliza darasa la sita anatakiwa kuendelea moja kwa moja darasa la tisa, ambapo kiujumla atakuwa kapunguza miaka miwili (madarasa mawili). Pamoja na nia nzuri za kutaka kuimarisha mfumo wa elimu

yetu bado mfumo huu unatia shaka kutokana na ukweli kwamba wanafunzi wetu wakati wanapomaliza darasa la kumi na mbili wanakuwa bado wadogo sana na uwezo wao pia unakuwa ni mdogo kulingana na darasa wanalotakiwa kusoma. Hii ni kutokana na mitaala ya elimu ya madarasa ya awali hayajaweza kuwajenga mihimili katika masomo ya juu ipasavyo. Aidha, umri wao na ufahamu kiujumla bado unakuwa mdogo hususan anapomalizia darasa la kumi na mbili.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuwa baadhi ya nchi zinatumia mfumo huu lakini kuna mambo mengi ambayo yanaweza yakasababisha mfumo huu usiwe na tija kwetu. Kwa msingi huo, Kamati yangu inaishauri serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ifanye tathmini ya kina kuhusu ubora na mapungufu ya mfumo huo, kwani huenda ikawa athari yake ni kubwa kuliko manufaa kwa mujibu wa mazingira ya nchi yetu. Pia, kamati yangu inaishauri serikali kupitia Wizara ya Elimu kuanzisha mitaala ya elimu ya amali ili kumuandaa kijana wetu akimaliza masomo ya Sekondari aweze kuwa na ujuzi ili kumuandaa kujitegemea hapo baadae.

Mhe. Naibu Spika, Sera ya Elimu ya Zanzibar inaelekeza kuwa, mwanafunzi yeyote anatakiwa kuanza darasa la maandalizi '*nursery'*, hata hivyo, hali halisi inaonesha kuwa bado serikali haiko tayari kutekelezwa kwa sera hiyo. Hii ni kutokana na kuwa ni skuli chache za serikali ambazo zina skuli ya maandalizi. Mhe. Naibu Spika, katika kuthibitisha hili, Kamati ya Wenyeviti inamtaka Mhe. Waziri kulieleza Baraza hili ni skuli ngapi za serikali Unguja na Pemba ambazo zina skuli za maandalizi na skuli ngapi hazina skuli hizo.

Mhe. Naibu Spika, imezoweleka kuwa Skuli ya Mwanakwerekwe 'C' hutumiwa na serikali kuwahifadhia wananchi wanaokabiliwa na janga la mafuriko wakati wa mvua kubwa. Kwa kuwa wanafunzi wanaosoma skuli hii hupata usumbufu mkubwa ikiwemo wa kuhamishiwa skuli nyengine na kusoma siku tatu kwa wiki, na kwa kuwa skuli wanazohamishiwa wanafunzi wa skuli hii pia husoma siku nne kwa wiki. Kamati ya Wenyeviti inaiomba serikali kulitafutia ufumbuzi wa kudumu wa suala hili haraka iwezekanavyo ili kuwaondoshea usumbufu usio wa lazima watoto wetu hawa na walimu wao kwa kutenga eneo maalum kwa kadhia hii.

Mhe. Naibu Spika, pia, kamati hii inaishauri serikali kuunda Kamati maalum itakayosimamia vibali vya ujenzi pamoja na kusimamia maeneo ya vianzio vya maji, mabonde ya mpunga na kufuatilia maeneo ya eka tatu yaliyotolewa kwa ajili ya kilimo. Tunashauri hili kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na ujenzi wa kiholela katika maeneo mengi ya Zanzibar.

Vyuo vya Amali

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika kitabu cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi 2016 na Mpango wa Maendeleo 2016/2017 kwenye ukurasa wa 34 imeelezwa kuwa serikali imedhamiria kujenga vituo viwili vya Mafunzo ya Amali kimoja Makunduchi na kimoja Daya Mtambwe. Kamati yangu inaipongeza azma hiyo, hata hivyo, imebainika kuwa bado kuna muitikio mdogo kwa wananchi katika kuvitumia Vyuo vya Amali vilivyopo na bado serikali inaendelea kuvijenga vyuo hivyo. Kutokana na kasoro hiyo, kamati hii inaishauri serikali kuendelea kuwahamasisha wananchi kuvitumia vyuo hivi hasa ikizingatiwa kuwa serikali haina uwezo wa kuajiri wananchi wake wote. Pia, tunaishauri serikali kuviimarisha zaidi vyuo vilivyopo ili viweze kutoa wahitimu wenye fani mbali mbali.

MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nitowe maoni ya kamati yangu katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii ni bajeti ya kwanza katika Baraza hili la Tisa, changamoto kubwa inayoikabili bajeti ya mwaka huu ni suala la kuongeza mapato pamoja na udhibiti wa mapato yatakayokusanywa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba upatikanaji wa michango ya Washirika wa Maendeleo imekuwa haina uhakika, hivyo kuendelea kuitegemea katika bajeti yetu kumekuwa kukiyumbisha mipango yetu na kupelekea kutokufikiwa kwa malengo tunayojiwekea.

Utumiaji wa Mashine za Kutolea Risiti (*Electronic Fiscal Devices - EFD*)

Mhe. Naibu Spika, suala la kuvuja kwa mapato na uwezo mdogo wa kukusanya mapato kwa vyombo vilivyopewa jukumu hilo pamoja na uchache wa vianzio vya mapato kwa ujumla, vimekuwa vikiipa changamoto kubwa Bajeti ya Serikali. Hivyo, tunalazimika kuwa na vyanzo vya mapato vya ndani vyenye kujitosheleza na vyenye uhakika, pamoja na kuwa na mikakati imara ya kudhibiti mapato yanayopatikana ili kupunguza utegemezi wa bajeti kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, moja kati ya eneo ambalo tumekuwa na changamoto kubwa ya kuvuja kwa mapato ni mfumo wa malipo kwa njia ya "*cash*". Pamoja na

serikali kueleza kuwa na nia ya kuondokana na mfumo huo kwa kuanzisha mfumo wa ulipaji kwa kutumia mashine za kutolea risiti za (*EFD*) ambapo kwa bajeti ya mwaka 2016/2017 imepanga kununua mashine 1,000 utekelezaji wa mpango huo umekuwa wa kusuasua. Hivyo, kamati yangu inaisisitiza serikali kuharakisha utumiaji wa mfumo huo katika maeneo mbali mbali ya biashara na utalii ambayo moja kwa moja yanahusika na ukusanyaji wa mapato. Kwani mfumo huu utasaida kupunguza tatizo la uvujaji wa mapato ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaishauri serikali kufanya utafiti kwanza kuhusu idadi ya wafanyabiashara kabla haijafanya ununuzi wa mashine hizi ili kujua mahitaji halisi ya mashine hizo. Aidha, kamati yangu inaishauri serikali wakati wa utekelezaji wake waanze kwa majaribio yaani "*pilot area*" ili kuona changamoto za utumiaji juu ya mfumo huo. Vile vile, kamati yangu inaishauri Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) wajifunze kwa wenzao wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ambao wameshaanza kutumia mfumo huo.

Sambamba na hilo, kama ambavyo ilishauri bajeti ya mwaka jana, kamati yangu inasisitiza ili kudhibiti uvujaji wa mapato, malipo ya ada zote katika huduma zinazotolewa na wizara na Taasisi za Serikali zilipwe kwa njia ya benki. Aidha, kamati yangu inasisitiza serikali kuachana na mfumo wa kulipia kwa "*cash*" kwa kuwa tayari mafanikio ya mfumo wa kulipia kwa njia ya *electronic* "*E-Card*" unaotumika katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar "*Airport*" umeonesha mafanikio makubwa kwa kuongezeka makusanyo maradufu. Iwapo tutaendelea na mfumo huu sehemu nyengine ni dhahiri tutaweza kuongeza mapato yetu kwa kiasi kikubwa. Pamoja na marekebisho hayo bado serikali kupitia Kamisheni ya Utalii inashauriwa kuwataka wageni wote wanaoingia nchini kufanya malipo yao kupitia mfumo huo ili kuzuia uvujaji wa mapato.

Mhe. Naibu Spika, eneo hili ikiwa tutalisimamia vizuri basi tunaweza kuvuka idadi ya lengo la ukusanyaji wa mapato tulilojitengea.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inashauri Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA)* na Zanzibar (*ZRB*) kukaa kwa pamoja kuondokana na mvutano baina ya *ZRB* na *TRA* katika kukusanya mapato ya *stamp duty*. Aidha, viwango vya ulipaji kodi hiyo ni tofauti baina ya Serikali ya Tanzania Bara na Serikali ya Zanzibar. Kamati yangu inashauri serikali ifanye mapitio ya Sheria za kodi na kuweka utaratibu mzuri ambao hautoleta utata katika ukusanyaji wa kodi hizo na kuweka wazi ni chombo kipi kati ya hivi viwili kina haki au malaka ya kukusanya kodi hiyo.

Sekta ya Utalii

Mhe. Naibu Spika, uchumi wetu kwa kiasi kikubwa unategemea mapato yatokanayo na Sekta ya Utalii. Hata hivyo, bado serikali haijaweka mikakati imara ya kuhakikisha kwamba mapato katika sekta hii yanakusanywa kwa ufanisi, kumekuwa na upotevu wa mapato katika sekta hii kutokana na mianya iliyopo ambayo kama itadhibitiwa serikali inaweza kuongeza sehemu kubwa ya mapato yake.

Mhe. Naibu Spika, takwimu zinaonesha kupungua kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini hali ambayo inazidi kupunguza mapato ya ndani ya serikali kupitia sekta hii. Ni ukweli usiofichika kuwa sekta ya utalii ni nguzo kuu na roho ya uchumi wetu na inaeleweka wazi kabisa kuwa wadau katika sekta hii wenye muamko wa Kiteknohama. Hivyo, kutokana na upotevu mkubwa wa mapato kupitia sekta hii, kamati inaishauri serikali iandae utaratibu mbadala wa ulipaji kodi kupitia sekta hii na iharakishe zoezi la utumiaji wa mashine za *Electronic Fiscal Devices* (*EFD*), ambazo Mhe. Naibu Spika, mjadala wake umeshakuwa wa muda mrefu. Mbali na hilo, serikali na mamlaka husika ziimarishe utaratibu wa kukusanya takwimu za wageni wanaongia nchini, kwani inaaminika kuwa, Zanzibar inapokea wageni wengi zaidi ya ambao takwimu zetu zinaonesha kwa sasa.

Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na udangayifu kwa baadhi ya mahoteli kuhusu idadi halisi ya wageni wanaopokea, hivyo, kodi kutozwa kinyume na uhalisia na kupelekea kuikosesha serikali mapato. Aidha, kuna baadhi ya wageni wanaingia nchini na kufungua Kampuni za "*Diving*" na kuajiri wataalamu kutoka nje, lakini viwango vya kodi vinavyolipiwa ni vidogo. Vile vile, hakuna utaratibu mzuri wa kufuatilia aina ya shughuli za kitalii ambazo zinafanywa ikiwemo "*Diving and Snorkeling*", ambazo kimsingi zinatofautiana katika malipo, hivyo na ulipaji kodi zake unapaswa kutofautina. Ni vyema kukaandaliwa utaratibu maalum wa kufuatilia ili kuhakikisha kwamba udhibiti wa mapato katika eneo hilo unaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hili, kuna suala la wageni wanaoishi nchini kwa vibali vilivokwisha muda wake na wale wanaofanya kazi nchini kinyume na sheria na kuikosesha serikali mapato. Kamati yangu inaishauri serikali isimamie sheria hii ili kila mgeni afanye kazi na kuishi nchini kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa. Aidha, serikali iweke mikakati ya ufuatiliaji katika sekta ya michezo ya baharini ya kitalii kwa kuweka mgawanyo maalum wa maeneo hayo kwa mujibu wa shughuli husika ili kuweka urahisi wa kufuatilia na ukusanyaji wa mapato. Kwa upande mwengine, kamati yangu

inaishauri serikali kuweka utaratibu wa kudhibiti uingizaji wa wageni kwa kufanya kazi kwa karibu na mashirika ya ndege na boti za kusafirishia abiria kwa kutumia "*manifesto*" zao pamoja na Idara ya Uhamiaji ambapo nakala ya orodha ya wageni wanaoingia nchini ipelekwe *ZRB* ili kujua idadi halisi ya wageni wanaoingia na kuepuka udanganyifu.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya wageni wamekuwa wanafanya udanganyifu kwa kushirikiana na wenyeji "*Tour*" kwa majina ya wenyeji, wakati umiliki wote na shughuli za uendeshaji yaani "*management*" ipo chini ya wageni, kitu ambacho ni kinyume na sheria, na kwa kiasi kikubwa hali hiyo inaikosesha mapato serikali. Ni vyema serikali ikasimamia utekelezaji wa sheria kwa kuhakikisha kwamba kazi ambazo haziruhusiwi kufanywa na wageni wasiachiwe kuzifanya ili kuweza kufikia malengo ya kuwasaidia wananchi wetu. Vile vile, kuna baadhi ya wafanyabiashara wengi wanaendesha biashara ya Utalii kupitia *"Tour Operator"* bila ya kulipia kodi.

Kamati yangu inaishauri serikali ihakikishe kwamba Jumuiya ya *ZATO* katika taratibu za usajili wa Kampuni za *"Tour Operators"* nayo inashirikishwa ambao wanaweza wakasaidia kwa karibu kuzitambua Kampuni zote zinazoendesha biashara hiyo. Iwapo Kampuni zote za *"Tour Operators"* zitasajiliwa kwa kuishirikisha Jumuiya ya *ZATO*, itasaidia kupunguza tatizo la udanganyifu unaofanywa na wageni katika masuala ya kumiliki kwa kampuni hizo. Aidha, Idara ya Uhamiaji ikishirikiana na Kamisheni ya Kazi ziendelee kufanya ukaguzi wa vibali vya kazi na vya kuishi vya wananchi wageni.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya gari za *taxi* zinachukuwa wageni na kuwatembeza sehemu za vivutio vya kitalii. Kwa mujibu wa sheria gari hizo haziruhusiwi kutembeza wageni sehemu za kitalii, isipokuwa shughuli hizo zifanywe na gari za *"Private Hire"* pekee ambazo zimesajiliwa na zinalipia kodi kwa ajili ya kazi hizo. Kuziruhusu gari za *taxi* kuchukuwa na kutembeza wageni katika sehemu za kitalii ni uvunjaji wa sheria za nchi ambapo pia kuikosesha mapato serikali.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine katika sekta hii ni tatizo la baadhi ya tozo mbali mbali za sekta ya utalii kulipwa katika mamlaka mbili tofauti, yaani *ZRB* na Kamisheni ya Utalii. Hali hii inaonesha kutokuwepo kwa mashirikiano baina ya mamlaka mbili hizo. Ili kupunguza usumbufu kwa walipa kodi na kuufanya mfumo wa ulipaji kodi uwe rafiki zaidi, kamati yangu inashauri baadhi ya kodi zijumuishwe na kulipwa sehemu moja, yaani ziwe "*centralized*" ambapo kodi zinazofanana ziwe na sehemu moja tu ya kulipia kodi ambayo itakusanya asilimia ya taasisi husika.

Mhe. Naibu Spika, Bodi ya Wakurugenzi ya Kamisheni ya Utalii ambayo inajumuisha Makamishna mbali mbali ni chombo muhimu sana katika maendeleo ya Sekta ya Utalii. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wa chombo hicho Kamati yangu imepata taarifa kwamba, bodi hii haikutani kwa kawaida, kama ni hivyo maana yake bodi hii haitekelezi majukumu yake kama ambavyo ilitarajiwa. Hali hii inapelekea kuzorota kwa shughuli za Kamisheni hii. Kamati yangu inaishauri serikali kulifuatilia suala hili kwa karibu ili kubaini kasoro zilizopo ili chombo hicho kiweze kutekeleza majukumu yake kama sheria inavyotaka.

Mhe. Naibu Spika, suala la utalii halitokamilika katika hotuba hii bila ya kugusia Makumbusho ya Zanzibar ambayo ni moja kati ya kianzio cha mapato. Watalii wengi wa Zanzibar licha ya kuvutiwa na Mji Mkongwe na fukwe nzuri zilizozunguka kisiwa cha Zanzibar, Makumbusho ya Historia ya Zanzibar ni sababu nyengine inayowafanya watalii wengi kufika kwa wingi Zanzibar, kitu ambacho kiuhalisia kwa sasa hakipo. Hii ni kutokana na kutofanya kazi kwa Makumbusho ya Mnazi Mmoja kwa kipindi kirefu sasa na Makumbusho ya Beit el Ajaib kwa takriban miaka mitatu. Suala hili limeisikitisha sana kamati, kwani nchi za wenzetu ikiwemo Misri imekuwa ikiingiza wageni na mapato mengi kupitia makumbusho yao ambayo ni kianzio kikubwa cha mapato wakati sisi tunafikia hadi kuvifunga halafu tunalalamika eti mapato yetu yanashuka wakati tunashindwa kuwa wabunifu katika kuviendeleza vivutio hivyo vya asili.

Kutokufanya kazi makumbusho hizo, kunaikosesha serikali mapato na kuzorotesha utekelezaji wa bajeti zetu. Pia, tunaitaka serikali inapowapa watu dhamana basi wawekewe na masharti ya kuboresha na kuwekewa malengo ya ufanisi wao na wasipofikia basi wanyang'anywe nafasi hizo, vyenginevyo, tutaendelea kuwapa watu dhamana bila ya kuona mabadiliko yoyote. Hivyo, kamati inashauri kuhakikisha kwamba marekebisho ya Makumbusho hayo na mamlaka inayohusiana na mambo ya makumbusho ifirikirie wazo la kuanzisha makumbusho mapya ili kuongeza wigo wa eneo hilo, kwani Zanzibar ni tajiri wa historia ambayo ikitumika vizuri inaweza kusaidia katika kuimarisha sekta hii ya utalii.

Ufanisi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*)

Mhe. Naibu Spika, haitakuwa busara kugusia nyanja mbali mbali zilizogusiwa katika bajeti hii bila kuwapongeza *ZRB* na *TRA* kwa Zanzibar, kwa jitihada zao za kuendelea kuikusanyia serikali mapato ili kuweza kutekeleza mipango yake ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, niwapongeze *ZRB* kwa umahiri wake wa ukusanywaji wa mapato unaonekana kuridhisha kwa mujibu wa takwimu zinazoonekana katika nyaraka zilizowasilishwa kwenye kamati yangu.

Mhe. Naibu Spika, licha ya mafanikio hayo, Kamati imebaini kuwa bado kuna changamoto katika Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) ambayo inazorotesha ufanisi wake na kuikosesha mapato serikali zaidi. Changamoto hizo ni pamoja na kuwepo kwa mianya mingi ya walipa kodi kufanya udanganyifu hususan wamiliki wa mahoteli na muda mwengine kukataa fedha za walipa kodi zinapokuwa pungufu au zinapolipwa kwa fedha ya Tanzania badala ya Dola.

Mhe. Naibu Spika, ili kuondokana kabisa na tatizo la Bodi ya Mapato – *ZRB* kutofikia malengo, lakini pia kukuza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato wa Bodi hiyo. Kamati yangu inaishauri Bodi ya Mapato iandae utaratibu maalum wa kuwapima watendaji uwezo na uwajibikaji wa wafanyakazi wake kama ambavyo inafanywa na Mashirika binafsi mengi yakiwemo mabenki. Katika taasisi nyingi za serikali kunakosekana mfumo sahihi wa ufuatiliaji na tathmini.

Mhe. Naibu Spika, ni lazima serikali ibadilike kwa kuwawekea mifumo ya ufuatiliaji na tathmini wafanyakazi wake ambapo kila mtumishi awekewe malengo na afanyiwe tathmini na mkuu wake wa kazi, ili kuweza kupima kwa kiasi gani anatekeleza majukumu yake.Uzoefu unaonyesha kuwa mashirika binafsi wanafanya kazi vizuri kwa kuwa mara kwa mara huwapima kiutendaji watendaji wao. Aidha, kutokana na kuwepo kwa uvujaji wa mapato kutokana na mifumo ya ukusanyaji mapato, Kamati yangu inaamini kiwango kinachokadiriwa cha mapato na *ZRB* ni kidogo sana ukilinganisha na hali halisi. Ili kukabiliana na tatizo hili, kamati yangu inaishauri *"Ceiling Committee"* kuwa makini zaidi wakati wa ukadiriaji wa mapato ili kila taasisi iweze kukusanya mapato kutokana na vianzio vyake.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Wenyeviti inaiomba serikali kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuifanyia ukaguzi maalum Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) kuhusiana na ukusanyaji wa mapato, na ripoti hiyo iwasilishwe mbele ya Baraza hili Tukufu kwa lengo la kujiridhisha. Mhe. Naibu Spika, tunashauri hili kwa kuwa tunaamini kuwa tunaamini kiwango cha mapato kinachokusanywa na Bodi hii ni kidogo sana kama itakavyoelekezwa hapo awali.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekelezwa hili, kamati yangu inaishauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kufuata hatua zote zinazopaswa kutekelezwa wakati wa ukaguzi. Kwani asilimia kubwa ya Taasisi

za Serikali huilalamikia ofisi hii kuwa inavikiuka baadhi ya vipengele vinavyopaswa kufuatwa wakati wa ukaguzi. Baadhi ya vipengele hivyo ni kama vile, kutokufanya mkutano wa kuingia *'Entry Meeting'*, mkutano wa kutokea *'Exit Meeting'* pamoja na kutokuwa na mashirikiano ya karibu na watendaji wa taasisi wanayoifanyia ukaguzi. Kitendo hiki huipelekea ofisi hii kuandaa ripoti yenye kasoro nyingi kwa Taasisi za Serikali na endapo Kamati ya *PAC* ikifanya ukaguzi wake basi baadhi ya kasoro hizo hupatiwa jawabu.

Mhe. Naibu Spika, katika kuthibitisha hili, tafadhali rejea Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za SMZ kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Pamoja na Ripoti ya Ukodishwaji wa Ardhi kwa Wawekezaji ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika ukurasa wa 55 na ukurasa wa 102 hadi 106. Katika kurasa hizo yameorodheshwa maeneo ya ardhi ambayo Ofisi ya Mdhibiti ilidai kuwa ilishindwa kupata taarifa hizo, ingawa Kamati ya *PAC* ilivyofanya uchunguzi wake ilifanikiwa kupata taarifa hizo (Tafadhali rejea Ripoti ya Kamati ya *PAC* ya mwaka 2013/2014 ukurasa wa 151 hadi 156).

Vianzio vipya vya mapato

Mhe. Naibu Spika, katika azma ya kuongeza mapato ya serikali ni lazima tukatanua wigo wa mapato kwa kuanzisha vyanzo vipya vya mapato ambavyo bado havijafikiwa, kamati yangu inaamini bado viko vyanzo vingi vya mapato iwapo vitawekewa utaratibu mzuri vinaweza kusaidia kuongeza mapato ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, naomba niainishe baadhi ya vyanzo vya mapato ambavyo kamati yangu inapendekeza vizingatiwe na serikali katika ukusanyaji wa mapato mapya.

i. Kwenye boti za kuwatembezea wageni kwa mfano, Kinazini, Fumba, Kizimkazi, Kiwengwa, Nungwi, Forodhani nakadhalika;
ii. Mashamba ya viungo vya watu binafsi *"Spice Farm"* kwa mfano Kizimbani, Kijichi, Dole, nakadhalika;
iii. Viwanja vya mpira mfano Amani na Gombani *Stadium*;
iv. Kodi ya uchafuzi wa mazingira kwa wazalishaji wadogo kama vile viwanda vya upasuaji mbao;
v. Kodi ya majengo na ardhi;
vi. Kodi kwa wanaotoa huduma ya tiba asili kwa wale waliosajiliwa;

vii. Kodi kwa biashara ndogo ndogo ambapo, serikali inashauriwa kufanya utafiti kwanza kuhusiana na kianzio hiki kwa lengo la kujua idadi halisi ya biashara hizo na baadae zisajiliwe rasmi;

viii. Kuhakikisha kuwa kunatolewa vibali kwa wageni wanaoishi nchini na kuvifanyia mapitio vile vibali ambavyo vimeshatolewa ili wageni hao waweze kuishi kihalali;

ix. Kuimarishwa utaratibu wa ulipwaji kodi kwenye minada katika masoko hususan masoko au madiko ya samaki na minada mbali mbali; na

x. Matumizi ya mashine za kielektroniki *"electronic device"* kila kwenye eneo la ukusanyaji mapato.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Benki Kuu (*BoT*) ndio yenye dhamana ya moja kwa moja ya kusimamia mabenki mengine na kwa kuwa mabenki yana muingiliano mkubwa na wawekezaji kutokana na huduma zao za fedha wanazotoa, na kwa kuwa katika shughuli hizo kuna taratibu na masharti ambayo yamewekwa kisheria. Kamati yangu inashauri serikali kupitia Benki Kuu (*BoT*) isimamie vyema mabenki mengine ili kuhakikisha benki hizo zinazingatia sheria na taratibu wakati wa kutoa huduma kwa wateja wao hususan wageni ili kuepusha udanganyifu na kutoruhusu mianya ya kukwepa kulipia kodi ambayo yanaikosesha serikali mapato.

Mhe. Naibu Spika, katika dhamira ya serikali ya kupunguza msongomano wa magari eneo la Mji Mkongwe, kamati yangu inaishauri serikali iandae utaratibu maalum kwa zile gari zinazoingia eneo hilo kulipia ada, ambazo zitazingatia matabaka maalum. Kamati yangu inapendekeza kwamba, kwa kuwa kuna baadhi ya wananchi wanaingia Mji Mkongwe kwa kazi maalum kama vile wafanyakazi ambao ofisi zao zimo ndani ya Mji Mkongwe na walio na makaazi yao katika Mji Mkongwe, tunawashauri hawa wasilipishwe kodi na badala yake wapatiwe vibali maalum vya kuwaruhusu kuingia na magari yao. Lakini kwa wale ambao wanaingia kwa shughuli zao nyengine ambazo si za kudumu, kuwe na ada maalum ambayo watapaswa kulipia.

Utaratibu huo pia mbali na kupunguza tatizo la msongomano wa magari lakini pia itasaidia kuiongezea serikali mapato. Aidha, kamati yangu inapendekeza serikali itoze kodi magari yenye uzito mkubwa yanayotumia barabara za mjini ili kufidia uharibifu unaosababishwa na uzito wa magari hayo. Katika kulitekeleza hili kwa ufanisi, Kamati yangu inapendekeza Serikali ianze kulifanyia kazi suala hili la uwekaji wa mizani ya kupimia uzito wa magari hayo.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo Kamati yangu inahisi halijasimamiwa ipasavyo katika ukusanyaji wa mapato, ni maeneno ya maegesho ya magari. Kamati yangu inaamini katika eneo hili serikali inaweza ikaongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato, iwapo itaweka mikakati madhubuti ambayo kwa sasa haipo. Kamati yangu inaishauri serikali ifuatilie kwa karibu eneo hilo. Vile vile, katika kukuza ufanisi na kuzuiwa uvujaji wa mapato, kamati yangu inaishauri serikali iangalie uwezekano wa kutangaza zabuni "*tender*" kwa kampuni binafsi zinazoweza kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Serikali. Kwa sasa inaonekana hakuna utaratibu mzuri wa ukusanyaji wa mapato ya *parking* za magari.

Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu tulikuwa tukishuhudia magari yakitokea Tanzania Bara kutembea Zanzibar bila ya kusajiliwa tena, lakini kwa upande wa Magari yanayotokea Zanzibar hayaruhusiwi kutembea Tanzania Bara bila ya kusajiliwa. Kufuatia taarifa ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kupitia hotuba yake ya Mapendekezo ya Bajeti, serikali itaanza utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kwa vyombo vinavyotokea Tanzania Bara kuja Zanzibar kuanzia Julai 1, 2016. Kamati yangu inaipongeza serikali kwa uamuzi wake huo, ambao sio tu utaweka utaratibu katika utekelezaji wa sheria lakini pia itasaidia kuiongezea mapato serikali.

Mhe. Naibu Spika, kitu chengine ambacho Wajumbe wa Kamati hii wamekiona ni kuhusiana na ada ndogo zinazotozwa na Wizara mbali mbali kwa mujibu wa huduma zinazotolewa na wizara husika. Tumegundua kuwa, serikali inapoteza sehemu kubwa ya mapato yake kupitia wizara zake kwa kutoza ada ya chini sana kulingana na thamani ya huduma wanayotolewa wananchi, hata mara nyengine kupelekea taasisi husika kushindwa kujiendesha kutokana na kushindwa kurejesha gharama hata za utoaji wa huduma hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mfano mzuri wa hili ni kupitia Mamlaka ya Maji "*ZAWA*", ambapo kamati yangu imearifiwa kuwa kwa sasa ina deni kubwa la umeme kwa Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) ambalo hushwindwa kulilipa kutokana na fedha chache inayopata kutokana na mauzo ya maji ambayo mara nyingi wananchi hawayalipii kabisa.

Mhe. Naibu Spika, hali kama hii pia inajitokeza kwa Taasisi zetu nyengine kama vile Kamisheni ya Utalii na kadhalika. Kwa mnasaba huo, Kamati hii inaishauri serikali kuyafanyia mapitio ada na tozo mbali mbali zinazotozwa na Taasisi zake na kuhakikisha kuwa zinaendana na uhalisia wa thamani za huduma zinazotolewa *(value for money)*.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kuwa Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO)* linadaiwa na *TANESCO* deni linalokisiwa kuwa ni Tsh. 69 bilioni hadi mwezi wa Machi, 2016, na kwa kuwa Shirika hili hulipa fidia ya Tsh. 350 milioni kwa mwezi kwa huduma ya umeme kwa upande wa Pemba kutokana na idadi ndogo ya watumiaji wa huduma hii. Kamati ya Wenyeviti inaishauri serikali kuwashajihisha wawekezaji kuwekeza kisiwani Pemba ili kutatua tatizo hilo. Vile vile, Kamati hii inalishauri Shirika la Umeme kuendelea kutoa taaluma kuhusiana na huduma wanayoitoa ya kuunga umeme kwa njia ya mkopo. Pia, Kamati inatoa wito kwa wananchi kulipa mikopo yao kwa wakati ili Shirika hili liweze kujiendesha kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, tunalishauri Shirika la Umeme kufanya uhakiki kwa watumiaji wa umeme (wateja) ili kujiridhisha kuwa watu wote wanaofaidika na huduma hiyo wapo kihalali na wanalipa ankara zao bila ya matatizo yoyote. Mhe.Naibu Spika, tunalishauri hili kwa kuwa wapo baadhi ya watu wanafaidika na huduma ya umeme bila ya kulipa malipo yoyote.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine katika matumizi ya Serikali ambayo Kamati yangu imeona ni vyema kuligusia katika hotuba hii ni suala la Ruzuku. Mhe. Naibu Spika, serikali inabeba jukumu kubwa mno la kuzipatia ruzuku taasisi zake kadhaa ambazo kiuhalisia na kwa kuzingatia shughuli zao zinaweza kujiendesha zenyewe.

Mhe. Naibu Spika,, licha ya kuwa na historia inayotofautiana na nchi nyingi duniani juu ya uendeshaji wa shughuli za serikali. Lakini, sasa imefika wakati kwa serikali kujivua na jukumu la kuzipatia ruzuku baadhi ya taasisi zake ili iwe chachu ya taasisi hizo kujiendeleza na kujiimarisha kiutendaji na kimapato. Kwani uzoefu unaonesha kuwa asilimia kubwa ya taasisi zinazopokea ruzuku kutoka serikalini hazitekelezi majukumu yao ipasavyo hususan kwa upande wa ukusanyaji wa mapato na zimebweteka kwa kujua kuwa Ruzuku yao ya kila mwezi ipo na kuendelea kufanya kazi kimazoea.

Mhe. Naibu Spika**,** Kamati yangu inaishauri serikali kuwa, kwa kuwa hivi sasa imeweka nguvu zake katika kupunguza utegemezi wa kibajeti kutoka nje, na mpango wake wa kupunguza matumizi, ni vyema serikali katika bajeti ijayo ikafikiria namna ya kupunguza au kuondosha kabisa ruzuku zinazotolewa kwa mashirika na mamlaka ambazo zinaweza kujiendesha zenyewe.

Mhe. Naibu Spika, katika bajeti hii Serikali imedhamiria kutoongeza ada/ kodi yoyote ile au kuanzisha kodi mpya kwa lengo la kuwapunguzia wananchi ukali wa maisha. Kamati yangu inaunga mkono hatua hiyo kwa kujenga mustakbali

mzuri wa serikali na wananchi kwa ujumla. Hata hivyo, Kamati hii inaiomba serikali kuifanyia marekebisho ada inayolipwa na abiria wanaosafiri kwa njia ya ndege ambayo ni Tsh. 2,000/-. Tunashauri hili kwa kuwa si busara kumtoza abiria anayesafiri kwa njia ya ndege na boti kiwango kimoja cha fedha.

Mawasiliano

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo Kamati yangu inapenda kupatiwa ufafanuzi kwa faida ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa ujumla ni eneo linalohusiana na mabadiliko ya umiliki wa Kampuni ya *Zantel* ambayo imetajwa kuwa kama ni moja ya sababu zilizopelekea kupungua kwa mapato ya serikali.

Kamati yangu inaomba kuelezwa ni sababu zipi hasa zilizopelekea kubadilika kwa umiliki wa Kampuni hiyo, pamoja na kujua kwa sasa serikali inamilika hisa '*shares'* ngapi katika Kampuni hiyo, na kwa wastani serikali imepoteza mapato yenye thamani gani kutokana na mabadiliko hayo.

Mhe. Naibu Spika, wa kuzingatia mazingira ya biashara na utandawazi, tunashauri kuwa, ni vyema Serikali ikatanua wigo wa uwekezaji kwa kuwa na hisa '*shares'* sio tu katika kampuni moja ya simu, bali hata katika Kampuni nyengine za mawasiliano pamoja na Kampuni nyenginezo. Ili kuepukana na athari zinazoweza kujitokeza mara baada ya uwekezaji kuyumba katika sekta fulani, lakini pia kutaifanya Serikali kuongeza vyanzo vyake vya mapato yatokanayo na uwekezaji.

Sekta ya Viwanda

Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia kitabu cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo, imeweka programu ya kuimarisha maendeleo ya sekta ya viwanda kuwa ni miongoni mwa vipaumbele. Uchumi wa nchi nyingi ambazo zimezungukwa na bahari hutegemea sekta za huduma katika kuendeleza ukuaji wa uchumi wake, lakini hali hii haizuii nchi hizi kufanya uwekezaji katika viwanda vya uzalishaji ambavyo vinaendana na mazingira halisi ya nchi hizo, kwani kuna nchi za visiwa licha ya kuwekeza kwenye huduma, pia wameanzisha viwanda ambavyo vinaendana na mazingira yao.

Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwa na viwanda kwani nchi haiwezi kupiga hatua ya maendeleo bila ya kuwa na viwanda. Aidha, sekta ya viwanda ni muhimu sana katika kutatua tatizo la ajira na kuongeza fedha za kigeni kupitia bidhaa mbali mbali zitakazosafirishwa nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na azma hiyo nzuri bado Serikali haijaweka mikakati imara ambayo inaonesha dhamira ya kweli ya utekelezaji wa sera hiyo. Katika utekelezaji wa mkakati huo, Kamati yangu inaishauri Serikali kupitia Kitengo cha *PPP* kufanya tafiti za viwanda mbadala vinavyoweza kuanzishwa Zanzibar ambavyo havitakinzana na mazingira yetu na kwa namna moja au nyengine vitasaidia wazalishaji wadogo wadogo. Mfano wa viwanda hivyo ni kama viwanda vya kusindika samaki, viwanda vya kusarifu mwani na vyengine vinavyolingana na hivyo.

Aidha, Kamati yangu inaishauri Serikali kuchukua hatua za kuwahamasisha wawekezaji kuwekeza katika viwanda hivyo, kwa kuweka mazingira rafiki pamoja na kuvilinda kibiashara.

Mchakato wa Uandaaji wa Bajeti ya Serikali

Mhe. Naibu Spika, Bajeti ni chombo cha wananchi na inatayarishwa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi, hivyo suala la ushirikishwaji wa wananchi halina mjadala.

Mhe. Naibu Spika, ushirikishwaji wa wahusika "*stakeholders*" katika mchakato wa uandaaji wa bajeti kuu ya Serikali kuanzia ngazi ya awali, umekuwa ni kilio cha muda mrefu, hali ambayo imeibua maswali mengi wakati Kamati yangu ilipokaa na wahusika "*stakeholders*" kujadili bajeti hii. Bado bajeti yetu imekuwa ikikosa ushirikishwaji mkubwa wa wahusika mbali mbali katika hatua za awali, na kama kuna ushirikishwaji ni kwa kiasi kidogo sana, na mara nyingi hushirikishwa katika hatua za mwisho ambapo inakuwa vigumu kuweza kuzingatia mapendekezo yao na marekebisho.

Kamati yangu inaishauri serikali iandae utaratibu ambao katika uandaaji wa bajeti kutakuwa na ushirikishaji wa wananchi kupitia vikundi na jumuiya zao mbali mbali kwa kusikiliza maoni yao katika hatua za awali za uandaaji wa Bajeti ili dhana ya kuwa na bajeti ya wananchi iwe na uhalisia.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande mwengine, suala la ucheleweshaji wa vitabu vya Bajeti, kwa Kamati ya Wenyeviti na Kamati nyengine za kisekta kwa kiasi kikubwa kunapunguza ufanisi wa upitiaji wa bajeti ya Serikali, kwani, wajumbe kwa kusaidiana na makatibu wao hukosa muda wa kutosha wa kuhakiki na kuzipitia vizuri bajeti hizo. Hivyo, tunaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kujitahidi kuwasilisha mapema vitabu hivyo ili dhamira ya kuipitia, kuichambua na hatimaye kutoa mapendekezo iwe na tija juu ya Bajeti hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Katika bajeti ya 2016/2017 Serikali imepanga kuja na mkakati wa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima pamoja na kukuza ufanisi katika taratibu za matumizi.

Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuja na mkakati huo kwa kuhakikisha fedha zinazotumika zinaleta tija kama ilivyoainishwa katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2016/2017. Hii ni hatua nzuri sana kwa Serikali katika kuhakikisha fedha nyingi zaidi zinakwenda katika miradi ya maendelo na mambo mengine ya lazima katika uendeshaji wa shughuli za Serikali.

Aidha, Kamati yangu pia inaipongeza Serikali kwa azma yake ya kutopandisha kodi yoyote kwa mwaka wa fedha 2016/2017, badala yake, itajikita katika kuimarisha usimamizi na utendaji wa ndani. Hili ni jambo jema kwa kuwa limedhamiria kuwapunguzia makali ya maisha wananchi, lakini pia, kuongeza mapato ya Serikali, cha msingi Kamati yangu inasisitiza serikali kuwa na mikakati mizuri ya kusimamia utekelezaji huo.

Miundombinu ya usafiri

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya bandari ni moja kati ya sekta muhimu sana katika ukusanyaji wa mapato ya nchi hususan kwa nchi za visiwa. Kwa muda mrefu sasa wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika kutokana na usumbufu ambao wanaupata bandarini kutokana na muda mrefu wanaosubiri kushusha mizigo yao.

Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na mrundikano mkubwa wa meli zinazosubiri zamu za kushusha mizigo ambapo meli zinakaa takriban mwezi mzima, hali hii inawasababishia hasara na kuwakatisha tamaa wafanyabiashara. Kamati yangu inaishauri serikali kuweka mikakati maalum na ya haraka kushughulikia tatizo hilo kabla wafanyabishara hawajakimbia.

Mhe. Naibu Spika, Katika kutatua tatizo hili, Kamati yangu inaishauri Serikali kuharakisha mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri ambao umekuwa katika mipango na vitabu siku nyingi ili bandari hiyo itakapokamilika iweze kusaidiana na bandari iliyopo sasa. Sambamba na hilo, ni vyema Serikali ikaimarisha mazingira ya bandari nyengine ndogo ndogo kama vile bandari ya Mkokotoni ambayo kwa sasa imekuwa ikitegemewa sana katika kusafirishia mizigo, hususan kwa bidhaa zinazotoka na kwenda Tanzania Bara lakini pia kuhakikisha kuwa ushuru na kodi zinalipwa ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kuwa Serikali imetenga eneo maalum katika kijiji cha Chuini kutumiwa na waanikaji wa madagaa wanaotumia eneo la Mpigaduri linalotarajiwa kujengwa Bandari. Kamati hii inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa wananchi hao wanahamia katika eneo hilo jipya mapema iwezekanavyo ili kuepusha mvutano usio wa lazima, hata hivyo tunaomba eneo hilo kwanza liandaliwe mapema.

Mhe. Naibu Spika, Pamoja na fedha zilizotengwa ambazo ni Tsh. 1.7 Bilioni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Wete – Chake Chake.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba Mhe. Waziri aelewe kuwa mradi huo sio mpya, ni muendelezo wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara tatu za Pemba chini ya *BADEA*. Barabara zinazohusika na mradi huo ni Wete – Konde, Wete – Gando na Wete – Chake Chake kwa awamu ya kwanza, ambapo, barabara ya Wete – Gando na Wete – Konde zimeshakamilika. Hata hivyo, Mjenzi anaidai Serikali jumla ya USD 9.4 Milioni na Tsh. 3 Bilioni, ingawa Mhe. Waziri hajatwambia deni hilo litalipwa lini. Kwa kuwa deni hilo limeshakuwa zaidi ya miaka mitatu sasa na kuendelea kutokumlipa mjenzi kwa mujibu wa mkataba deni litakuwa linaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mnasaba huo, tunamuomba Mhe. Waziri alieleze Baraza lako ni lini deni hilo ambalo ni mzigo mwengine kwa serikali litalipwa? Pamoja na deni la barabara ya Amani – Dunga na Mfenesini – Bumbwini.

Pencheni za wazee

Mhe. Naibu Spika, Suala la wazee kuwalipa *universal pension* ni la kupongezwa, hata hivyo, Kamati yangu inaiomba serikali kuhakikisha wazee wote wenye umri wa miaka 70 na kuendelea wanapatiwa haki yao hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Ili kuweka ufanisi katika taratibu za malipo hayo, Kamati yetu inaishauri Serikali iweke "*database*" ya kuwatambua wazee wote, kwa kujua idadi halisi ya wazee wanaolipwa. Kwa kuwa mzee anapofariki malipo yake yanatakiwa kukatishwa, Kamati yangu inaomba kupatiwa ufafanuzi kwa sasa serikali inatumia utaratibu gani wa kuwatambua wazee pindi mzee anapofariki.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Wenyeviti inaiomba serikali kuandaa pia utaratibu wa kuwapatia matibabu bure wazee hawa ili kuzidi kuwaenzi.

Mhe. Naibu Spika, Kwa sasa utaratibu wa kulipa kiinua mgongo wastaafu hauridhishi hata kidogo. Hii inatokana na kuwa inachukua muda mrefu kwa mstaafu kupata kiinua mgongo chake. Ili kujali thamani ya wastaafu pamoja na kuwapa fursa ya kujiendeleza vizuri kimaisha, Kamati yangu inashauri serikali kuandaa utaratibu maalum wa kuwalipa wastaafu ili ndani ya miezi sita awe amelipwa kiinua mgongo.

Mhe. Naibu Spika, katika kutatua hili Kamati yangu inaishauri serikali kuanzisha mfuko maalum '*Sinking Fund'* utakaohudumia shughuli kama hizo.

Kiwango cha utekelezaji wa bajeti

Mhe. Naibu Spika, Kiwango cha utekelezaji wa bajeti ni kipimo juu ya kiasi gani serikali kuwa na bajeti inayotekelezeka na yenye uhalisia. Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016 kwa kipindi cha miezi tisa, Julai 2015 hadi Machi 2016 inaonesha kati ya Tsh 830.4 bilioni ni Tsh 352.8 bilioni tu zilizotumika sawa na asilimia 42.5 tu ya bajeti.

Aidha, matarajio ya makusanyo ya mapato ya ndani na nje hadi ifikapo Juni 2016 yanatarajiwa kufikia 517.4 bilioni sawa na asilimia 62 tu ya bajeti ya mwaka.

Mhe. Naibu Spika, sehemu kubwa ya mapungufu hayo inatokana na kutopatikana kwa fedha za maendelo zikiwemo sehemu ya mchango wa Serikali pamoja na washirika wa maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, swali la kujiuliza ni kwa nini kila mwaka Serikali inaongeza bajeti wakati bajeti ya nyuma hatukuweza kuitekeleza, kutokana na kutokuwa na uhalisia wa upatikanaji wa fedha hizo? Kamati yangu inashauri ni vyema Serikali ikaandaa bajeti yenye uhalisia ambayo inaweza kutekelezeka.

Maslahi ya Watumishi wa Umma

Mhe. Naibu Spika, Katika hotuba ya Mhe. Waziri kwenye kitabu cha Mapendekezo ya Bajeti kwenye ukurasa wa 24 Sekta ya Afya imeelezwa kuwa ni mojawapo ya sekta tano ambazo zinabeba malengo makuu ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, tunalipongeza hili kwa kuwa sekta ya afya ina umuhimu wa pekee katika maisha ya mwanadamu. Vile vile, tunaipongeza sana Serikali kwa jitihada mbali mbali inazozichukua katika kuwapatia wananchi huduma za Afya. Hata hivyo, ili kuongeza ufanisi zaidi katika jitihada hizo, Kamati yangu

inaisisitiza serikali kuharakisha Sera ya Bima ya Afya kwa Watumishi wa Umma, ili watumishi hawa wapate huduma bora zaidi za afya, na kwa wakati na waweze kulitumikia Taifa lao kwa nguvu kubwa. Suala hili hata Baraza la Wawakilishi nalo tunasisitiza kuwa waje waanze mara moja kutekeleza Bima ya Afya kwa wafanyakazi na watumishi wote wa Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaipongeza sana Serikali kwa azma yake ya kutaka kupandisha kima cha chini cha mshahara kuanzia mwezi Aprili katika bajeti ya mwaka huu. Jambo hili ni jema na tunampongeza sana Mhe. Rais kwa kulisema hili.

Aidha, Kamati yangu pia inaipongeza serikali kwa dhamira yake ya kutaka kufanya marekebisho ya Kodi ya Mapato ili kupunguza kiwango cha kodi wanachotozwa wafanyakazi wa kipato cha chini kutoka asilimia 13 kiwango cha sasa hadi kufikia asilimi 9 kama ilivyo kwa wafanyakazi wa upande wa Tanzania Bara. Hatua hii itasaidia kuimarisha maisha ya watumishi wa umma kwa kuwaongezea kipato zaidi katika mfuko wao wa matumizi. Sambamba na hatua hizo nzuri, Kamati yangu pia inaishauri Serikali kuzingatia kuendeleza mfumo wa kuwapandisha daraja *increment* watumishi kila baada ya muda fulani. Kamati inashauri hili kwa kuwa uzoefu unaonesha kuwa kila mishahara inapoongezwa, basi na wafanyabiashara nao huongeza bei za bidhaa maradufu.

Hitimisho

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia ili kuifanya bajeti yetu tunayoipitisha iwe na uhakika katika matumizi halisi basi ni vyema pesa zote zitakazoidhinishwa na Baraza hili zitumike kama zilivyopangwa, yaani kuwe na *discipline* ya matumizi. Lakini pia, serikali ituoneshe ni madeni gani tunayodaiwa na makampuni, mashirika ya ndani na nje, na kuhakikisha yale yote yanayowezekana kulipwa kwenye bajeti hii yalipwe, na yale madeni ambayo yanatusababishia kuyalipia riba kila mwaka yamalizwe ili yasiiongezee serikali mzigo wa madeni yanaweza kulipwa bila ya riba.

Pia, tuwe na mpango maalum kwa muda maalum, ili suala la malipo kwa "*cash*" liondoke na kuwa na mfumo wa malipo kupitia Benki au kutumia mashine za "*electronic card".*

Mhe. Naibu Spika, tukiweza kufikia hatua hiyo basi tunaamini kwa vianzio hivi hivi vya mapato tulivyonavyo tunaweza kuifikisha bajeti yetu kufikia Tsh. Trilioni moja.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wayajadili na hatimae kuyapitisha Mapendekezo ya Bajeti, Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Machano Othman Said ambaye umesoma hotuba ya Kamati ya Wenyeviti. Sasa majadiliano yanaendelea, lakini kabla ya majadiliano Waheshimiwa Wajumbe mnaombwa muwasilishe vitabu vya Makadirio ya Bajeti 2016/2017 kidogo vinataka kufanyiwa marekebisho. Kwa hiyo, mnaombwa haraka wale ambao wanavyo hasa vile vidogo vimetoka karatasi wanaombwa wawasilishe kwa wahudumu.

Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa nataka niwakumbushe kwamba Kanuni yetu ya 58(6), inasema kwamba wale ambao watachangia, muda wa kuchangia ni dakika 30. Mimi nimepewa uwezo wa kuongeza dakika zisizozidi 10. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe ninawaomba sana katika uchangiaji wenu muende moja kwa moja kwenye hoja ili kuhakikisha munaweza kuzitumia hizo dakika zenu. Sidhani kama nitakuwa na uwezo mkubwa wa kuongeza hizo dakika 10. Kwa sababu ninaamini wengi watataka kuchangia. Hivyo, ningewaomba wale wote ambao watapata fursa ya kuchangia basi watumie hizo dakika zao 30.

Waheshimiwa Wajumbe, mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Ali Suleiman Ali, baada ya hapo atafuatia Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali na tutaendelea na Mhe. Simai Mohamed Said.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia bajeti yetu kuu ya serikali. Lakini pia nikushukuru wewe kwa kuniona mtu wa mwanzo baada ya Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kuchangia hotuba yetu hii.

Tatu, ninamshukuru au ninampongeza sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyotuletea hapa na kuchangiwa; zote mbili kwa pamoja; mipango na mwelekeo wa bajeti. Lakini pia nimshukuru Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa mwelekeo wake mzuri na imani yake nzuri kwa wananchi wake wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo niseme tu kwamba bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Wenyeviti. Lakini kwa kuwa nafasi hii ya kusoma

taarifa ya Wenyeviti anapewa mmoja Mhe. Mwenyekiti au mwengine yeyote. Na sisi tuna wajibu wa kuongeza ubora zaidi bajeti hii kwa maslahi ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuwa na mambo machache sana lakini yana umuhimu kwa mujibu wa maendeleo ya nchi yetu. Nchi yoyote duniani, inategemea mapato yake ya makusanyo. Mapato hayo...

(Hapa umeme ulizimika kwa muda mfupi)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuwe na subra kidogo. Tuendelee.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Ninaamini Mhe. Naibu Spika, mapato ni uti wa mgongo wa serikali. Bila ya mapato hatuwezi kusimama hapa kuzungumzia lolote; mambo ya bajeti na maendeleo ya nchi yetu. Nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wake, kubwa la kuliangalia mbele ni kukusanya mapato yetu bila ya utani au bila ya kumuonea aibu mtu.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu vianzio vya mapato vipo vingi sana. Mimi mara nyingi ninapojadili lolote au ninapotoa taarifa yangu hufanya utafiti. Hata ninapouliza swali nishalifanyia utafiti. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, tuingie katika mambo ya risiti. Wananchi wetu hawana uzoefu wa kupokea risiti au kudai risiti. Risiti ni pato la nchi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nilibahatika katika Baraza ninakumbuka kwenye 2010, nilipata ziara moja nikaenda Rwanda kwenye mambo ya wajasiri amali wa jua kali. Kama unakwenda kununua sindano ya kushonea, lazima upewe risiti, ununue kibiriti lazima upewe risiti. Lakini ninathibitisha kwamba hapa tulipo, tufanye mambo mbali mbali ya kufanya kama utafiti wa mambo mbali mbali, ukienda duka lololote unaweza kwenda kununua vitu vya milioni moja risiti hupewi, labda uidai. Kwa hivyo, pana mambo mawili. Muuza duka anakuangalia ulivyo. Niiombe wizara kutokana na watendaji wetu pawe na uzoefu maalum wa kudai risiti kwa wananchi, kwa sababu risiti ni chanzo kimojawapo cha kukusanya mapato.

Mhe. Naibu Spika, la pili kubwa, kukusanya ni sehemu ya kwanza lakini matumizi ni sehemu ya pili. Niiombe sana wizara, matumizi yadhibitiwe kwa uangalifu sana. Kama Mhe. Rais alivyotwambia katika uzinduzi wake wa Baraza, alisema tu kwamba atahakikisha udhibiti unapatikana ili kutumia

matumizi yetu tunayoyapata kwa kadri ya mambo tunayojipangia. Kwa hivyo kudhibiti matumizi ni sehemu mojawapo ya kujihakikishia kwamba tunakwenda vyema kwenye maendeleo yetu ya bajeti yetu tunayoipanga hapa.

Mhe. Naibu Spika, nilisema kwamba mimi bahati nzuri ni Mjumbe wa Kamati ya Wenyeviti. Lakini pamoja na hayo, na wananchi wananitegemea wanisikie katika jimbo langu au wananchi wa nchi yetu nzima hii ya Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, maendeleo yanatokana na mambo matatu; Fedha, Changamoto zilizokuwemo katika maeneo yetu (fedha ndiyo italeta maendeleo hayo ninayotaka kuyataja), na tatizo la maji, barabara na vituo vya afya. Ni sehemu kubwa ya jamii yetu kujisikia kwamba inapata huduma bora katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Naiomba Wizara yetu ya Fedha na Mipango ifanye bidii kwa baadhi ya maeneo ambayo kero hiyo imekuwa ya muda mrefu sana. Mimi Jimbo langu jipya la Kijitoupele, wananchi wanaishi katika mazingira ambayo si mabaya kusema mabaya, lakini mabaya. Kwa sababu kuna maeneo maji ya kunywa bado hawayapati ya kuridhisha, hakuna.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano ukitaka kugombea popote lazima ufanye utafiti kwanza, wananchi wana kero gani. Jimbo langu jipya lakini nina mazingira matatu muhimu. Kwanza ni maji. Kuna eneo linaitwa Kwarara Madina. Jina la Madina ni kubwa. Maana ukienda Makka, Madina ndipo unapoanzia lakini jina zuri lakini huko kwahala kugumu sana maisha yao. Maji hawayajui yalivyo. Nilisema siku moja wakati Mhe. Rais alipokuja kuzindua Baraza, nilisema kuwa watu wa huko wanakunywa togwa, maji hayana thamani. Hata ukiyachemsha pia ni kero. Na ndiyo maana kipindupindu kilianzia huko kikateremka huku chini. Mwenyezi Mungu atunusuru!

Mhe. Naibu Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri suala hili kwa upendeleo tuliangalie kwa hali na mali. Lakini visima ni sehemu ya kwanza. Pili ni sehemu ya umeme. Umeme hadi kufika leo Tumbatu kwa rafiki yangu Mhe. Haji Omar Kheri unang'ara. Ukienda visima mbali mbali vya Unguja na Pemba vinang'ara umeme. Ni suala la kuipongeza serikali yetu kwa dhati kabisa na mimi ninaipongeza. (*Makofi*)

Na mimi ninaipongeza lakini kwa bahati mbaya huku Madina (yaani Kwarara Madina) mpaka leo hakuna umeme, yaani umeme wa aina yoyote hakuna. Naiomba serikali kwa huruma ili wananchi wapate maji, basi ni lazima kwanza wapate umeme. Ninaamini kama tutapata nguzo kumi na sita mpaka ishirini, ninaamini kama nimejitolea Mwakilishi wao kwa wananchi wangu pamoja na Mbunge wangu Mhe. Shamshi Vuai Nahodha, tutasaidiana kwa hali na mali

wananchi wale wapate umeme haraka ili visima vipatikane kusaidia maendeleo ya wananchi wetu wale wajisikie kama nao wanaishi kwenye jamii inayokubali maendeleo ya leo.

Mhe. Naibu Spika, huku kwahala pia kulikuwa na matatizo makubwa ya barabara mpaka leo. Maana ukitoka Meli Tano hakwendeki. Lakini bahati nzuri ninamshukuru Mhe. Naibu Waziri pamoja na Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, kwa kazi nzuri ambayo wanapita kuona maeneo mbali mbali na kuyafanyia kazi. (*Makofi*)

Mimi nilipeleka maombi maalum Mheshimiwa nisaidie wananchi wangu hawa angalau wapate usafiri wa daladala. Daladala Mhe. Naibu Spika, huko hakuna daladala, hakuna chochote. Bahati nzuri tumekwenda kidogo tumepata msaada wa Wizara na juhudi za Mbunge na Mwakilishi tukaongeza tumeziba yale mashimo mengi katika barabara hiyo. Sasa hivi barabara zinapitika afadhali. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pia ninasema kwamba ninatoa taarifa kwa niaba ya mwenzangu Mhe. Mbunge ambaye yupo Bungeni, huko Madina nilikozungumza mwanzo. Huko walikuwa wanatumia labda gari ya ng'ombe. Ile gari ya *carry* haiendi, *PRADO* haliendi; gari ya aina yoyote haiendi. Lakini juzi kwa ujasiri kabisa tumejitolea na Mhe. Mbunge, tumeipiga *grader* barabara hiyo. Leo gari ya aina yoyote inakwenda mbio bila ya matatizo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri na Naibu Waziri wa Usafirishaji yupo hapa, nitaiomba serikali daladala za *route* ya Kwarara lazima zifike Madina. Kwa sababu wananchi wako wanaishi katika mazingira magumu. Wanafunzi wanatoka huko wanakuja zao Meli Tano - Kijitoupele wadogo kwa mguu bila ya msaada wowote. Lakini zikiwekwa daladala wanajua watapata msaada.

Bahati nzuri barabara hiyo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anaijua, ameshakwenda kutuwekea jiwe la msingi katika Skuli mpya ya Sekondari ya Tumaini iliyokuwepo huko Kwarara huko ninakozungumza. Mhe. Naibu Spika, barabara ninafikiri kipindi alichokuja na sasa hivi ukienda utakuta tofauti kwa asilimia kama 80 hivi inapitika vizuri. (*Makofi*)

Mhe.Naibu Spika, jengine nizungumzie tatizo tulilokuwa nalo la visima mbali mbali kwenye sehemu zetu hizi. Mimi katika Jimbo langu la Kijitoupele kuna kisima kipo Mwanakwerekwe "C", kilichimbwa zamani sana ambapo tupo mpaka mmoja na Jimbo la Mwanakwerekwe na Jimbo la Kijitoupele

NyumbaMbili. Kisima hichi kilifanyiwa matengenezo vizuri na kina maji ya kutosha. Ili serikali ipunguze gharama za kupigiwa hesabu za hali ya juu kuna matatizo hivi hivi watu wakafanya yao. Kama patapatiwa mashine kubwa ya kutosha na mabomba ya kutosha kwa maeneo ya Mwanakwerekwe "C" Nyumba Mbili mpaka viwanja vya Mafunzo pale Tomondo watakuwa hawana shida ya maji kwa muda mrefu kama itawezekana kutekelezeka hivyo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naiomba serikali hili halina gharama kubwa kuliko kuja kutafuta mengine yakazalisha mambo ambayo hatuyategemei. Ninamuomba Mhe. Waziri, Naibu Waziri twende tukatembee na wauone ukweli huo. Fedha zilitoka kwa bahati mbaya lakini ninasikia zimetumika kwa bahati mbaya hatukuelewa. Mpaka leo maji yanapatikana lakini kisima kipo na maji ya kutosha, lakini pengine Mhe. Naibu Waziri, ijapokuwa alinijibu juzi kwamba kuna kisima Taveta Magirizi, ni kisima kizuri kimechimbwa kikubwa na maji yake yametuthibitishia Meli Nne, Taveta, Kijitoupele mpaka Tomondo Uzi. Kikitengenezwa kisima hicho kama kitapata mabomba na umeme tu sasa hivi, watu watakunywa maji bila ya matatizo, ni mashine, mabomba pamoja na umeme. Mambo hayo mimi ninaomba kuna mifuko ya Mbunge na Mwakilishi tupo tayari kutumia huduma hizo kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu kuipunguzia hasara au matumizi makubwa serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuna kisima ambacho kinatumika kwa muda mrefu Tomondo Uzi Uwanja wa Mpira. Mimi nimeshakuwa mwenyeji Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri, lakini tutakutaka wewe Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Waziri acha afanye kazi za utawala. Twende ukakione kisima hicho kipo, kilikuwa kinazalisha maji mpaka Kijitoupele, lakini walikuja watu wakatumia ujanja wao, maji yale wameya-*block* hayaendi tena kule Kijitoupele, yapo hapa hapa tu Tomondo na hapa Tomondo siyo sehemu zote.

Nimuombe sana Mhe. Waziri hili tulifuatilie tulifanyie kazi. Bahati nzuri Waheshimiwa Mawaziri hii ni bajeti kuu ya serikali, kila mtu imemgusa katika wizara zote. Kila mtu mwenye lake aliwahi hapa. Kama kaja kukosa kwenye wizara, hapa ameshapata na ninaamini hatukosi. Kwa sababu muda wa kutosha umewekwa kwa mpangilio wa kueleza shida za wananchi wetu kwa serikali yetu.

Hivyo nimuombe Mhe. Waziri huyu mfanyakazi anayesemekana hafai. Kwanza si muajiriwa. Kwa hivyo anafanya kazi yake anavyotaka. Anawahatarisha wananchi hao kukosa maji kwa jambo la uzembe kabisa. Namuomba sana Mhe. Waziri hili ataliona wakati wote, tulifuatilie ili kuhakikisha kwamba tunafanya kazi zetu kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo ambayo yalijitokeza bahati nzuri kwenye Jimbo la Mwanakwerekwe lilijenga hospitali nzuri na *dispensary* kubwa. Tulitegemea wazazi, watoto wetu, akinababa watapata huduma hapo hapo. Kwa bahati nzuri imeshaezekwa na kufanywa kila kitu, bado umaliziaji. Naiomba serikali kwa kuwa wananchi wataitegemea Kwarara, wanaokwenda Fuoni waache kwenda huko waje hapa Taveta, Meli Nne Uzi, Tomondo Uzi na majirani wa Pangawe watakuja hapa kuhudumiwa na hospitali.

Niiombe serikali hili suala lipo na lipo vizuri, lakini na sisi tumesema tukienda kwa kuchangia mimi na Mbunge, tumesema tujitolee hapa mifuko mia moja hivi sasa kwa ajili ya uanzishaji ili serikali ipate nguvu ya kuifanyia kazi na wananchi wetu wafaidike. Hiyo tutaitekeleza kwa haraka kwenye kipindi hichi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nimezungumza tatizo la umeme, sina haja ya kulirudia tena, kituo cha afya sina haja kukirejea tena.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho na nimesema mchango wangu tumeuingiza katika Kamati ya Wenyeviti. Niiombe serikali hivi sasa kuna matatizo mengi kwenye jamii zetu au katika jamii tunavyoishi kwenye maeneo yetu. Kama inavyosema taarifa siku hadi siku Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tulimuona juzi na jana yupo katika ziara mbali mbali ya kutembelea katika maeneo ambayo yaliyopatwa na maafa fulani.

Mimi niseme tu Mhe. Naibu Spika, kuna mgomo wa makusudi sasa hivi umeandaliwa na wafanyakazi wengi ndiyo wameandaa mgomo huo kwa ajili ya serikali kuikomoa. Lakini nilisema siku moja watajikomoa wao, kwa sababu serikali ina maamuzi yake. Kama mtu ana *complain* yoyote ya kulipa ushuru au kuna mfanyabiashara yeyote anachochea wenziwe wasilipe ushuru, mimi ninaiomba serikali ichukue hatua ya mara moja kumdhibiti mtu yule na kuhakikisha inamuweka pahala pasipojulikana kwa muda usiojulikana. Vyenginevyo Mhe. Naibu Spika, nchi hatwendi. Na nchi tukiwa na huruma sana hatwendi. Lazima tuangalie faida na hasara kwenye jamii yetu. Faida kubwa ya serikali ni ushuru. Lakini kuna watu wanafanya *sabotage* ya makusudi hawataki ushuru. Ni vyema tuliangalie hili kwa manufaa ya nchi yetu. (*Makofi*)

Jengine la mwisho Mhe. Naibu Spika, kuhusu uchochezi. Uchochezi bado upo na tuseme tu kwamba wakimuona Ali Suleiman Ali (Shihata) hawasemi wale watu. Kwa sababu wanajua Ali Suleiman labda atafikisha pahala panapohusika, na mimi sirudi nyuma, lakini niseme tu kwamba yeyote anayeleta chokochoko

katika nchi Mhe. Naibu Spika, akahifadhiwe kwa muda usiojulikana. Vyenginevyo, ninarudia tena hatwendi. (*Makofi*)

Sasa hivi tumefikia wakati Mhe. Naibu Spika, kuna maiti watu hawataki kuwazika huko. Shihata CCM tusiende mazikoni au mtoto wa Shihata tusiende kwenye shughuli yake. Lakini niseme tu Mhe. Naibu Spika, tuwe wakali na tuhakikishe kwamba serikali hii ipo mikononi kwa asilimia yote. Tumepewa na Mwenyezi Mungu tuwatumikie wananchi wetu bila ya ubaguzi. (*Makofi*)

Kwa hivyo, ninamshukuru Mhe. Rais wetu, ninamshukuru Makamu wa Pili wa Rais, ninawashukuru Mawaziri, Manaibu Mawaziri na watendaji wetu, wamo katika mwelekeo huo wa uadilifu. Mimi ninasisitiza uadilifu kwanza mengine baadae. Kila mwenye haja yake tumtimizie kwa manufaa ya maisha ya kila siku. Tusimdhulumu mtu bila ya kutaka kudhulumiwa. Akitaka kudhulumiwa na sisi tumdhulumu.(*Makofi*)

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba hoja hii ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Mimi na wananchi wa Jimbo la Kijitoupele na ninaitakia kheri bajeti hii ipite bila ya matatizo. Ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ninakushukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali. Baada ya hapo tutampa nafasi Mhe. Simai Mohamed Said na baadae kama muda utatosha atachangia Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Naibu Spika, wa Baraza la Wawakilishi. Kwanza nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutupa pumzi hizi tulizokuwanazo, maana yake yeye ndiye mwenye kuhifadhi pumzi zetu, ni nguvu zake Mwenyezi Mungu.

Vile vile, nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Uzini kwa kupitia Chama cha Mapinduzi ndicho nilichokalia kiti hiki cha leo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuipongeza kwa dhati bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyowasilishwa na kaka yangu Waziri wa Fedha, Dkt. Khalid Salum pamoja na watendaji wake. Nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Fedha nzima na taasisi zake zote za *ZRB, TRA*, makusanyo yote na sehemu zote kwa kazi nzuri na uzalendo na usikivu mkubwa kwa kuweza kusimamia bajeti hii na kutupa maelekezo, na sisi kama wawakilishi kazi yetu ni kuipitisha.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitoe tu mawazo, tukienda kwenye ukurasa wa 29 kifungu cha 68(a), uwekaji wa kamera, vifaa vya ulinzi shilingi bilioni 18.

Hizi sambamba na pendekezo hili inapendekezwa zaidi kuwa kwa mwaka ujao wa fedha jumla ya shilingi bilioni 26.6 kutoka kwenye mfuko wa miundombinu, zitumike kugharimia miradi ya miundombinu ifuatayo.

Mhe. Naibu Spika, sisi sote hapa tumetokana na wakulima na wakwezi. Tulifanya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar kuwaletea wananchi neema ya maendeleo ya maji na huduma nyengine zote, na tumeingia humu kwa nguvu za wananchi na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, tunaposema uwekaji wa kamera na ulinzi shilingi bilioni 18, *is alot of money*. Mhe. Naibu Spika, hizi pesa kwa ushauri zingepelekwa kwenye barabara zetu za ndani, kwa sababu Mhe. Naibu Spika, leo barabara zetu za ndani hali yake ni mbaya na kufika sisi Baraza la Wawakilishi na kuunda serikali yetu inayoongozwa na Mzee wetu Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni wakulima na wakwezi ndio walio wengi.

Mhe. Naibu Spika, sasa barabara zetu ukianzia Uzini, hata ile gari ya ng'ombe yule ng'ombe ng'oo, ng'oo anaumia kutokana na barabara za ndani hazipitiki. Sasa nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha na serikali tuwe wasikivu, lakini barabara za ndani ni mbaya sana na zinaumiza. Wazee wetu; mama zetu wanapoteza roho hii leo kwa sababu ya barabara za ndani. Sasa pesa hizi mimi naamini zingepelekwa kwenye barabara za ndani *wallahi* kwa mwezi huu 15 wa Shaaban uliomalizia jana, hapa tutakuwa hatuna matatizo hata miaka 100 ijayo katika ushindani wa kisiasa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nijue tumeshafanya zoezi hili la uwekaji kamera, tija gani iliyopatikana kwetu sisi na gharama ngapi zimetumika. Mhe. Naibu Spika, naiomba sana serikali pesa hizi, ushauri wangu, wananchi wa Uzini na majimbo mengine, leo ukienda njia ya Miwani, Manzese, Bambi Kijibwa Mtu, Mchangani, Pagali, sehemu zote Mhe. Naibu Spika, ukienda yule ng'ombe analia, seuze binadamu. Kwa hivyo, lazima tufike hapa tuwe na huruma na wakulima na wakwezi, serikali hii ndio tegemeo letu, lakini leo tunapanda magari mazuri halafu mwananchi wetu wa ndani unaposema unataka kumuondoshea umaskini kwa MKUZA, bado ataendelea kuwa maskini.

Kwa hivyo, ningeomba hii miundombinu shilingi bilioni 18 hizi zingetumika na zingemaliza barabara za ndani. Mimi Mhe. Naibu Spika, naahidi niko tayari

kushirikiana na serikali yangu inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein, kama kutakuwa na mapungufu nitakwenda mimi nje kujaliza hayo mapungufu yenyewe na uwezo huo ninao, uwezo huo ndio wananchi wamenifikisha hapa nilipofika. Lakini naomba sana wizara shilingi bilioni 18 miundombinu wakati kuna barabara ukienda, watu wengine wanashindwa kwenda kutoa ahsante kwa sababu hali ni ngumu, huko kuna mambo mengi lakini barabara za ndani hazifai na Mwenyezi Mungu katuletea mtihani wa mvua ya masika ndio imezidi.

Kwa hivyo, naomba sana, mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Uzini, na kwa niaba ya nchi hii sote, naomba kuona serikali iwe wasikivu katika hili, barabara za ndani hazipitiki na huko ndio kwenye kilimo, ukitaka kumuondoshea mkulima umaskini tena wala hahitaji lami ni kifusi tu.

Mimi Jimbo langu la Uzini hata barabara moja ya ndani haina lami, lakini sitaki kuwa *selfish*, nataka twende kwa maendeleo ya pamoja. Kwa hivyo, serikali ituambie hiyo awamu ya kwanza iliyoanza ilileta tija gani ya kuhusu suala hili la kamera, halafu ni gharama gani imetumika.

Mhe. Naibu Spika, 'mkaa na maiti haachi kulialia', lakini kwa kweli jambo hili litasononesha sana, tunataka kwenda kwa wananchi sisi watendaji ndio wenyewe wahusika barabara za ndani hakuna moja iliyokuwa safi. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kuomba tu serikali kwa kupitia Waziri wa Fedha naamini na yeye katoka huko huko tulikotoka. Huko kwa wakulima na wakwezi ndio sisi tulipotokea, ndio tukaja hapa, sasa hilo niliomba nitoe rai na nitoe ushauri kwamba hizi shilingi bilioni 18 ni pesa nyingi na zitamaliza matatizo mengi, nyengine zinaweza kubakia na zikafanya vitu vyengine.

Mhe. Naibu Spika, nikiwacha hili nije kwenye suala la gawio la *BoT*. Mhe. Naibu Spika, asilimia 4.5 ilikuwa ya muda. Sasa mimi nilitaka niombe tu serikali kwa kupitia Waziri wa Fedha maandishi yapo. Mimi nakumbuka wakati wa Dkt. Salmin Amour Juma Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Komandoo. Mwaka 1996 kuna ripoti ya *IMF* na tukakubaliana kwamba hii asilimia 4.5 iwe ya muda na maandishi yapo.

Mhe. Naibu Spika, 'mkaa na maiti haachi kulialia', kwa hivyo nilikuwa naomba wizara inayohusika, na mimi nashukuru sana kwamba Wizara ya Fedha ina Katibu Mkuu wa fedha Khamis Mussa.

Mhe. Naibu Spika, huyu Katibu Mkuu ana rasilimali kubwa, kwa sababu toka wakati wa Dkt. Salmin Amour Juma alianza kuwa mtendaji katika nchi hii,

alitokea *TRA, ZIPA,* na Wizara ya Fedha. Sasa kwa kweli anatutosheleza kutuambia na anafahamu Hazina ya Zanzibar.

Kwa hivyo, mimi ningeomba serikali tusikae tukazifungia kwenye makabati yetu makabrasha, vitu hivi vipo na tulikuwa na majadiliano, sasa tukisema tu asilimia 4.5 wakati 1996, hata *IMF* tulikubaliana kwamba hii ilikuwa ya muda. Kwa hivyo, naomba serikali sikivu Mhe. Waziri wa Fedha tukalitizama hili na kuweza kulizungumza jambo kama hili. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, niombe na kama kuna vitu vyengine hawana mimi ninavyo kichwani kwangu vitu vingi sana katika masuala haya, kwa sababu nilishiriki kikamilifu *Alhamdulillah,* na vile vile anaweza kutusaidia Mhe. Waziri Amina Salum hapa ambaye tunaye humu ndani, ambaye ndiye ninayemuona humu ndani ambaye alishiriki mambo mengi sana wakati wa Dkt. Salmin Amour Juma, ambapo na yeye ana hazina kubwa sana ya kuweza kutusaidia humu ndani, lakini tukiacha hapo Mhe. Naibu Spika, twende kwenye *VAT*.

Mhe. Naibu Spika, suala la *VAT* ambalo tumeambiwa kwenye *paragraph ya* 7, 8 pamoja na 9, lakini kwenye hiki kifungu cha 7, athari iliyojieleza awali kutorudishiwa fedha za *VAT* za vifaa vitokavyo Tanzania Bara ambavyo vimechelewa.

Mhe. Naibu Spika, nikwambie na niliambie hili Baraza, wakati wa Dkt. Salmin Amour Juma hili jambo lilijitokeza kuhusu suala la *VAT, sale tax* na kwa kweli serikali ya Dkt. Salmin Amour Juma Komandoo, Mwenyezi Mungu ampe afya, kwamba tulichelewa sisi kwa sababu ya kadhia hiyo hiyo tuliyokuwa tumeiona na Zanzibar hatukuwa tayari, lakini kwa watendaji tulijaribu kukaa kitako tulikuwa wagumu sana wakati wa Dkt. Salmin Amour Juma suala hili la *VAT*, wakati ule lilikuwa linaitwa *sale tax* lilikuwa sio rahisi katika suala hili la *VAT*, lakini tulipofika sasa wakati wa Dkt. Salmin Amour ikabidi sasa tutumie hekima twendeni kule, lakini ilikuwa ni ngumu sana. Sasa leo yanajirejea haya, wenzetu wamefuta suala la *VAT* bila ya kujua misingi yake, bila kujua *issue* zake, bila kujua *terms of references* zilizokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nampongeza sana Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein na Dkt. Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni Marais wasikivu sana, ningewaomba watendaji waandae programu maalum ya kuwapa viongozi hawa, kwa sababu tunaeleza vitu ambavyo vipo na vinafahamika. Rais Magufuli ni msikivu sana katika serikali yake, kwa hivyo ni vizuri viongozi tukakaa tukaweza kuwapa vitu vyenye msingi.

Kwa hivyo, matumaini yangu Mhe. Naibu Spika, hili suala la *VAT* litizamwe na linaweza kuleta athari, kwa sababu unaposema unafuta, naamini pesa zetu zitarejea, ukiendelea ina maana unaviambia viwanda vya Dar-es-Salaam ikifika Zanzibar hapa itozwe tena *VAT* wakati tuna ushirikiano mkubwa, tuna Muungano wetu imara.

Kwa hivyo, mimi ningeomba kwa wenzetu, hivi vitu vipo na vielelezo vipo. Mimi leo nataka niseme wazi, awamu ya Dkt. Salmin Amour iliyosimamia vitu vyote vya uimarishaji wa Muungano wetu, inatutosheleza kuvichukua vitu vile tukaviunganisha tukapata Muungano uliokuwa imara wa serikali mbili, hicho kitu hakiepukiki, tutajenga uimara wa udugu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba vitu hivi vipo kwenye makabati, yangefunguliwa yakatolewa vumbi yakajadiliwa, viko wazi, na wenzetu walifanya kwa nia nzuri.

Mhe. Naibu Spika, ninachoomba katika hali hii yatazamwe masuala haya yaliyokuwepo tukaeni kitako ili tuone kwamba tunafanya vizuri katika kuisaidia Zanzibar na kushirikiana na wenzetu wa Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Tume ya Pamoja ya Fedha. Tume hii ingekuwa imekaa basi mambo mengi tungeepukana nayo. Tume ya Pamoja ya Fedha imo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukurasa wa 134. Lakini kwa bahati nzuri au mbaya na mimi nina uhakika hii Tume ya Pamoja iliyoundwa, tena kwa bahati nzuri Mwenyekiti wetu anatoka Zanzibar Mwinyimbegu ni Mwenyekiti wa Tume ya Pamoja.

Sasa Mhe. Naibu Spika, *they are not the losers, we are the losers.* Tume hii ya pamoja ya fedha mwaka mzima haijapata kukaa, ambapo mambo mengi yangeweza kuondoshwa humu, imo ndani ya Katiba halafu unakaa mwaka mzima tena Mzanzibari ndio Mwenyekiti. Mimi nataka aje anithibitishie Mhe. Waziri wa Fedha, ni lini ilikaa Tume ya Pamoja ya Fedha, haya yote yasingejitokeza, haya mambo ya *VAT*, mambo ya asilimia 4.5 na mambo yote ya jumla. Lakini ukienda wenzetu wanaweza kusema kwamba hatuna fedha, hivi sisi Wazanzibari, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatuna fedha ya kuchangia ile Tume ikapata posho. Mimi niko tayari kutoa posho ya shilingi milioni 10 ili Tume ikae, haizidi shilingi milioni 10.

Kwa hivyo, nimuombe Mwinyimbegu na wenzake tuwe na uzalendo, tumeunda Tume ya Pamoja kwa mwaka mzima haijakutana, sasa kuna vitu hivi Mheshimiwa tusilaumu tu wakati sisi wenyewe *we are not aggressive* katika

kufuatilia haya mambo, *commitment*. Kwa hivyo, ningeomba Tume hii ya Fedha ya Pamoja, hata hapo nyuma; mimi nampongeza sana Makamu Mwenyekiti wa Tume, Juma Kasonga.

Mhe. Naibu Spika, huyu Mzee Juma Kasonga kwa kweli ni mtu mwenye huruma sana kwa pande zote mbili, lakini leo tumekaa tumeunda Tume imo ndani ya Katiba ukurasa wa 134, kuna Tume hii imetoa ripoti zake kwa Marais waliopita mpaka leo imekaliwa.

Mimi nafikiri vizuri zile tume zilivyokaa, yale makabrasha yatolewe yaletwe kwenye Baraza na Bunge, lakini tunafika leo mwaka mzima, tutakwenda na mwaka mzima mwengine Tume ya Fedha ya Pamoja ndio inayoondosha matatizo au umuhimu wa kuunganisha serikali zetu na Muungano wetu.

Kwa hivyo, ningemuomba Mwenyekiti Mwinyimbegu, mimi nitampa pesa hizo shilingi milioni 10, maana tumezoea kuchukua shilingi milioni 1, laki 5, tutoe, lakini tunaumia, kuna mambo muhimu. Tunasimama hapa sote sisi Wawakilishi tunazungumzia maji, barabara, umeme na tunazungumza kero za wananchi, tumefika ndani kuwatumikia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni boi wa Uzini, ni mfanyakazi wa Uzini kupitia Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, lazima tuone jambo hili linatekelezwa, serikali yetu imeshafanya mambo mengine ambayo inaongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein, imeshaunda miundombinu ya barabara, umeme na mambo mengi. Lakini kuna mambo mengine ni lazima tusaidiane katika kukamilisha vitu kama hivi.

Mhe. Naibu Spika, ni kawaida kwa sote tunapaswa tuwe wamoja, kwa sote tunapaswa tuwe na umoja na mshikamano.

Mhe. Naibu Spika, hayo yanayosemwa nje Zanzibar kuwekewa vikwazo, hizo ni 'kelele za mlango hazimkeri mwenye nyumba', nasema tuko tayari kula muhogo na sembe, lakini Zanzibar tutaamua sisi wenyewe maamuzi yetu, hiyo ndio sera yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, sio jambo geni hili, wakati wa Dkt. Salmin Amour mpaka sisimizi waliwekewa vikwazo, yule sisimizi aliwekewa vikwazo, nchi imekwenda *Alhamdulillah*. Kwa hivyo, ninachotaka kikubwa ni mashirikiano.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachosema kwamba katika mazingira kama haya na kama sisi wawakilishi tukaeni pamoja ili tuone faida ya nchi yetu, faida ya kujenga msimamo wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nawapongeza wenzangu kwa kujitoa. Wenzetu wamejitoa, *'kuvuja kwa pakacha nafuu ya mchukuzi'*, lakini ni lazima tuwe na *commitment* humu ndani kwenda kuitekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, wananchi walio wengi wana maamuzi yetu sisi humu, ndio maana Rais akapata asilimia kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, katika kumalizia naiomba serikali na nawaomba viongozi na watendaji tuwe wakweli kwenda kuwatumikia wananchi. Baraza letu hili umeliona Mhe. Naibu Spika, halina Muhindi, Muarabu wala Mnyamwezi. Baraza letu la Zanzibar *is the Cosmopolitan*, na ndio chama chetu tulichokuwa nacho hapa tunachoringia. Mimi nimetoka Uzini Raza, ni jambo la demokrasia ndani ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nimeambiwa sio ukurasa wa 134 basi naomba nisawazishe tu, lakini imo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha hiyo imo, lakini naomba niiondoshe hii ya ukurasa wa 134 nimeambiwa labda nimekosea namba, lakini imo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Pamoja kati ya Zanzibar na ndugu zetu wa Bara.

Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, mimi nimetoka kwenye *grassroots*, na nitafanya kila hali na mali ili kuhakikisha nashirikiana na serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein, inayoongozwa na Makamu wa Pili jemedari, huyu naweza kumwita Komandoo sasa Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya pamoja na watendaji wake. *(Makofi)*

Kwa kweli nitajitahidi kwa uwezo wetu wote kuhakikisha kila jambo tunasaidiana katika kulitekeleza. Mhe. Naibu Spika, Mungu amenijaalia mimi natoka kwenye familia ya kimasikini sana, wazee wangu mimi wakichunga punda lakini Mwenyezi Mungu amenijaalia kufika hapa nilipofika. Nataka kushirikiana na serikali yangu kwa upande wa taasisi zote za Serikali zinazofanya kazi kuanzia walimu, kilimo, maji, umeme, mawasiliano wanaofanya kazi jimbo la Uzini niko tayari kuwapa mamilioni ya mkopo usiokuwa na riba, usiokuwa na tija, usiokuwa na ada na niwakate elfu hamsini kwa mwezi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio neema ambayo naweza kuirejesha, bila ya wao mimi nisingelifika nikaitwa Raza hapa, kwa hivyo natoa wito kwa jimbo langu la Uzini na nitakaa na kuhakikisha baada ya kumaliza Uzini nitashirikiana na Majimbo yote ya Unguja na Pemba kuona tunaweza kusaidiana kwa pamoja.

Mwisho, mimi niwapongeze wafanyabiashara wa Zanzibar, kina Bombay Bazaar, Turky na wafanyakazi wengine Simba Chai. Mhe. Naibu Spika, nataka kuwaambia Wawakilishi Serikali yetu sikivu, chakula hakijapanda bei, chakula kipo cha kutosha na naomba Mheshimiwa waambie Wawakilishi kwamba *rate* tuliyowekewa sisi Zanzibar kwa wananchi, nguo, chakula ni *rate* ya aina yake katika Afrika Mashariki na Kati. Kwa hivyo nilikuwa natoa wito kwamba wafanyabiashara tunaingia mwezi wa Ramadhani tujaribu kupunguza na kutumia zakka zetu tuwasaidie wananchi bila ya kujali rangi, kabila au dini, hawa ni wenzetu wachache tu, lakini ninachotaka kusema msimamo wa wafanyabiashara kuna chakula cha kutosha, wafanyabiashara watahudumiwa na tuko tayari kwenda kuwahudumia kokote kwa kupata chakula kilichokuwa kinakubalika na *TBS* pamoja na bei zake; sukari, mchele, unga wa ngano, nguo vitu vyote hivyo vipo vya kutosha.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kupata fursa hii leo kufika hapa sote kwa pamoja, na nilishtuka mwanzo pale kuitwa Simai Mohamed Simai lakini sasa nashukuru umeniita jina langu kamili ni Simai Mohamed Said. Jina la Simai kwa faida ya wote ni jina la Marehemu babu wa bibi ambaye anaitwa Bimwanakweli Simai Hassan kule nyumbani, Mungu awarehemu wote wazee wangu.

Nianze pia kwa kuwashukuru na kuwapongeza pia Wajumbe wote leo kufika hapa, na kwa kuchaguliwa kwa wingi wa kura. Pia nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ushindi mkubwa alioupata.

Pia, nichukue fursa hii pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kwa wingi pamoja na Makamu wake Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Mhe. Naibu Spika, kuna methali ya Kiswahili inayosema kwamba "Kamba yangu ndefu lakini haifungi kuni". Hapa ninamaanisha kuwa kuni ndio bajeti na kamba ndio sisi. Kwa maana hiyo inabidi kamba tuitoe mafundo tuinyooshe

na tuifanye iwe imara ili tuweze kufunga mzigo wetu wa kuni, na hiyo niseme kwamba Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio kazi yetu sisi hapa sote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuliokuwepo kuweza kuisadia na kuishauri Serikali.Lakini niseme kabla sijaanza kutoa mchango wangu ningependa tufanye masahihisho kwenye ukurasa wa 38 wa hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kifungu namba 71 anasema:

"Serikali itaendelea kutekeleza programu ya mjumuisho ya kuendeleza utalii, kufanya utafiti wa hali ya utalii na biashara katika visiwa vya Fundo, Kokota, Njao, Bawe, *Prison Island* na Changuu; kuanza ujenzi wa vituo vya usalama na kuandaa maonesho na matamasha ya kibiashara".

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba *Prison Island* na Changuu ni kisiwa kimoja kwa mujibu hapa inavyoonesha, kuna Chumbe, kuna Bawe, kuna *Prison* na kuna *Grave Island.* Sasa hapa sijui itakuwaje, lakini pia katika kifungu hichi ningependa pia Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake atueleze maana yake ni matamasha gani ya kibiashara hapa ameyakusudia kwenye visiwa hivi.

Mhe. Naibu Spika, sasa niruhusu niende kwenye mchango wangu na nitaanza moja kwa moja na deni la Taifa. Mhe. Waziri, aliposoma hotuba yake alizungumzia kwamba katika kipindi cha miezi tisa iliyopita Serikali imekopa jumla ya bilioni 10 ikisababisha deni la Taifa liongezeke kwa asilimia 5.7 sawa na bilioni 398.6 za Tanzania kufikia Machi, 2016. Hili limetoka kutoka bilioni 317.2 hapo Machi, 2015.

Mhe. Waziri atakapokuja nataka nifahamu kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali hili deni linawekwa katika *account* gani ya shilingi au dola, maana yake amezungumzia kwamba kuporomoka kwa dola pia inasababisha hili deni kuongezeka, sasa kama kuna mfuko unawekwa maalum je, ni wa shilingi au ni wa dola, kama ni wa dola basi nitaridhika na maelezo. Lakini kama sio wa dola ningependa kufahamu kwa nini haujawa kama upo nafikiri hili linakuwepo kwenye *Consolidated fund.*

La tatu ukuaji wa uchumi umezungumziwa kwamba usipungue asilimia nane (8%) na umetaja hususan suala la biashara ya utalii kwenye kipengele cha (f) 39 na pia imesemekana imekuwa inazungumzwa pia kwamba asilimia 80 ya fedha za kigeni zinatokana hapa kwenye biashara ya utalii.

Mimi nitapita juu juu kutoa mawazo yangu na fikra zangu kuweza kuisaidia Serikali na kuishauri, lakini katika umuhimu huo nataka kufahamu ili

kuhakikisha hii biashara inakwenda vizuri na inakuwa endelevu ni viashiria gani wanatumia Serikali kuulinda huu utalii. Najua Serikali inajipanga kutafuta masoko mapya, na naelewa hii ni kazi ya Waziri husika katika biashara hii ya utalii na yeye ndiye mwenye mpango mzima, lakini pia kwenye mpango huu ambao Wizara hii ya Fedha na Tume ya Mipango pia mnahusika nahisi moja kwa moja kwenye Dira ya Taifa.

Mhe. Naibu Spika, kuna maneno ambayo na hisia inakuwepo kwamba Zanzibar ni kisiwa pekee na wageni watakuja tu hapa. Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nikupeni mifano ya visiwa ambavyo viko vizuri ambavyo vina mvuto pia kama vya kwetu vya Unguja na Pemba. Kuna visiwa hapa Ugiriki kuna Crete, Rhodes, Pelion, Santorini, Velanio, Serifos, Naxos, Mykonos, na vingi vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, pia ukienda Thailand kuna visiwa vya Krabi, Koh Chang, Koh Samui, Ko Lanta, Phuket. Na hapa kusini mwa Comoro kuna Panarea, Tenerife, Grand Canaria, Lanzarote, La Palma, La Gomera, Fuerteventura.
Ukienda kwenye *Spanish costas*; kuna Costa Del Sol, Costa Brava, Costa Blanca, Costa del Maria na nyingi nyengine.

Ukienda huku South Asia, kuna Indonesia, kuna Bali, Java, Sumatra, Borneo na Lombok; hivi vyote ni visiwa wala sitaki kuvigusa hivi visiwa hapa vya Sychelles na Mauritius Lakini pia kuna Morocco na Tunisia tunashindana nazo na hapa kote ndipo kwenye ushindani.

Mhe. Naibu Spika, sisi sote kabla ya kuingia kwenye Baraza hili tulifanya kampeni ili kujiuza kwa wananchi, hapa nataka nieleweke kama hatujitangazi tusijilaumu. Ukitaka upate pesa lazima utumie pesa. Tunashindana na watu wengi huko nje, kuna maeneo mengi mazuri yenye mvuto, tumpe pesa Waziri wa Utalii aende akafanye hiyo kazi ili hayo malengo yafikiwe, tusimuonee Waziri wa Utalii wakati mwenyewe pesa hana, atafanyaje hiyo *promotion* ya Zanzibar. Tunalaumu sana tunapiga kelele, kwa hivyo lazima tujipange.

Na mimi hapa nataka niishauri Serikali na hasa Mawaziri ambao wanasimamia katika masuala yote, mimi nashauri muunde *Think Tank* ambayo itaendana katika hii *Public Private Partnership* ili mapato yetu yaongezeke na tuweze kujipanga. Jina la Zanzibar lazima litangazwe kuna *Opportunity* nzuri za kufungua milango. Natoa mfano wa michezo ya kuigiza (*filming industry)*, kuifanya Zanzibar mojawapo ya *location* zitakazotumika katika sehemu ya kuigiza, tunajua kule kuna *Hollywood*, kuna *Nollywood*, kuna *Bollywood;* hawa wote tunaweza kuwaalika wakaja hapa Zanzibar, tuangalie mchezo Mhe.

Naibu Spika, kama amewahi kuuona unaitwa *Out of Africa* wali- *act* Nairobi mwaka 1984 mchezo ule ulishinda katika *Oscars,* na mpaka leo unajulikana Duniani kote, lakini umeweza kuitangaza Kenya katika kila nyanja ya nchi yao, mbuga zao watu wamejua Kenya kutokana na mchezo mmoja.

Uangalieni mchezo unaitwa *The Ghost and the Darkness* unahusiana na masuala ya simba wanaokula binadamu. Mchezo ule ni kuhusiana na Kenya lakini umerekodiwa *South Africa.* Hii ni *Opportunity* ambayo tunaiacha, lakini hapa ndipo kwenye sanaa ambayo itaweza kunyanyua sifa za nchi kwa Jamhuri yetu pamoja na visiwa vyetu vya Zanzibar, tuangalie hii nafasi tunaweza kui-*capture* vipi Mhe. Waziri, ili hayo mapato tunayoyataka tuweze kuyapata, lakini unapotumia shilingi kama hii nchi yetu unapata kuitangaza moja kwa moja hutumii pesa utaandikwa katika magazeti, matangazo utaoneshwa maeneo mengi kabisa.

Lakini pia uwezekano wa Jina la Zanzibar kuwa linasikika duniani mnaweza kuwaalika waandishi maarufu kwenye majarida tofauti, kuna *Hindustan Times*, kuna *The Telegraph*, kuna haya magazeti mengi duniani wanaweza kualikwa hapa mkazungumzia mambo ya nchi lakini pia mkapachika pia na masuala ya utalii ili tuweze kuitangaza nchi yetu.

Leo nchi yetu tunatangaziwa kutokana na waandishi wanavyotaka wao huko nje. Matokeo madogo ya Zanzibar yanaandikwa vibaya yanatuletea sifa mbaya nje kwa sababu Serikali haifanyi wajibu wake, kwa hivyo lazima tukazane na sisi.

Katika hotuba ya Mhe. Rais nilitoa mchango wangu nilizungumza suala la *visa* tunaangalia mapato, Zanzibar tunakwenda kwenye *Seasonal Business;* ya msimu, tuna vitanda karibu sasa hivi itakuwa elfu kumi na tatu au kumi na nne vitanda nusu ya mwaka vinakuwa viko vitupu, mnapiga kelele wageni hawalipi lakini pia vile vitanda vinatakiwa vilaliwe na wageni kwa nini hamuangalii kwa kushauriana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano mkaondoa *visa* wakati wa *low season,* mkifanya hilo mnakwenda hapo Nairobi mnachukua wazungu wote na wale wote ambao raia wanaoishi pale sio wananchi waje Zanzibar bure *week-end,* mtawaachia hao wawekezaji wafanye *promotion* na *packages* na *Kenya Airways* waje hapa Zanzibar. Leo kitanda kinalala kitupu bure bure kwa nini, wakati tayari Kigali kuna watu, Nairobi hapo kuna watu wa *UN* zaidi ya watu elfu kumi na tano wameajiriwa.

Na hapa ninapozungumzia suala la *visa* niseme hata hii *low season* mimi Mhe. Waziri, na Mawaziri wote mliokuwepo hapa nataka nyinyi kwanza muwe

mabalozi wazuri wa nchi yetu muache kuanza kusema hizi kauli za *low season* mnaiua nchi, hakuna cha *low season*, mkisema *low season* mnasema wageni wasije, iteni *the green season*, msimu wa kijani.

Waarabu wanapenda mvua, twendeni kule tukawaalike waje. Mimi dada yangu anaishi Arabuni, akisikia mvua inanyesha anatoka nje anacheza kwa furaha, maana yake mvua hawaioni. *South Africa* ndio wanavyoita *The Green Season*, tafuteni jina zuri ili wageni waje, mnavyosema *low season, low season* maana yake mnawakataa wageni wasije ni *low season,* tufanyeni kazi mwaka mzima wageni hapa waje na huo ndio wajibu wetu sisi ili tukitaka fedha tupate.

Pia, nataka nitoe tahadhari moja ni sahihi kuweka malengo ya kukusanya bilioni 800 nimeona hapo ikifika 2020/2021, lakini ni vizuri mkaangalia *alternative measures* za kwenu Mhe. Waziri naomba Mhe. Naibu Spika, hili waliangalie sana kwanza kwa nini msifikirie kuanzisha na kujenga au kualika (*international multi companies)* makampuni yaje kuanzisha hapa *Assembling Plants* katika maeneo ya Fumba. Zipo kampuni zitakuwa ziko tayari, kuna soko la Afrika ya Mashariki na Kati hapo kuna watu zaidi ya milioni mia moja wanahitaji huduma tofauti. Mnaweza mkachukua na kuwaalika watu wa *NOKIA, SAMSUNG* wakafungua eneo la Fumba wakaja na vifaa vyao wakafanya *Assembling Plant* tukachukua zile TV, Simu katika mahitaji ambayo hayatengenezi katika Afrika ya Mashariki halafu tukaenda tukawauzia kule mtapata ajira ya watu wengi, mtakuwa mna soko ambalo mna uhakika nalo mnauza na mtaitangaza Zanzibar kibiashara, lakini hili eneo limekuwa linapigiwa kelele pamoja na Micheweni, lakini sasa hivi angalau kuna kiwanda cha maziwa kimejengwa, kuna mpango wa majumba. Lakini fungueni tunataka *International Companies*, msikae mkasema utalii, leteni makampuni haya ya nje yaje hapa tuyaone, na niwapongeze sana hapa. Sasa hivi hapa Mji Mkongwe tuna hoteli yetu ya *Park Hyatt* ni katika hoteli kubwa nzuri, 5 *stars, East Africa* hakuna, kwa hilo lazima Serikali niwapongeze sana, *well done!*(*Makofi*)

Lakini sambamba na hili Mhe. Naibu Spika, lazima Wizara mjiangalie katika mpango mzima wa suala la umeme hii *submarine cable* yetu inachukua 100 (*MW)*, ule waya wa zamani unachukua 40 (*MW)* tuna mpango sasa wa kujenga na tumefungua milango kwa ajili ya kujenga *Real Estate* tuna kampuni inajenga Kaskazini, tuna nyumba zinataka kujengwa na kampuni ya Bakhressa, tuna nyumba zinazojengwa na *ZSFF* hapa Mbweni, umeme wetu utazidi kuongezeka na *demands* ya umeme inakuwa iko juu baina ya saa 12.00 ya jioni na saa 4.00.

Kwenye suala la umeme mnajipanga vipi, kwa sababu ikiwa *demand* itashuka na katika miaka ijayo tunategemea *cable* ya *MW* 100 isije ikaanza kuzidiwa sasa, lazima muanze kuangalia katika miaka ya mbele tutakwenda vipi. Na kama ule waya wa *MW* 40 japokuwa una uwezo wa kuchukua *MW* 45 lakini uwezo wake ni 40, je tutaweza kuutumia ili twende kwenye 140, kwa hivyo umeme wetu na haya tunapotaka ku-*expand* lazima tuwe waangalifu. Mhe. Naibu Spika, wazungu wanasema y*ou can not expand without control* kwa hivyo tuwe waangalifu katika umeme wetu tujipime na tuangalie wapi tunapokwenda.

Nataka pia Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho yako unieleze tena kwa kina suala la *E. Government.* Najua Mhe. Rais alifungua ule mradi na ikafanywa pale wakati wa Sherehe za Mapinduzi, nataka tuelewe huu mradi unakwenda vipi, matumizi yake yakoje, na mlikopa pesa nafikiri katika *Exim Bank* ya China, sasa nafikiria umesema kuna hatua ya pili, hiyo hatua ya kwanza wananchi wa Zanzibar na Serikali wamefaidika vipi.
Pia, sambamba na hili nataka nitoe ushauri kuhusiana na MV Mapinduzi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilijikhini na pia iliwanyima wafanyakazi wake matumizi ya kila aina ili tununue meli yetu ile *MV Mapinduzi II.* Kwa kweli meli ni nzuri na safi kabisa, na mnastahiki kupongezwa kwa hali na mali.

Mhe. Waziri wa Fedha na nakumbuka na Katibu wako yupo pale juu, lakini sitogeuka nyuma kumuangalia nataka anisikie, nakumbuka alisaini baada ya siku ya uzinduzi malipo ya awamu ya tatu na tumelipa bilioni zaidi ya sabiini (70) kama sikosei, zilikuwa 31 *point something million Dollars* labda zitakwenda kwenye bilioni 72 au 73, lakini pesa hizi wamelipa wananchi na walipa kodi, hii meli Mhe. Naibu Spika, tunaiangaliaje kuhakikisha kwamba hivi fedha zilizotumika katika hii meli zitaweza kutumika ipasavyo, hii meli ilindwe, mtaitumia njia gani.

Mhe. Naibu Spika, tulipokuwa kwenye semina yule aliyekuja kutusaidia kutufundisha nilimuuliza kwenye suala la meli unatoa wazo gani ili meli yetu tuilinde, akashauri mnaweza kuingia mkataba pengine na kampuni za binafsi ili mkaisimamia vizuri. Sasa utakapokuja Mhe. Waziri tueleze hizi bilioni sabiini unazilinda vipi katika miaka ishirini ijayo tutafaidika vipi, na wananchi wa Unguja na Pemba naamini wanataka kujua tayari maneno yako nje kwamba hii meli keshokutwa hamna kitu. Sasa tunataka tujue.

Jengine ni kuhusiana na uwekezaji wa ndani na nje Mhe. Naibu Spika, ni lazima Serikali yetu ichukue juhudi za kuwalinda maneno mengi yanasemwa

kwamba wafanyabiashara ni hivi na hivi, lakini Zanzibar tunategemea utalii biashara na huduma, wanaolipa ni hawa hawa wanaotusaidia tuwathamini, tuwapende, tusiwakejeli. Na sisi pia Waheshimiwa tuwe makini sana tunapowasema hawa wafanyabiashara wetu, isifike wakati wa kampeni tunakwenda kuomba tusaidie huku, huku, tunachangia wanafanya kazi nzuri tuwapende na tuwathamini, makofi basi! *(Makofi)*

Ni muhimu pia Serikali kuhakikisha kwamba hapatokei migongano na hizi Halmashauri zetu. Wakati mwengine Serikali mnajipanga na mambo yenu, lakini inatokea migongano na Halmashauri zetu, wanasema yao kule kuwasumbua wawekezaji na wananchi, wakulima wadogo wadogo, wafugaji na huku Serikali ina mpango mwengine, lazima tucheze mchezo wa karibu sana, wananchi tusiwasumbue na wafanyabiashara tusiwasumbue.
Mhe. Nabu Spika, nataka niseme suala zima la ajira. Ni kwamba tukitaka vijana wafaidike na ajira niseme kabisa ninavyoamini mimi basi Chuo cha Karume hiki hapa lazima tukikamate, tukithamini na tukipende ili twende tukawasomeshe vijana wetu.

Tena mimi hapa nataka nimshauri Makamu wa Pili wa Rais pamoja na waziri husika wende wakaangalie ile hali ya chuo ilivyo, mtu anasoma *refrigeration*, *marine engineering*, *mechanical engineering*, *electrical engineering* anatumia *machine* ya mwaka 1947 unatarajia leo ataajiriwa vipi nje. Anatumia *switch board* ambayo inahitaji kompyuta ndio maana mnapiga kelele hizi kazi zinachukuliwa, *mechanical engineer* si kwenye mahoteli, kwa sababu hawa watu wetu pia wanakuwa bado ule uwezo wanafundishwa lakini haipo, anajifunza kuwa *experience* anaweza akakosea pale akaripua dude lote likamripukia yeye.

Kwa hiyo, tuwaelimishe twende tukakiangalie kile chuo pale Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na waziri husika aangalie, ili kile chuo tuweze kuunganisha zile ajira zilizokuwepo nje pamoja na chuo chetu, ili tuweze kuwasaidia Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, na pia katika huu mpango mkuu wa Tume ya Mipango ni vizuri Mhe. Waziri mkaipitia hii sheria ya manunuzi, kwani kuna changamoto nyingi sana katika sheria hii. Katika mahitaji ambayo hayapatikani Zanzibar kwa nyinyi ambao mko serikalini na munahitaji, hivyo kunahitajika maamuzi tena ya haraka kubana na kuokoa hizi fedha ambazo mnatumia nyingi bila ya mpangilio.

Vile vile nataka niseme kuhusu safari za nje ambazo Mhe. Naibu Spika, imegusiwa katika hotuba. Nasemaje anayestahiki kwenda nje aende, asiyestahiki asiende, tusije tukabaki Wazanzibari hapa na serikali yetu tumekuwa tunapitwa na mambo yanayofanyika duniani.

Dunia mambo yanakwenda kwa kasi sana, wataalamu ambao tunawajua wameshajifunza kama kuna semina, kuna mkutano muhimu waende, wakirudi watakuja kutusaidia tusiwabane watendaji wa serikali tukawaambia wasisafiri. Baneni matumizi wakitumia kama ndege *first class* wawekeeni kwenye *economy class*, ndege dola 300 viko vyumba vya bei nafuu waende wakajipange kama kweli na wao wanataka kutusaidia nchi yetu, lakini kwenye mikutano waende. Utaratibu utumike mpya lakini waende, mimi nashauri waende.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu magari Mhe. Waziri alizungumzia katika hotuba yake, ni wazo zuri la serikali kusimamia mapato tofauti. Magari ambayo yatakayotoka kwenda Tanzania Bara ambayo mapato yake yatakuwa yanalipwa Zanzibar, hili jambo Mhe. Waziri nawapongeza sana serikali kwa kuja na wazo hili, lakini ningependa kujua haya mapato kwa kweli yatabakia hapa hapa Zanzibar? Najua yanabaki Zanzibar lakini atuhakikishie yanabaki hapa Zanzibar.

Vile vile, Mhe. Waziri kuna suala moja la msingi kama unanisikiliza. Mhe. Naibu Spika, nasemaje magari ambayo yanayotoka nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Kenya, kutoka Malawi, kutoka Mozambique yanaingia Tanzania kwa miezi mitatu wanapewa *temporary permit* ya kuingia, wanalipa dola 100, dola 40. Leo Mkenya anabaki na miezi mitatu anatembea na gari yake ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini Mzanzibari ukimuachia yule sio mfanyabiashara leo anataka kutoka na gari yake kwenda Tanzania Bara kwa matembezi, fursa hiyo anasumbuliwa hawezi kuondoa gari yake akaambiwa kuna utaratibu huu, huu, huu na huyu ni Mzanzibari, Mtanzania, ndani ya nchi yake hawezi kuondoka. Kwa nini iwe hivi?

Mhe. Naibu Spika, watu 200 wanaofanya biashara ya magari hilo ni la kwao, lakini Wazanzibari waliokuwa wengi wanataka waende wakatembelee jamaa zao, waendelee kwenda kutembea huko kwenye Jamhuri ya Muungano, waende kwenye mbuga, skuli zinafungwa hawawezi pengine kulipia matumizi mengi lakini waende na gari zao wazitie katika *Azam Sea Link*, aingie hapa atoke pale lakini anasumbuliwa. Nataka Mhe. Waziri atakapokuja hapa utueleze kwa nini hili jambo linatokezea.

Pia, nataka nizungumze suala moja ambalo mawaziri wote wapo hapa waliangalie kwa kina kama litawezekana. Biashara ya utalii sio kwamba inavyochukuliwa tu ni biashara ya kuuza nyanya, mboga na vitu vyengine. Hii ni *industry*, pia inahitaji utaalamu na utaalamu wake lazima watu wetu tuwasomeshe ili wawe na elimu ya kutosha, wazungumze lakini pia waweze kufanya hizo kazi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashauri kama itawezekana tuna ndugu zetu kutoka Bara wanafanya kazi hapa ni Watanzania wenzetu, tuna Wazanzibari wenzetu wanasoma hapa pia. Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambao wao ndio wanatuunganisha sisi na Jamhuri kule na Ofisi ya Makamu wa Rais, waangalie kama kuna uwezekano wa kujenga Chuo cha Utalii cha Jamhuri ya Muungano hapa Zanzibar cha kisasa, ili vijana wetu wote waliokuwepo hapa waende waka-*raise criteria* zao za masomo ili waweze kupata hizi ajira na wazidi kujiendeleza.

Nasema hivi kwa sababu chuo chetu tunafahamu kina changamoto zake, japokuwa na serikali yetu inafanya kazi nzuri, ni kwamba tunapoangalia ajira ndani ya utalii tusiangalie ajira za ndani, tuangalieni ajira pia za nje. Kuna Wakenya zaidi ya 15,000 wanafanya kazi Dubai kwenye hii *hospitality industry*, kwa hiyo tuwasomeshe vijana wetu watoke nje na wao waende zao Marekani. Leo unasikia kuna Meneja Mzanzibari anafanya kazi Brazil, anafanya kazi China, anafanya kazi Jamaica lakini lazima tuwasomeshe. Kwa hiyo, tuanzeni hapa hatujachelewa.

Pia, hapa hapa naunganisha kama inawezekana tujenge *boarding school* ya kisasa. Pia, kule kwenye Kisiwa cha Uzi Kusini Unguja au Pemba inawezekana pia, *boarding school* ya kisasa ili vijana wakasome kule wapige kitabu, wakirudi hapa wanakuwa wako tayari, na hiyo *boarding school* watakuja watu kutoka nje kuja kusoma. Tumeona mfano wa *Zanzibar University* wanapokea wageni wengi sasa hivi kutoka nchi jirani, na sisi twende katika hatua nyengine pia, tubadilike.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naomba niseme kwamba ninaunga mkono hoja, lakini nitafurahi sana na nitaridhika zaidi Mhe. Waziri aliyesoma bajeti na muhusika mkuu atakapokuja hapa anipe maelezo ya kina kuhusiana na deni la Taifa. Nitahitaji maelezo mazuri ambayo yataweza kunipaka siagi niridhike.

Pia, Mhe. Waziri nataka nimtakie kila la kheri na wataalamu wake na watendaji wake wote katika kutafuta hizi bilioni 324.8 za mikopo na nyengine

wanazozitaka ili kuifanya hii bajeti ikamilike. Naamini Mhe. Waziri ni muadilifu, hodari, mchapakazi na ataliweza kulifanikisha hili ili bajeti yetu iweze kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, lakini kabla sijamaliza hapo nataka nimshauri katika suala la *programme* ya *PBB*. Hii *program* tumepata tabu sana kuipitia hebu Mhe. Waziri iangalie kwamba *programme* hii uliyokuwa nayo ya *PBB*, maana yake kama utampa mtu milioni 2,000,000 lakini anahitaji *activities* zaidi ya kumi, tano, sita kuzifanya ukampelekea milioni 5,000,000, kwenye *programme* yako *activity* yako haitaonekana. Mimi nakushauri kama itawezekana muanzishe *programme* ambayo itakuwa *realistic* ya pembeni, ambayo itakuwa inakidhi haja zenu kama taasisi au ile idara itapokea milioni 50,000,000 basi ile *breakdown* ya matumizi yako utaiona. Hii *PBB* bado tuna mtihani nayo, lakini ni wazo zuri, yaani *programme* hii itafanya kazi zaidi vizuri kwa nchi ambazo zina fedha za kutosha na wao hawana *benefit* kwenye bajeti. Ninaamini kama utaangalia kwa undani Mhe. Waziri na Waheshimiwa Wajumbe hili tuna mtihani wetu hapa.

Kwa hiyo, baada ya hayo maelezo yangu machache nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni yangu, nitasubiri wizara zinazokuja ili niweze kutoa mawazo yangu ya kina kuhusu jimbo langu na kuwapa maelezo zaidi.

Baada ya hapo naitakia serikali kila la kheri na naunga bajeti hii mkono mia baada ya mia kwa maelezo yangu niliyoyatoa. Ahsanteni. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa muda uliobakia ni mchache sana ni dakika 10 tu, na nafikiri itakuwa sio vizuri kumpa Mhe. Nadir aanze, sidhani kama ataweza kumaliza, Mhe. Nadir unaweza kuchangia?

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ndio.

Mhe. Naibu Spika: Haya Mhe. Nadir, karibu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, mimi nitachangia muda mdogo, unanitosha muda wa dakika 10.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uzima na kunijaalia kufika salama na nawashukuru watendaji wote waliofika hapa kwa uzima kabisa. Kwa kweli mimi nitachangia hotuba ya serikali nitaanza na suala la uchumi.

Mhe. Naibu Spika, uchumi bila ya sisi wenyewe kukaa kwa makini na wizara husika zinazohusiana na mapato kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango katika kuhakikisha kuyakamata yale mapato yanavyotakiwa, na sio kuachilia yakapenyapenya katika njia isiyojulikana. Kinachotakiwa katika uchumi wetu kwanza tujipange sisi wenyewe ndani ya serikali halafu ndio tuangalie uchumi ambao tutatoka nje ya serikali au ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wizara zinazohusika na mapato yote wanatakiwa wawe makini kwenye kukusanya mapato hayo na vile vile wawe karibu sana kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha, ili kumsaidia makusanyo hayo yakamilike vile inavyotakikana. Nitatoa mfano kwenye suala la utalii sisi tunategemea sana utalii, bandari, *airport*, karafuu na masuala mengine katika *income* zetu za serikali yetu ya Zanzibar.

Kwenye suala la utalii ningeshauri au ningetoa pendekezo langu. Sasa hivi tuna *system* ya kwamba *ZRB* au *TRA* ni kwamba *TRA* wanaweza waka-*charge* mfano kwa mwaka wakam-*charge* mtu akalipa *in four terms*, yaani miezi mitatu, mitatu, mitatu, au sita sita au mwaka *direct*. Hii *ZRB* ningemshauri Waziri wa Fedha kama inawezekana akaweka *fixed rate* kwa ajili ya mahoteli makubwa au *standards* za kati mfano mdogo tu mahoteli mengi yana historia miaka mitano au kumi nyuma ulipaji wake ndani ya *ZRB* au *TRA* wanayo historia hawa wanalipa kiasi gani. Sasa haya mapato wakayachukua wakaangalia mwaka 2010 amelipa bei gani, 2012 kalipa bei gani, 2013 kalipa bei gani.

Kwa mwaka huu serikali ili isipate matatizo ya kutoa watu wa *ZRB* kila siku kwenda kwenye mahoteli ya shamba na ya mjini kwenda kuuliza vyumba, kuchukua funguo za vyumba, kwenda kupekua vyumba. Haya yote yanasababisha matatizo makubwa kwa wafanyabiashara wa mahoteli na pengine na wageni waliokuwepo pale. Kwa kweli kama serikali au Wizara ya Fedha itashirikiana na vyanzo vya mapato wakaweka *fixed rate* kwa ajili ya wale wafanyabiashara wakubwa wakawapangia tu kwa mwaka huu mfano *Kempinski* au *Hyatt Regency* tunataka wewe mwaka mzima utulipe dola 80,000 lakini igawe mara nne kwa mwaka, utatulipa kila miezi mitatu dola 20,000. Hili pendekezo kama linawezekana itakuwa vizuri hata serikali itakuwa ina uhakika inapata kiasi gani kwa biashara kubwa kwa mwaka moja kwa moja bila ya kwenda kila siku kukusanya au kusubiri kwa mwezi.

Mhe. Naibu Spika, nimesema hivi kwa sababu nina uhakika kwenye masuala ya hoteli, rikodi zipo na tunajua siku gani ambapo hoteli zinafungwa, zile

zilizokuwa zinafungwa tunaweza tukawaachia muda wa mwezi mmoja tukautoa lakini ile miezi 11 tukaangalie ile hata *statistics* zao za wageni kwenye ile hoteli ziko vipi wakachajiwa.

Vile vile, ili nchi yetu utalii uzidi na uvutie basi ningemuomba Mhe. Rais na Mhe. Makamu wa Rais akawatoa watendaji wakiwemo Mhe. Waziri wa Utalii, Mhe. Waziri wa Biashara wakatoka nje ya nchi wakaenda mfano kama nchi ya Brazil, Russia, Turkey, India na China. Ni nchi ambazo wananchi wake matajiri sana, sasa hivi wanapata pesa na wanasafiri, lakini mfano kama nchi ya Brazil na Urusi sasa hivi ukienda kuwauliza nafikiri katika watu milioni 1,000,000 hamna hata watu 100 wanaoijua Zanzibar, wengi wanasafiri kwenda nchi nyengine hawaijui Zanzibar. Sasa mimi ningewaomba hata kama labda ile *trip* ya kwenda Mhe. Rais mwenyewe ni kubwa na pesa ni nyingi, basi wangewatoa Waheshimiwa Mawaziri wakaenda kuwatangazia wakaita mikutano ya wale wafanyabiashara wakubwa wa nchi ile ili waitangaze nchi yetu na waombe vile vile kwenye *TV* zile za *states TV* ya ile nchi yenyewe itangaziwe angalau muda wa dakika 10 nchi yetu ya Zanzibar wakapata kuifahamu wale wageni na kuwaeleza hali halisi ya nchi yetu, uchumi wetu pamoja na vitu gani ambavyo tunaweza tukawapa wao vikawafaidisha.

Mhe. Naibu Spika, hili nafikiria likifanyika litaweza kuvuta wageni ambao hawaijui nchi yetu. Kwa kweli sisi tume-*base* sana na nchi ambazo zinatujua hasa za *European Union*, ukisema *America* labda nchi tatu tu au nne *United States*, Canada ndio nchi ambazo zinaijua Zanzibar lakini ziko nchi ambazo zina matajiri. Venezuela huko, Cuba na nchi nyengine ambazo wanataka ku-*invest* mambo ya *industry*, mambo ya mahoteli lakini hawaijui nchi. Kwa hiyo, ningeomba wangetoka hata kama alivyosema Mhe. Simai kwamba sio lazima wasafiri kwa *first class* wachukue *economy*, mawaziri wanaweza wakapanda mfano hata *business class*, *first class* kutokana na hadhi yao lakini wale watendaji wengine wawili watatu wakapanda *economy*.

Mimi kwa suala hili la kutangazia nchi yetu hata mimi binafsi niko tayari kujitolea tiketi mwenyewe, pesa za matumizi kwenda kutangaza nchi yetu katika nchi ambazo tunajua uchumi wake unakua kama Brazil ina pesa nyingi, wananchi wake ni matajiri wanasafiri Urusi, Ukraine sasa hivi ni nchi ambazo zile zenye vita kama Syria, Egypt, Turkey sasa hivi matajiri wote wanataka kutoka kwenye ile nchi waje kutafuta nchi nyengine ambazo zilizokuwa zina usalama wa-*invest*. Nchi yetu kwa kweli ina usalama wa hali ya juu na inakubalika.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kuhusiana na suala la wageni ningeshauri wizara zote zinazohusika, watalii tunatakiwa tuwaenzi kwa sababu wao ndio wanaotupatia kipato kikubwa kwa kuja kwao. Mfano mdogo ukianza *airport* mgeni ametoka Canada, ametoka America masaa 18 au masaa 22 kufika Zanzibar, matokeo yake akifika pale mabegi anabebeshwa, mtu anafika kumwambia mimi siwezi naumwa na mgongo, hakuna wa kumsaidia ndani ya *airport* yetu ya Zanzibar, anabebeshwa mzigo mwenyewe akiwa mtu mzima ana miaka 70, akiwa miaka 50 anabebeshwa anapitishwa kwenye *screen* inatoka. Mhe. Naibu Spika, akitoka hapo mgeni amepanda gari anakwenda zake Nungwi basi atakutana na *traffic* zaidi ya mara 12 anasimamishwa, ataanzia…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika tatu malizia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana.

Vile vile, ningeomba sana vile vituo ambavyo havina umuhimu vya kukera wageni vikasimamisha, mgeni anatoka *airport* amechoka, masaa yote mpaka kufika Nungwi anasimamishwa mara 12 anapekuliwa. Hili naomba sana liondoshwe linakera wageni na linawaudhi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, suala la kuweka *camera* katika mji. Nchi nyingi sasa hivi *traffic offences* zinaingiza pesa kwa kupitia zile *camera*. Kutumia 8 bilioni shilingi kama ni kwa nchi ishakuwa na uhakika itaingiza sio tatizo kwangu mimi, kwa sababu kuweka zile *camera* kwanza sasa hivi dunia imeharibika nchi inatakiwa iwe na ulinzi, lakini *camera* zile waziweke katika kuingiza *income* ambazo zitakamata wale wanaotumia njia vibaya, wahalifu kuwafanyisha *charges* ili zile *camera* zikawa zinazalisha kipato.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda mdogo uliobakia mimi naipitisha au naweza kuja kuchangia tena jioni kidogo nitapoingia, lakini kwa sasa hotuba hii naipitisha mia kwa mia mpaka hapo jioni nitaendelea tena kidogo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir, na kwa kuwa bado muda wako ulikuwa haujamalizika kwa hiyo unayo nafasi tena jioni ya kuja kuendelea kuchangia.

Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa utulivu wenu lakini pamoja na michango yenu ambayo mumechangia, na ningeomba niwasomee majina ya watu ambao wataanza kuchangia jioni tukiingia ili muwe tayari kwa hilo.

Waheshimiwa Wajumbe, watakaoanza kuchangia atakuwa ni Mhe. Nadir Abdul-latif, baadae atafuata Mhe. Shehe Hamad Mattar na baadae atafuata Mhe. Suleiman Sarahani Said, hao ndio watakaokuwa wachangiaji wetu tutakaporudia tena jioni saa 11:00.

Waheshimiwa Wajumbe, tena ningeomba nitoe tangazo ambalo linatoka kwa Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na kuwaomba Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Mwanasheria Mkuu wakutane kabla ya kutoka hapa.

Baada ya matangazo hayo Waheshimiwa naahirisha kikao hiki hadi jioni saa 11:00 jioni ya leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii tena kumalizia muda wangu na niwashukuru wajumbe wote kwa kushiriki tena kwa wakati wa jioni.

Kwa kweli niliishia suala la *camera* za mjini ambazo serikali imeona umuhimu zaidi kuweka katika mji wetu wote wa Zanzibar. Hili suala nililizungumza hapo asubuhi na naendelea kulizungumza tena kwa ufupi ili niendelee na mada nyengine.

Mhe. Spika, kwa kweli *camera* zina malengo yake, serikali haijaweka *camera* zile kwa kupoteza pesa, lakini serikali imeweka *camera* kwa manufaa ya kulinda nchi yetu kwa ajili ya utalii wetu pamoja na kulinda wafanyabiashara na mali zao wakiwemo wananchi wenyewe wa Zanzibar, pamoja na wageni tunaowapokea kutoka nchi tofauti. *Camera* zile zina malengo mazuri katika serikali yetu na uwekaji wa *camera* sio Zanzibar tu bado sisi tumechelewa kuziweka, ukienda nchi nyengine wanazo *camera* zaidi ya miaka 50 nyuma ndani ya miji yao ambazo zinawasaidia sana kwenye masuala ya uhalifu na kuweza kuona jambo lolote linalowakera au linalowahusu wageni katika nchi ile, au matukio mbali mbali yanayofanyika ya uhalifu kuweza kuya-*control* kwa wepesi kabisa.

Vile vile, nilitoa mawazo hizi *camera* zisiwe kazi yake kuangalia watalii kuwasaidia kwenye uhalifu, wizi au masuala yoyote yanayotokea ya kuharibu nchi yetu, *camera* vile vile zitumike kwenye masuala ya uchumi. Kama tunavyofahamu nchi nyingi sasa hivi zinatumia *camera* za aina mbili, zipo *camera* kama hizi tulizoweka sisi zinachukua masaa 24 kurikodi hali halisi ya mji iliyotokea usiku na mchana, lakini kuna nchi nyengine kuna *camera* ambazo ukipita tu, *red light* au kwenye *traffic light* haijakuruhusu wewe ukisema upite unavyotaka wewe inakupiga picha na inajirikodi. Lakini kutokana na *system* hii kwamba serikali yetu bado haijawa nayo, na bei yake pia ni kubwa vifaa vile, ningeomba *camera* hizi zilizowekwa ziweze kuzalisha pesa au ziingize *income* kwa ajili ya *security* kwa wale wanaovunja sheria za barabara na wanaovunja sheria nyengine zozote ambazo hazikubaliani na sheria za nchi yetu ya Zanzibar au Tanzania kwa ujumla.

Mhe. Spika, ningeomba sana kumshauri Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kama yupo au hata Naibu wake, kwa kweli sisi tuna bahati kubwa sana ya *Indian Ocean* na akikaa vizuri akitafakari vipi vya kuzalisha au kuingiza mapato kwa njia ya uvuvi basi tutaingiza pesa nyingi sana katika uvuvi kuliko nchi nyengine tulizonazo.

Kwa ufupi *Indian Ocean* tuna samaki wakubwa wakiwemo Jodari ambao wanaitwa *Tuna*; *Marlin*, Nduaro; *King Fish*, Nguru na samaki wengine wakubwa ambao tunao ndani ya bahari yetu.

Mhe. Waziri, kama atakaa na serikali pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kuangalia vipi wataweza kutengeneza viwanda vidogo vidogo vya hali ya chini na vya *medium size,* ili kuweza kuwainua hawa *locals* ambao ni sisi wenyewe Wazanzibari. Wavuvi kuanza kwenda kuvua *deep sea* kuwafundisha pamoja na kutoa labda baadhi ya boti zinazoweza kwenda kuvua *deep sea* kwa kushirikiana, ili kuwawezesha hawa wananchi wetu wa Zanzibar wanyonge wakaanza kufungua viwanda vidogo vidogo na vya kati. Kwa kweli wakifanya hivi tutaweza kutengeneza viwanda hata kama kiwanda kitakuwa cha serikali, wavuvi watakwenda kuvua na wale samaki watawauzia serikali kwa bei nafuu, basi serikali itapokuwa na kiwanda kile kidogo au cha kati itatengeneza wale samaki kwa njia ya vikopo, njia ya *packet* na kuuza kwenye mahoteli pamoja na nje ya nchi na kupata mapato ya *foreign currency* kwa wingi na tutakuwa Zanzibar wenyewe tumeshaanza kutengeneza samaki kwa kupitia viwanda.

Kwa mfano, sasa hivi hapa Zanzibar kuna mtu anatoa samaki kutoka China nafikiri kwa makontena anauza peduu, baada ya wale kuku wa peduu sasa hivi

kuna samaki wa peduu, na kwa ufupi tukiona wauzaji samaki wengi wameshakuwa hawaendi kuvua au hawauzi samaki *fresh* wanauza samaki wa barafu ambao wanaletwa kwa makontena kutoka nchini China na nchi nyengine ambazo wananunua.

Kwa kweli wananchi wetu wavuvi waliokuwa wanyonge wakipewa elimu hii, wakipewa na vifaa husika ambavyo vitawawezesha kwenda *deep sea* kuvua, basi mimi naamini watavua na vile vile wataweza kuiuzia serikali kwa bei nafuu, na serikali itaweza kufungua kiwanda ili tukaanza kutengeneza samaki wetu sisi wa vikopo kupeleka nje ya nchi pamoja na kuuza kwenye mahoteli, lakini itakuwa samaki *fresh* sio wale wa peduu kama wanaoletwa.

Mhe. Spika, pia kuna kitu kinaitwa *PPP*, (*Public Private Partnership*). Huu ni uongozi ambao naweza nikautolea mfano.

Mhe. Makamu wa Rais wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amekaa nao nafikiri jana hivi na amejaribu kuzungumza nao vitu vya kushauriana na vitu vya kuleta maendeleo pamoja na kuinua uchumi katika nchi yetu. Na mimi namshauri vile vile Mhe. Waziri wa Fedha angekaa na watu wa sekta kama hizi za binafsi, ili wakaangalia vipi wataweza kuinua uchumi kwa pamoja, bila ya kuona tabu na kupanga hili suala kila baada ya muda kuonana na hawa watu ambao wanahusiana na *Public Private Partnership*.

Mhe. Spika, kuna kitu kinaitwa *ZCC, (Zanzibar Chamber of Commerce*). Hii inamuhusu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko; naweza nikasema hivyo sijajua majina yamebadilishwa vipi ya wizara hiyo, lakini inawezekana iko vile vile. Hii *Zanzibar Chamber of Commerce* inamuhusisha waziri mwenyewe ndiye Mwenyekiti wa bodi hii na anatakiwa akaenayo aiite kila baada ya muda hasa kwa nchi yetu iliyokuwa ndogo, basi sio vibaya kila baada ya miezi miwili akawaita wafanyabiashara wa hapa nchini ambao ni *locals* na hata kama kuna *foreigners* basi akawaita akakaa nao, akazungumza na kuangalia vipi hali ya uchumi inavyokwenda kwa upande wa wafanyabiashara wanaoleta bidhaa kutoka nje, na wale wanaozalisha hapa pengine kuuza hapa hapa nchini au kutoa nje ya nchi.

Hii *Zanzibar Chamber of Commerce* ni jambo muhimu sana, na ni moyo katika hii Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa sababu kama atakaa na wafanyabiashara Mhe. Waziri wa Biashara basi atapata mambo mengi, atapata faida nyingi kutoka kwa wafanyabiashara pamoja na kuona matatizo gani ataweza kuyatatua yeye pamoja na wizara yake. Kwa kweli wafanyabiashara binafsi hasa hawa wanaofanya biashara za *local*, ambao ni wenzetu

Wazanzibari wanajitahidi sana kuleta mizigo, kuleta vyakula ambavyo sisi hatuna uwezo navyo, na vile vile wanajitahidi kuuza kwa bei nzuri, japokuwa hali ya uchumi kwa upande wetu Zanzibar sasa hivi si nzuri sana, lakini huko nje sehemu nyingi vitu vimeshuka bei. Hivyo, anatakiwa Waziri wa Biashara akae nao hawa aweze kuwahoji wafanyabiashara hata kama bei wanayonunua aweze kujua ili kuangalia hali ya uchumi Zanzibar atai-*control* vipi kwenye masuala ya vyakula na masuala mengine.

Kwa mfano, wafanyabiashara wa Zanzibar vitu vyote karibu asilimia 70 ya chakula chetu wanakileta kutoka nje; kuanzia mchele, sukari, unga, samli, siagi, vitu vyote hivyo ambavyo vyengine tunaweza hata kuvizalisha wenyewe, lakini hatujaanza ndio maana vinatoka nje. Hivi Mhe. Waziri anatakiwa akae nao aangalie ajue na bei wanazonunua na mambo mengine. Vile vile ajaribu kuwapatia hata bei ambayo ikiwezekana awaambie bwana wee bei hii basi kiuzwe kwa kiwango hiki tunavyotaka sisi kama serikali, tufahamiane muuze hivi vitu.

Pia, *Zanzibar Business Council* hii Mwenyekiti wake Mhe. Rais mwenyewe, nchi nyingi inayo na naamini Zanzibar ipo. Mhe. Rais anakuwa ni mwenyekiti pamoja na mawaziri wote wanaohusika wanakuwa ni wajumbe wake. Kwa mfano, yeye Mhe. Rais anatakiwa kila baada ya muda nchi zilizoendelea au nchi kubwa naamini kila baada ya miezi miwili anaita wafanyabiashara wakubwa wote wa nchi ile *locals* na *foreign investors* kwenye meza moja wanakaa *round table.*

Mhe. Rais anazungumza nao *face to face* wafanyabiashara wote na wale watatoa mchango wao wa kueleza hali halisi ya uchumi na matatizo yao, pale pale Mhe. Rais anao uwezo yeye mwenyewe kuwapa amri wale mawaziri walioko pale, inategemea yule muhusika anazungumza nini. Kwa mfano, atazungumza suala la ulinzi basi atamuinua Waziri wa Ulinzi kutaka ufafanuzi au kutoa pale pale mamlaka kwamba kifanyike hiki. Hili suala litainua uchumi wetu na hawa *investors* wote watahisi kwamba wanathaminiwa wanaitwa na Mhe. Rais kusikilizwa matatizo yao na watapata moyo sana hata wengine kupeana taarifa kutoka nchini kwao kwamba Zanzibar ni nchi nzuri, sehemu ya utalii mzuri, sehemu ya biashara nzuri, Rais mwenyewe yuko pamoja na sisi kwa kutusikiliza pamoja na waziri wake pia ni watendaji. Hili ningeomba sana Mhe. Rais alitekeleze atavyoona yeye kwa njia yake ni vizuri, ili suala hili hata wafanyabiashara waone wanathaminiwa kwa kuitwa na yeye kuliko kuitwa na mawaziri au watu wa chini zaidi.

Mimi ushauri wangu hii *ZBC* Mhe. Rais akaangalie muda wake na kuangalia mfano kama kisiwa chetu ni kidogo au nchi yetu ni ndogo basi akaiweka angalau mara tatu kwa mwaka kuwaita hawa wafanyabiashara, *locals* na *foreigners* kwa pamoja, wakakaa meza moja akawasikiliza matatizo yao na wao wakatoa ya kwao. Hii italeta zaidi uaminifu kwamba sisi wafanyabiashara tunayo *access* ya kwenda kumuona Mhe. Rais na italeta moyo zaidi hata kwa watu wa nje kama nilivyoeleza.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika tano.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana. Mhe. Spika, ili nchi yetu iwe ina uchumi mzuri, basi tuhakikishe masuala mengi ya ndani ya nchi yetu yako sawa kwa mfano barabara. Nitatoa mfano katika *infrastructure* watu wanapotaka kuja ku-*invest* kitu kimoja wanachokiangalia barabara imo, umeme wa uhakika pia wanauangalia uwepo pamoja na usalama wa ile nchi, uwepo mzuri na wengine wanaangalia vile vile *GDP per capital* au *economy* ya ile nchi iko vipi. Lakini kutokana na sisi sasa hivi uchumi wetu sio mbaya kwa mujibu wa hali yetu, na tuna asilimia 17 kwenye bajeti yetu ambayo tunakopa, hii sioni kwamba ni tatizo kutokana na uchumi wa nchi yetu na *Inshaallah* tutapoanza kutoa gesi zetu na mafuta tutakuwa sisi ndio tunaokopesha nchi nyengine.

Mhe. Spika, kwa kweli mfano wa barabara yangu ya Jimbo la Chaani imeanza Kinyasini nyuma kuishia mpaka Gamba. Ile barabara ni maarufu sana, na barabara ile kwenye masuala ya utalii ni muhimu kwa sababu ime-*connect* kuendea Kiwengwa, Pwani Mchangani, Matemwe na mashamba mengine.

Mhe. Spika, leo mtu mgeni anataka kwenda Kiwengwa anazunguka kuendea Donge anapitia Mkokotoni, azunguke ndio aende kwenye safari zake za hoteli anazozitarajia wakati ilikuwa ipo njia ya *shortcut*. Njia hii namuomba Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ajitahidi aitie lami kwa sababu ni muhimu sana, na hivi sasa ina mashimo mengi ikija mvua inaweza kusababisha hata ajali, ina mashimo haipitiki wakati ni njia muhimu ina mahoteli mengi *five stars*, *four stars* kwa upande ule. Ningeomba sana, haimo kwenye bajeti lakini Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango angeona umuhimu wa barabara hii itengenezwe kwa kuwa muda mrefu inatiwa kifusi, inawekwa sawa, lakini matokeo yake inachimbuka baada ya mwezi tu. Ningeomba sana ifikiriwe kwa sababu ni moja ambayo wageni itawarahisishia hasa wanapotoka safari zao za mbali kutaka kwenda kupumzika kuliko kupita kwenye mashimo na kusababisha ajali.

Mhe. Spika, vile vile, ningeomba kumshauri Mhe. Rais na Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha umeme tulionao ni umeme ambao sio wetu tunategemea kutoka nchini Tanzania, lakini ningeomba tungejitahidi sisi wenyewe Zanzibar tukaweka njia yoyote ile ya ubunifu ya kuleta umeme wa maji. Kwa mfano, Dubai wanatumia umeme kwa njia ya maji, wana maji ya chumvi pia wanakunywa ambayo wanayasafisha na wanatumia kwa kunywa, kukoga na hayana tatizo. Ningeomba tungefikiria sisi wenyewe Zanzibar hata kama hatuna uwezo tukatafute nchi zenye uwezo ambazo zina umeme ule kama Dubai, Norway ina umeme wa upepo na nchi ambazo zinatumia umeme wa *solar*, tukakaa nazo tukawaleta hapa tukawaambia sisi tunahitaji umeme wetu labda *KW* 500 bei gani ita-*cost* kwenye masuala ya umeme wa upepo, wa jua na umeme wa maji.

Ningemshauri Waziri wa Fedha basi kwenye uzalishaji ule wao waje wa-*invest* ule mradi watutengezee halafu wakate mapato mle mle wachukue asilimia yao mpaka zile pesa wanazotudai zimalize na sisi umeme wetu tutakuwanao, kuliko kila siku ikawa umeme wetu hauna uhakika na kwa hali iliyopo ya uchumi sasa hivi na mambo yanavyojitokeza.

Mhe. Spika, kwa mfano itokezee umeme tumekuja kuambiwa tunadaiwa unakatwa Zanzibar imekufa, kwa sababu katika kitu muhimu katika *investment* moja ni umeme, tutapokuwa na umeme wetu *reserve* basi utatupeleka pazuri. Ningeomba sana kushauri kwa Mhe. Rais na serikali yake kwa ujumla, umeme tujitahidini sana tuwe na wetu japo wa kukopa watakata wenyewe waliotukopesha kidogo kidogo mpaka wamalize, lakini tuhakikishe tuna umeme wetu. Huo ni ushauri ambao nautoa na ninauomba.

Mhe. Spika, ahsante sana hotuba hii naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, ahsante nami sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kutujaalia uhai na uzima tukahudhuria katika kikao hiki kuendeleza shughuli zetu zilizotuleta hapa.

Mhe. Spika, nakushukuru pia kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali ambayo ni muhimu sana katika matumizi ya mwaka 2016/2017.

Pia, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake ambao wameandaa hotuba hii na leo wakaweza kutufikishia hapa na kuanza kujadili. Pia niitumie fursa hii kuwapa pole wananchi wenzangu kutoka

Pemba kwa misukosuko waliyoipata kwa wale ambao wameng'olewa vipando vyao, wamepigwa, kuharibiwa mali zao mbali mbali na hali mbaya ya kisiasa iliyoko kisiwani Pemba ya chuki. Vile vile, nimpe pole zaidi Mhe. Mwakilishi mwenzangu hapa Bi Khadija kwa kung'olewa mipunga yake.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwenye kuchangia katika kuimarisha uchumi katika hotuba hii.

Mhe. Spika, naomba kutokana na kwamba tuna lengo la kuufanya uchumi wetu ukue kuna sehemu ambayo mimi napendekeza tungeanza kuianzisha kupitia Wizara ya Afya kuanzisha Mfuko wa Bima ili Mfuko huu uendelee kuwepo na kuweza kunyanyua pato letu. Pia, pale ambapo tutakuwa na kasoro ya baadhi ya dawa ama huduma muhimu tutaweza kuutumia tukianzisha Mfuko huu wa Bima badala ya kutumia Mifuko inayotoka kwenye mashirika mengine ya binafsi.

Mhe. Spika, sasa niende katika Sekta ya Kilimo. Kama tunavyojua kwamba kilimo tunasema ni uti wa mgongo, lakini nafasi kubwa nayo iko katika kuongeza mapato yetu ya ndani kupitia sekta ya kilimo, pia tunatengeneza ajira kwa vijana wetu ambao kuwa ndio nguvu kazi kama inavyoeleza katika kauli mbiu ya mwenge 2016 kwamba vijana ndio nguvu kazi na tuwawezeshe.

Kwa hivyo, kupitia hapo sisi tunaweza kuongeza ajira lakini pia mapato yetu ya ndani, lakini kwa masharti ya kwamba tusilime vile tulivyozoea, tulime tutumie mbolea, na kwa maagizo ya wataalamu njaa itapotea.

Mhe. Spika, tutaweza kunyanyua uchumi wetu pia kwa kupunguza fedha yetu ambayo kuwa tunaitumia kwa kuagizia vyakula kutoka nje kama michele, watafiti wengi wameshafika hapa kuona kwamba ardhi tuliyonayo Zanzibar kwa kweli tunaweza kujitosheleza kwa chakula bado hatujaitumia, tukiitumia ipasavyo tutaweza kuongeza kipato chetu na kuidhibiti pesa yetu isiende nje kununua vyakula.

Mhe. Spika, pia, kupitia kilimo tutaweza kunyanyua kuanzia lile suala la kutumia viwanda. Viwanda leo tunaona hapa tunanunua *juice* kutoka nje, ni jambo la kushangaza mananasi tunayo, embe tunazo na matunda kadhaa wa kadhaa lakini tunatumia *juice* kama hizi kutoka nje. Tukitumia kilimo vizuri tutaweza kuanzisha viwanda vyetu hivi viweze kutoa ajira pia na mapato yetu na nimeliona hili kwa kuona kwamba vijana wetu tayari wengine wameshaanza kunyanyukia katika mambo ya kilimo, kama kule Pemba nimeyakuta mabonde ya Msaani na kwa hapa Unguja nimetembelea kwa sababu ni muumini wa

kilimo hata mabonde ya kule Mtule kwa Jimbo la Mhe. Jaku Hashim Ayoub Paje kule nimefika nimeona vijana namna wanavyowekeza katika mambo ya kilimo.

Kwa kweli wana hatua nzuri sana wanafaa kuelekezwa hawa na kuweza kupatiwa wataalamu wafanye kitu kwa uhakika yale masoko ambayo tunategemea kuyajenga basi yaweze kufanya kazi ili tuweze kuondoa ile kasoro ambayo ilijitokeza katika mazao ya kilimo kutoka asilimia 2.7 hadi kufikia angalau asilimia 3.5.

Mhe. Spika, niende katika sekta hii ya mifugo. Sekta hii vile vile ni sekta ambayo tukiitumia vizuri tutaweza kutengeneza pesa za ndani na hata pesa zetu za nje kwa kupitia wajasiriamali katika mifugo ya nyuki.

Mhe. Spika, nyuki wapo Zanzibar tena ni wengi na wana mali nzuri sana, tutaweza kupata asali kwa wingi, asali ambayo katika soko la dunia ina bei kubwa na ina ubora baadhi ya wafanyabiashara hawaridhiki kama hawajapata asali inatoka Zanzibar katika bidhaa zao wanazozalisha.

Mhe. Spika, suala hili liweze kupata nguvu ile sehemu ambayo iliwekwa katika shilingi milioni mia moja na arubaini, naomba na hawa wajasiriamali waangaliwe sana wafugaji wa nyuki wawezeshwe kwa kupatiwa mafunzo na vifaa vya kisasa katika kazi hiyo ya ufugaji wa nyuki.

Mhe. Spika, kama tutaziendeleza sekta hizi ndogo ndogo ndio zinazojaza kuifanya na hiyo sekta kubwa ikawa na nguvu sana kwani "haba na haba hujaza kibaba".

Mhe. Spika, katika hotuba yake Mhe. Waziri alionesha kupungua kwa mauzo ya bidhaa za nje ikiwemo karafuu na mwani. Kwa hivyo, nashauri kuongeza mikakati katika zao la mwani.

Mhe. Spika, zao la mwani toka lilipoanzishwa mwaka 1980 kule kisiwani Pemba katika fukwe za bahari ya Fundo, bado wananchi wanaendelea kupata manufaa mengi hasa wakiwemo kina mama. Kina mama sasa huwezi kumngojea kwamba lazima amsuburi baba anajinunulia nguo zake ananunua vyombo vyake vya harusi, na hata zamani walikuwa kina mama waliomo katika fukwe za bahari wanawasubiri akina baba warudi kwenye dago huko ndio waletewe fedha. Lakini hilo sasa hakuna, kina mama wanaweza kujijengea nyumba zao ambao wamo katika bahari kwa kupitia kilimo cha mwani. Lakini basi ina changamoto kubwa iliyoko mbele yao ikiwemo ni wakulima hawa

wanapunjwa katika bei, lakini na hawa wanunuzi nao hawana msimamo. Wakulima wanaweza wakakaa na bidhaa hii kwa wingi majumbani mwao hawajui hata wakati mwengine kukosa sehemu ya kuiweka ukakuta wanailengalenga tu katika sehemu mbali mbali.

Kwa hivyo, ni vyema mimi nashauri zao hili lirudi kama zamani ilivyokuwa Shirika la *ZSTC* kuendelea kulinunua wao. Kwa sababu itaonekana ule ubabaishaji kama karafuu ilivyodhitibitiwa na shirika hili na mwani nashauri kwamba lipelekwe hivyo hivyo.

Mhe. Spika, niende katika kuchangia maendeleo la kiuchumi Mhe. Waziri ameonesha ongezeko la wateja wapya waliounganishwa na *grid* ya umeme kutoka watu elfu kumi mia nne na arubaini na nne (10,444) mwaka 2014 mpaka elfu kumi na mbili mia tatu na sitini na sita (122,366) mwaka 2015. Ni sawa na wateja elfu moja na ishirini na sita iliongezeka kwa Zanzibar nzima. Lakini anasema kwamba kiwango hichi ni kidogo sana. Nasema ni kidogo kwa sababu wananchi wanaohitaji umeme huu ni wengi sana, lakini wanakumbwa na kadhia ya kwamba biashara ni ya Shirika la Umeme wananchi wanunue nguzo, mwananchi anunue waya kuna gharama ya kuchimba shimo mpaka kila kitu awalipie mafundi, wakati kazi ile ingefanywa na shirika wananchi wengi wangeweza kujitokeza na kuweza kuunganisha umeme wakaupata kuutumia kwa faida mbali mbali.

Kwa hivyo, mzigo huu naomba urudi kule kule kwa shirika ambao kuwa wao walibebe jukumu hilo bila ya kuona kwamba wao si jukumu lao, lakini ni jukumu lao na zaidi ukizingatia sasa hivi kunaundwa mfuko maalum wa miundombinu. Naomba hii fedha itumike katika kuwasogezea wananchi umeme, kuna vijiji ambavyo kuwa wanausikia tu umeme kama mita mia moja tu lakini wanashindwa, tuwaachie wananchi lile suala la *fitting* la nyumbani kwao lakini suala la kuvuta umeme libaki kwenye shirika.

Mhe. Spika, niendelee kuhusu kunakoongezeka mikopo, niishukuru serikali kupitia Wizara ya Elimu kwenye Bodi ya Mikopo kwamba mikopo imeongezeka kutoka 2,423 mwaka 2013/14 mpaka 3,429 mwaka 2014/15 sawa na asilimia 24.

Naipongeza sana serikali kupitia bodi hiyo lakini sasa kuna changamoto ambazo zipo hapa nina masikitiko makubwa sana Wizara ya Elimu kupitia Bodi ya Mikopo inapotoa mikopo kwa watu wanaosoma elimu ya juu utaona kwamba wanafunzi kwa mwaka mmoja kozi ya miaka mitatu mwaka mmoja unachukua gharama ya milioni tano. Lakini bodi inampa milioni moja laki tano

zikiwemo mambo ya usajili na baadhi ya huduma ndogo ndogo, hamna chakula, hamna malazi, hamna usafiri.

Mzigo huu unarudi kwa mzazi ni mzazi gani ambaye kuwa hana mradi wowote hana mkono mkubwa, ambapo pale ataweza kupata msaada akaweza kumsomesha mtoto huyo kwa mwaka shilingi milioni tano. Ongezeko hili alilioachiwa mtoto yule mwanafunzi yule sio yeye anaachiwa mzazi, watoto hawa ndio tunategemea ndio waje wakamate nafasi kama hizi, na kuwa ni wataalamu wa baadae lakini wanavunjika moyo.

Mhe. Spika, unafika pahali mwanafunzi anaingia chuoni mkopo hajapata, wazee wanaanza kuchanga changa aende akaanze kwa kuambiwa nendeni zinakuja, hatimaye akija anaanza masomo miezi sita au mitatu ndio mkopo unakuja, ukija anaoneshwa matokeo yake kwamba anasaidiwa milioni moja na laki tano hizi zilizobakia tutazitoa wapi. Naomba suala hili lifanyiwe marekebisho.

Mhe. Spika, niende katika masuala ya maji. Naipongeza sana serikali kwa kuongeza visima vingi vya maji ya safi na salama, lakini naona kwamba ongezeko hili la visima liende sambamba na kuviunganisha viweze kutumiwa kwa sababu ukipita huko mitaani utakuta visima vingi vimefunikwa vinasubiri kuunganishwa, sasa tutakuwa tunajinata kwamba tunaongeza visima vingi kutoka 28 mpaka 74 lakini hivi 46 havijaunganishwa, ile shida ya maji pale pale. Visima vile baadae vitakufa kwa sababu ninavyojua kwa kawaida ya kisima ukichimba ikiwa hakitumiki ile mirija inayoleta pale, nayo itakufa kama kisima umekichimba kinatumika kinaongezeka uzalishaji wake.

Kwa hivyo, hivi visima vinavyochimbwa viendelee kutumika, vifanye mikakati makusudi wa kuweza kutumika ili shida ya wananchi nayo iondokane tuwapunguzie mzigo akina mama ambao kuwa ndio hao tu wanaobeba kazi hiyo.

Mhe. Spika, niende katika mambo ya elimu tena hapo kwenye uanzishwaji wa skuli za maandalizi katika skuli za SMZ.

Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Elimu imekuwa ikipitia mkakati sana kuanzisha madarasa ya skuli za maandalizi katika skuli za serikali ni vyema. Lakini mwanzoni hapa nyuma ilipita kuwa kwa pale ambapo kuwa skuli za maandalizi ya jamii zipo basi hakuna sababu ya kuanzisha darasa jengine kule skuli za serikali. Lakini leo mambo yamegeuka, wananchi wamejenga skuli zile na gharama na serikali kutia mkono wao pale, majengo yapo na walimu wapo

tena wa kujitolea, hivi ninavyokwambia kuna walimu wanafika mwaka wa 12 wanajitolea kusomesha watoto wa chekechea, watoto wale na skuli zile ndio zinazotoa wanafunzi wakifika kule skuli za serikali ndio wanaotoka michipuo, mara nyingi sana na wanafunzi wale mara nyingi huwa wanafika mpaka Chuo kikuu kupitia pale pale skuli za jamii.

Kwa kweli kuziondoa skuli zile pale tukaweka skuli za serikali, kwa sababu wananchi kule wanajua hawalipi kwenye serikali zile skuli zetu za jamii zitakufa.

Kwa hivyo, sisi tunavyoumia kwa sababu tunazisimamia nikiwemo mimi kwa vile tutaona kwamba ile juhudi yetu haikuthaminiwa. Kwa hivyo, naiomba serikali kwamba pale ambapo bado skuli za jamii zipo ziendelee kutumika, na kule waendelee na skuli zao za msingi ili wale walimu waendelee kupata ajira na Wizara ya Elimu iwatizame kwa jicho la huruma kuwapatia ajira au angalau posho kwa kila mwezi ruzuku fulani itoke kwa kuelekeza walimu wale, pamoja na kwamba wao hawajali kwamba wanapata kiasi, wewe hata ukimpa shilingi laki moja kwa mwezi tayari au hamsini elfu au thamanini kwa mwezi tayari za uhakika maana leo wanasubiri wazee walipe ndio wapate. Sasa leo wazee wamepeleka watoto wao kwenye serikali hakuna anayelipa huku matokeo yake inaanza kufa siku hadi siku.

Mhe. Spika, narudia kwenye suala la umeme. Kama tunavyojua kwamba thamani ya mwanachi katika nchi yetu ni kubwa sana, na popote pale ana haki ya kuthaminiwa na kupewa huduma mbali mbali. Katika jimbo langu muna vijiji toka ilipoanzishwa hii serikali ya Mapinduzi haijawahi kupata kitu umeme wala ile barabara, kwa mfano kijiji cha Kwale Mpona. Kijiji hiki kipo na kina wakaazi kule wanafanya shughuli mbali mbali lakini huduma hii ya umeme bado wanaiona kama ni ndoto na huduma ya barabara.

Naiomba serikali kupitia taasisi hizi mbili za barabara zitumike kama ule mfuko wa barabara ufanye japo kwa njia ya fusi kama zilivyofanywa nyengine kwa kuanzia pale barabara kuu na kuelekea kule kijijini Kwale. Lakini pia Shirika la Umeme nao kupitia mfuko huu huu wa miundombinu utumike ili nao kule wananchi hawa wafaidike na suala la umeme; kuna misikiti, kuna majumba ambayo yanahitaji umeme. Sambamba na hilo kijiji cha Kwale Mpona pia vile vile umeme haujafika, misikiti inakaa giza na umeme uko karibu lakini ndio yale watafute nguzo watafute waya kitu ambacho Shirika la Umeme likifanya hivyo tayari linajiongezea mapato baada ya umeme ule kwenda tu kutembea kwenye mawaya bila ya matumizi yoyote. Hivyo, Mhe. Spika, naomba serikali iliangalie suala hili ambalo kwa wananchi ni kero.

Mhe. Spika, sambamba na kilio cha wafanyakazi katika ukurasa wa 23 ibara ya 55 ya kitabu cha Bajeti. Mhe. Spika, wafanyakazi wanatajwa hapa kuondolewa upungufu wa mikato kwenye mishahara yao ya *income tax* kuwasaidia katika kipato chao na kuongeza mishahara yao itaongezwa. Lakini bado kuna kilio cha wafanyakazi wanaotoka kama vile Wete kwenda Chake na Chake kwenda Mkoani, Wete kwenda Konde wafanyakazi hawa wanatoa pesa zao kwa ajili ya kwenda kazini, kama unajua au kama hujui Mhe. Spika, ulizia nauli za Pemba ni ngumu sana, mfanyakazi ikiwa atatoa pesa kila siku kwenda kazini ina maana atatumia karibu shilingi elfu tano. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Fedha iandae usafiri makusudi, na utafutwe wizara gani itasimamia pengine Wizara ya Utumishi ili huduma hii iwepo ya wafanyakazi wanaotoka Wete kwenda Chake na Chake kwenda Mkoani katika miji hii ili kuwaondoshea mzigo huu waweze kufika kwa wakati na waondoke kwa wakati.

Leo mfanyakazi wa Chake anakwenda Wete ama anafika saa nne na saa nane hayupo tena ofisini si hiari yake anataka afanye kazi lakini anasubiri apate *lift*. Naiomba sana serikali iliangalie hili kwani huduma kama hii hapa inapatikana, wenzetu wanapata gari wanapelekwa majumbani kwenda kazini, naomba sana serikali kwa huruma iliangalie suala hili.

Mhe. Spika, mwisho mimi niseme kwamba naiunga mkono hotuba hii ya bajeti asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Mhe. Spika, awali ya yote napenda niungane nanyi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote, tumtakie kheri Mtume wetu Muhammad (*SAW*), tuwatakie kheri ndugu zetu, wazee wetu waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mhe. Spika, na mimi napenda kumpongeza sana Rais wetu Mhe. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake na uimara wake katika kipindi chote alichoongoza cha serikali ya pamoja na mpaka leo akawa yuko imara katika kuliongoza Taifa hili la Zanzibar.

Mhe. Spika, na mimi naweza kusema kwamba nimpongeze Mhe. Khalid Waziri wetu wa Fedha kwa mambo matano. Kwanza nimpongeze sana juzi alipoingia kwa mbwembwe za aina yake kwa kujiamini sana na vile ndivyo inavyotakiwa.

Pili, nimshukuru kwa sababu alimuelezea sana uimara wake wa Mhe. Rais wetu Ali Mohamed Shein katika kuliongoza taifa hili.

Tatu nimshukuru kwamba hakuisahau familia yake, wengine wanasahau familia zao kwa hivyo nampongeza sana.

Uwasilishaji wake wa bajeti ni kivutio kikubwa alichokifanya hapa na jinsi bajeti yetu alivyoifafanua na upangaji wake. Hilo tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Na mimi basi niwashukuru wazee wangu mama yangu bi Fatma Suleiman, Mjomba wangu Dkt Nassor, Mke wangu bi Khadija Masoud watoto wangu wapendwa na ndugu zangu wote kwa jumla na wananchi wa Chake Chake ambao wamenichagua kwa kura nyingi za kishindo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kupata nafasi ya kuchangia bajeti yetu nzuri iliyopangika, na hii ndiyo bajeti ya Zanzibar. Hapa ninakubaliana nayo lakini pia ninaanza kwa kumshukuru Mhe. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya kule Tanzania Bara na kuirudishia heshima serikali yake. (*Makofi*)

Sababu Mhe. Spika, serikali yetu hasa Tanzania labda ilianza kupoteza hadhi kidogo kwa watu wengine walikuwa wamejisahau. Lakini Mhe. Magufuli ameirudisha heshima hiyo kwenye nchi ya Tanzania. Pia, nimshukuru na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa uimara yake. Ninawashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi waliochaguliwa kwa kishindo Mwenyezi Mungu awaongeze katika kazi zenu na murudi tena miaka mengine tukijaaliwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi katika bajeti yetu jambo la kwanza lililonifurahisha na kuniweka katika nyoyo safi ni kumaliza madeni ya viinua mgongo vile vilivyokuwa vinakuwa kama kero za wananchi kwa jumla. Mhe. Spika, hapa ni jambo muhimu sana tumelifanya. Pia tutapata baraka kwa Mwenyezi Mungu kwa kuondoa hizo kero za wananchi. Mhe. Spika, hilo lilikuwa ni la kwanza.(*Makofi*)

La pili, Mhe. Spika, nipongeze kwamba zile kelele za wafanyabiashara kuhusu madai ya magari yanayokwenda Tanzania Bara. Mhe. Spika, tatizo hilo umelimaliza. Na wananchi kwa kweli wanalipendelea sana. Pia yale mapato yetu yaliyokuwa yakihangaika-hangaika, sasa yatakuwa tumeyakusanya sisi wenyewe kwa kipato chetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mheshimiwa hilo ninakupongeza sana katika kazi zako na hata hii habari ya magari ambayo yanatembea na alama za "T". Mhe. Spika, yanatuumisha kichwa na imekuwa ni matatizo kidogo, lakini tatizo hili nalo

umeshaliweka pazuri kwamba kuanzia tarehe mosi magari haya yatatakiwa kutembea na namba za Zanzibar. Mhe. Spika, hilo ninalishukuru sana kwenye bajeti yetu.

Mhe. Spika, lakini ninataka niseme kwamba suala la serikali. Naomba suala hili tulitazame kwa kina. Serikali kama serikali nayo ina miradi yake. Inafanya miradi ya kujiendesha kibiashara au ilikuwepo hapo zamani. Lakini Mhe. Spika, biashara hizi zinazotengenezwa au zinazofanywa na serikali, zinakuwa na matatizo na inakuwa watu wanazicheka wanazifahamu kwamba haziendi. Maana yake imekuwa sisi kazi yetu ni kwamba kazi ya serikali yoyote haiendi, inayoweza kuchukuliwa na mtu wa kawaida, eti serikali ikashindwa.

Mhe. Spika, watu hawa ambao wanatupotezea mapato, watu hawa ambao wanayauwa mashirika ya umma. Halafu watu hawa wanabadilishiwa *section* nyengine kwenda kuuwa mashirika mengine. Mhe. Spika, hawa walipoteza mapato ya serikali na kodi za wananchi. Mhe. Spika, watu hawa washughulikiwe. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi sitoona vizuri nikasikia meli yetu ya Mapinduzi mpya (Mapinduzi 2). Meli yetu ambayo tumeitafuta kwa njia zozote zile ambazo zimepatikana, halafu tukaitengeneza, halafu tukampe mtu atumie. Sisi serikali tumeshindwa. Inawezekanaje suala kama hili. Mhe. Spika, watu kama hawa kama watu ambao watakuwa na uongozi wa meli hii, baada ya mwaka mmoja tukaona mapato yao na mambo yao hayaendi na tukauliza matatizo haya ikawa hamna. Mhe. Spika, watu hawa hawafai watumbuliwe majipu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ni lazima meli kama ile mpya ambayo ina uwezo wa kutumika kiilivyo. Kwa nini yafikie matatizo ya kusema meli ile tuanze kuikodisha au kuwapa watu. Hilo Mhe. Spika, kwa hali yoyote kwamba ulitazame kwa kipekee kwamba mashirika yetu ambayo ni ya kiserikali kwa nini yanakuwa yanakufa ovyo ovyo. Hapa lazima Mhe. Spika, ni suala ambalo la kuangalia sana.

Mhe. Spika, chengine ni kwamba sambamba na hotuba ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, aliyotungulia Baraza letu hapa. Mhe. Spika, kwa aliyeifahamu hotuba ile na bajeti hii inavyoendana, hatuwezi kushindwa hata siku moja. Hili ni suala kwa kasi tunayokwenda na kwa Mawaziri tulionao na Manaibu pamoja na Wawakilishi wote. Ninataka niseme kwamba hii bajeti ni ya Wizara ya Fedha na Mipango, lakini ni bajeti ya wananchi wote wakiwa Wawakilishi sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ni lazima tusimame kidedea mpaka mambo yetu tuhakikisha kama tulivyopanga yameendana na hali hiyo. Lakini Mhe. Spika, nataka niseme kwamba kuna sehemu nyingi ambazo mapato yetu yanapotea. Ukiangalia sehemu ambazo zina *parking* za magari, mapato madogo madogo ya shilingi ya mia tano zinapotea-potea kiana. Mhe. Spika, lazima tutafute mitambo ambayo inakuwa haiwezi lobolobo za kawaida Mitambo ambayo akiingia mtu pale inakatwa kutokana na mitambo. Siyo karatasi za mikononi.

Mhe. Spika, ile inapoteza mapato sana. Na shilingi mia tano Mhe. Spika, ni pesa nyingi sana kwa siku ambazo tunazihitaji kuendeleza mambo yetu. Hivyo Mhe. Spika, ni masuala ya maeneo mengi tunatumia *analogue* hii ya mikono mikono ambayo kwa kweli pesa zetu nyingi zinapotea-potea. Nyengine zinaingia kwa wasiokuwa waaminifu. Hivyo Mhe. Spika, ningeomba kwamba hali hii muitazame kwa kina.

Jengine Mhe. Spika, ninataka niseme kwamba kuhusu Uwanja wetu wa Ndege wa *Terminal 11*. Mhe. Spika, uwanja huu kutokana na ratiba iliyokuwemo ulikuwa mwaka 2013 ulikuwa umeshakabidhiwa kwa serikali. Uwanja huu ulikuwa tayari ni kioo cha Zanzibar na uwanja huu tayari ulikuwa ufanye kazi kwa kuongeza mapato mengi sana. Lakini Mhe. Spika, uwanja huu kwa sasa hivi imekuwa ni wimbo wa taifa. Imefika mwaka 2015, 2016 na bado unahitaji miaka miwili tena kuja kukamilika kwa uwanja. Wakati uwanja huu kunawezekana hata ikifika mwaka 2020 hauna hadhi tena ya kuwa tunataka tubadilishe uwanja mwengine.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri sana tutumie nguvu zetu kama tulivyotumia meli ya Mapinduzi 2. Katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu, hii *Terminal 11* ifanye kazi. Angalau tu turudishe ile hadhi yetu na mapato yetu yaliyopotea kwa muda mrefu. *Otherwise* kila siku pesa hizi zitaongezeka na mwisho wake ule uwanja hautotufaa kitu. Hivyo Mhe. Spika, mimi ningeshauri sana kwamba tutumie nguvu za ziada kuumaliza uwanja huu haraka iwezekanavyo ili mapato yetu yaweze kuendelea. Kwa hivyo ninashauri hilo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninataka niseme kwamba na watu ambao tunatumia mabarabara. Serikali imejitahidi sana kujenga barabara nyingi, maeneo ya Wete, Konde huko na maeneo mengine. Na sasa hivi kama kuna mabarabara hii ambayo ipo ya Fuoni wakati wowote itaanza kumalizwa na maeneo mengi. Lakini Mhe. Spika, kitu ambacho kinakuwa kigumu katika kujenga barabara zetu ni kwamba wakati wa kutaka kujenga barabara, huwa Mheshimiwa tunakaa kama tunashtuka. Sasa hivi hatujakuwa na plan. Tuna mabarabara mengi tutafumua kati kati maeneo. Kwa nini serikali haioni kwamba yangeanza kuyapima

maeneo ili wananchi wasiweze kuanza kuingia katika maeneo na kuanza kuja kulipa mapesa mengi yasiyokuwa na maana na bado malalamiko yanakuwa yanakuwa hayatoshi.

Sasa tungejipanga mapema tukaipiga ramani ya nchi yetu, tukapasua njia kabisa. Tukaitazama barabara hii usiiguse na wakati huo huo matangazo yawepo. Maana yake hapa Mhe. Spika, tunaacha watu tunawaona wanajenga kwenye barabara tunanyima kimya mpaka ukifika muda, tukaja kuitia serikali kwenye lawama. Haiwezekani Mhe. Spika, ni lazima tuweze kuwapenda wananchi wetu na kuwaeleza bwana! hapa haparuhusiwi mapema kabla hajaingia hasara. Hilo Mhe. Spika, ilikuwa na mimi nilichangie tuone kwamba tusirudie kutia hasara zisizokuwa na maana serikali yetu.

Mhe. Spika, na jengine nilikuwa naona kwamba ukiangalia sana kwenye kitabu sikuliona. Lakini ningefurahi sana ningeona kwamba kuna Shirika la Ndege la Zanzibar. Humu sikuiona. Lakini ilikuwa Mhe. Spika, umeshafika wakati kwa sasa hivi kuunda Shirika letu la Ndege la Zanzibar. Mhe. Spika, ipo haja kubwa sana sasa hivi ya kupata shirika letu ambalo litakuwa na mapato na watu watabalishana; wenzetu wakenda Dubai na sisi tunakwenda China, tunakwenda wapi. Na sisi Shirika la Zanzibar karafuu yetu itembee kwenye ndege Mhe. Spika. Mhe. Spika, ningeomba sana bajeti zijazo tukijaaliwa tufanye Shirika letu la Ndege la Zanzibar liweze kupatikana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, suala jengine nilikuwa ninasemea kwamba ipo haja lazima tuangalie. Kuna hasara lazima ziwepo katika mambo haya. Mhe. Spika, ilikuwa kuna haja ya ndege ya serikali. Ilikuwa tutafute ndege yetu ya serikali ya Rais ambayo itakuwa inahudumikia serikali, inamuhudumia na Rais. Sio Mhe. Spika, kila siku kutafuta ndege ambazo tuna-*risk*. Mhe. Spika, ndege nyengine yanakuwa ya ku-*risk*. Viongozi wetu tunawa-*risk* katika ndege nyengine. Lazima Mhe. Spika, ilikuwa katika hali isiyokuwa ya kawaida tujibane matumizi na ndiyo maisha, tutafute ndege yetu ya serikali. Hilo Mhe. Spika, nilikuwa naomba hili nalo lifanyiwe kazi kwenye kipindi kitakachokuja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Dkt. Shein kwa hatua aliyoifanya ya kupandisha mshahara kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, hii ni hatua kubwa sana. Haidhuru kwamba ule muda haujafika, ninajua tunajipanga. Lakini hii dhana ambayo tulikuwa hatuwezi, sasa tumeweza. Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa ahadi uliyokwishakuitoa panapo mwezi Aprili Mwenyezi Mungu akitujaalia mwaka 2017 watu wataanza kutumia shilingi laki tatu kwa mshahara wa chini. Ninamshukuru Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake huo.(*Makofi*)

Pia, nimpongeze tena Mhe. Dkt. Shein kwa gharamia wazee wale ambao wanafika miaka sabini. Rais wa Zanzibar anayefika miaka sabini ameanza au anaendelea kuwapa fidia fidia ndogo ndogo zitawasaidia na wakati wowote anaweza akasaidia kupandisha. Kwa hivyo hilo kidogo nilikuwa ninamshukuru sana Rais wetu kwa kujali maelezo kama hayo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba bajeti hii pamoja na mazongezonge yote, lakini wananchi hasa vijana wamekuwa na ari kubwa sana ya kwamba lazima wanataka waajiriwe ndani ya serikali. Mhe. Spika, hili ni la kweli. Wana haki na wao wa kuajiriwa lakini kwa kweli lazima tutizame kwamba vijana wote kuajiriwa ndani ya serikali, hili suala Mhe. Spika, linakuwa zito kweli kweli.

Mimi ninajua uajiri wa serikali ni uajiri mzuri sana. Na anayekuwa anayeajiriwa na serikali, halafu anadharau basi huyo atakuwa kapoteza dira yake. Kwa sababu Mhe. Spika, kuajiriwa ndani ya serikali. Kwanza kunakupa heshima, kunakupa uhakika wa maisha yako, ukenda kazini, usiende, ukiumwa wewe mshahara wako upo. Unapata kiinua chako cha mgongo cha uhakika, unatembea na kupata jamaa zako na marafiki zako katika maeneo mbali mbali. Unapata kujulikana unakopa kwa ajili ya serikali. Mhe. Spika, unajulikana na una hakika kama kila kipindi mshahara wako utapanda, unapata likizo za kupumzika kwa kupangwa.

Mhe. Spika, mtu huyu wa serikali, halafu anafika kuidharau serikali yetu. Sijui ni mtu wa aina gani na kama yeye ameona kwamba kwa kweli anayarudisha nyuma maendeleo yetu, bora angetuachia, yeye akenda kwenye kazi za binafsi, sisi tukaendelea na serikali yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini ninataka niseme kwamba kwenye mapato. Mhe. Spika, yanaanza mapato ya serikali juu, yanakuja mapato ya ndani, lakini yanakuja mapato ya mtu kwa mtu. Mhe. Spika, katika jinsi ya mambo wananchi wetu mapato yao yanashuka, kuna matatizo mengi utakuta kwamba tunashindwa kumudu maisha yetu. Mhe. Spika, kwanza ninataka niseme kwa upande wetu tumeshikwa na maradhi makubwa sana; maradhi ya sukari, kansa, moyo, *pressure*, ukimwi na maradhi mengine yametukabili sana. Hasa kwenye Kisiwa cha Pemba Mhe. Spika, hizo kansa zimezidi.

Mhe. Spika, ninataka niseme gharama kubwa. Sote Wawakilishi na watu wengine tunagharami kwenda Dar es Salaam mtu kwenda kupimwa, mtu kwenda kufanya matatizo yake. Kila siku ndege hizo, ndege moja ni shilingi laki mbili na nusu. Gharama za kule ni nyingi. Mimi ningeshauri serikali

kupunguza mambo haya, tungeletewa madaktari specialists wa maradhi haya wakaweza kukaa maeneo wakasaidia hii hali. (*Makofi*)

Mhe. Spika, wakapunguza ukali wa maisha. Kwa kweli maradhi yametukabili sana ingawa mpaka hatujajua chanzo. Tunakisia tu kwamba labda ni vyakula na kitu gani. Lakini pia mabadiliko ya nchi. Matibabu Mhe. Spika, ni muhimu. Tuna maradhi sana ya figo ya nini. Mhe. Spika, tungepatiwa wataalamu wa hali ya juu na vifaa vyake. Wakakaa pale Pemba kama timu, itatusaidia maradhi. Kila siku karibu tutajaa Dar es Salaam kwa kuzikwa kule, tunazikwa Dar es Salaam siku zote. (*Makofi*)

Watu wote wanaokaa Pemba wanaondoka kwa kwenda kufa Dar es Salaam kwa maradhi haya. Mhe. Spika, imekuwa taabu kweli kweli. Ninaiomba serikali Mhe. Spika, iweze kutusaidia suala hili kwa kupitia kule katika Kisiwa cha Pemba ambacho ni mbali na maeneo ya matibabu. Hilo Mhe. Spika, pia ningesema.

Mhe. Spika, ninataka niseme sasa hivi tunajenga skuli nyingi, tunajenga mambo mengi lakini hazikidhi viwango. Mhe. Spika, skuli zote zinazojengwa hazina viwanja vya michezo. Almuradi mtoto hana taaluma yoyote, zaidi ya kwenda kusoma ubaoni na akatoka pale. Tungefikiria sana tunapojenga maskuli basi tugharimike, lakini tupate na kiwanja cha michezo cha watoto. Hivi vinasaidia sana Mhe. Spika, ili kupunguza matatizo ambayo watoto wasipoteepotee mitaani. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini ninataka niseme chengine. Serikali inajitahidi sana kwa kila hali. Imefungua sijui dawati la nini, mambo mengi. Mhe. Spika, unyanyasaji wa kijinsia kwa sasa hivi umekithiri, unaongezeka pamoja na mambo yote yaliyofanyika. Mhe. Spika, kuna unyanyasaji huu mwengine wa kindoa.

Mhe. Spika, huu ningeiomba serikali ikaitupia macho tukajijua tufanye nini. Mhe. Spika, mume anakwenda kuposa katika binti mtoto mdogo sana anamchukua anakaa naye anazalisha mtoto wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne, wa tano. Katika kipindi chote hicho Mhe. Spika, bwana huyu anamwambia huyu mke wake mama stahili najenga, tukimaliza utastarehe unalala chini lakini utalala kwenye kitanda kizuri. Lakini pia nafanya mpango wa kukopa ili tupate gari ya kuendesha. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mama huyu wakati ambapo umeshafikia kwenye umri wa miaka kuanza thalathini kwenda mbele. Haya maeneo mengine yale ya hoteli za mtoto yameshalala, yameshakuwa taaban, sura zake zishachafuka. Mama huyu watoto

wamemkamata. Yule bwana anaamua kwenda kutafuta mtoto mdogo mbichi akamtia kwenye nyumba na akampa gari. Yule mama akamtoa nje kwa mateke akamtupa na watoto wake. Mhe. Spika, hili liangaliwe kwa nguvu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hali hii hiyo bajeti nayo inakuwa ngumu kuifanya. Matatizo inapata serikali. Kila siku tunachukua watoto wa mitaani na watoto wengine katika hali hii. Lakini Mhe. Spika, ninataka niseme kwamba sasa hivi tutizame kwa jicho la huruma sana. Kama tunapiga makelele basi tufanye. Wanawake na watoto Mhe. Spika, kama baba anatafanya vituko hivyo, atoke yeye kwenye nyumba kwa niaba ya serikali na kama ni gari aachiwe mama. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tulitazame kwa hima kwa sababu matatizo haya ninakwambia kweli yametukabili sana. Tunatazama tu yale matatizo ya nje nje lakini na haya ya ndani Mhe. Spika, watoto wengi wanapotea. Mimi ninaishauri serikali kwamba iweke sheria maalum, baada ya zile ndoa za Kiislamu ikishakufungwa, anaambiwa bwana! ukimuacha mama huyu katika mazingira haya basi unatoka wewe kwenye nyumba, unamuacha yeye na watoto. Tena wewe una hiyari yako, ukasema asiolewe aolewe, hiyo tena ni mambo mengine lakini nyumba unamuachia na gari unamuachia. Ili na yeye mama ajifundishe hata hajui ataendesha Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pamoja na maongezi ambayo ninayosema, sasa twende kwenye Shirika letu la Umeme. Mhe. Spika, Shirika la Umeme linavyofahamu hasa kule katika Kisiwa cha Pemba ambacho ninaweza kwamba *megawatts* zetu zinazotumia umeme ule, ni kama *megawatts 35.* Wakati ninavyofahamu mpaka hivi sasa Pemba labda ina uwezo wa kutumia *megawatts 10* kama inaweza. Kwa hivyo tuna *extra* ya megawatts 25 ambazo zimekaa.

Mhe. Spika, ule umeme uliokuja kule Pemba ni umeme wa wananchi wa Pemba hauna haja ya kukaa mule kwenye waya. Ule umeme Mhe. Spika, mimi ningeishauri serikali ikasambaza umeme kwa watu wote bure, halafu mapato yake yakakushanya kupitia kwenye mita zake. Angalau kuna watu kwa sababu uwezo wa kuvuta umeme mamilioni hawana, lakini kila siku wana uwezo wa kutumbikiza ile mita yao wakaweza kutumia umeme na wewe ukapata mapato. (*Makofi*)

Mhe. Spika, umeme huu unakaa kwenye waya hautumiki na watu wanahitaji umeme. Na sisi tumeshatoa ilani tutaleta umeme na maji. Basi tupelekeni halafu tutajua vya ku-*charge* kwa utaratibu. Mimi nina uhakika wananchi kudaiwa hawaoni tatizo, lakini tatizo linakuja na ukwasi, linakuja katika kutia

nguzo na kutia waya. Mhe.Spika, ningeshauri kwamba umeme usambazwe bure ili wananchi wapate umeme, baadae tutalipa kwa muda wa utaratibu ambao upo.

Mhe.Spika, chengine ninataka niseme suala la kilimo. Mhe. Spika, tunasema kuwa kilimo ni uti wa mgongo. Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya kazi kubwa sana katika kuirudisha mikarafuu. Mikarafuu Mhe. Spika, baada ya miaka kumi hizo tani zitaongezeka sijui sina takwimu, lakini zitaongezeka nyingi sana. Ingawa kwa wakati mwengine labda utaona muda bado ameshafanya kazi kubwa sana ya kushajihisha mikarafuu.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri kitu kimoja ambacho kipo ni kwamba kilimo cha mpunga. Niliwahi kumsikia Waziri alisema katika kipindi ambacho baada ya mwaka mmoja au miaka miwili huenda tukajitosheleza kwa chakula. Lakini ninataka nitoe rai na mimi.

Mhe. Spika, sasa hivi mashamba ya mpunga yote yanayojulikana ni mashamba ya mpunga trekta lisichague lilime bure, mwahala mote ili kuwatia hamasa wale ambao wanalima, asipolima hapokonywi shamba, lakini mtu mwengine atakwenda kuburuga na kumalizia mambo yake na kwa mwaka ule kipato cha mpunga kitaongezeka, na uzalishaji utaongezeka. Kwa hivyo, ningeshauri mheshimiwa, maeneo yanayokaa wazi yasikubalike kukaa wazi kwa sababu ardhi ni mali ya serikali, hatumpokonyi mtu kwamba ni chake, lakini kama huna haja ya kulima mwaka huu basi sisi tutalima na tukishalima tutachukua magunia yetu tunakuachia pale, una hiyari yako ukilima mwakani sawa hukulima tutakuja tena.

Mheshimiwa tungefanya hivi maeneo mengi yako wazi tuna vilimo vingi vya mbolea. Lakini mtu hata ukienda kumuambia kwamba nataka nilime hapa atakuambia usilime, sasa hii serikali itowe kauli ama alime yeye, sio aweke shamba yeye akakae Arabuni mashamba yapo tutayalima. Serikali inajua kwamba ardhi ya Zanzibar ni ndogo sana, ni lazima tuhakikishe kwamba kilimo hicho hicho kidogo.

Mhe. Spika, serikali sasa hivi inafurahi kwa sababu angalia matunda yetu yaliopo katika masoko yetu yanazaliwa hapa Zanzibar, ni kukubali kwa watu kusaidia kulima. Kwa hivyo, tungeshauri sana, hebu angalia ndizi zinazokuja kutoka Pemba Mhe. Spika, huamini kama ndizi hizi zinatoka Pemba, Pemba

ndogo lakini ndizi meli kwa meli siku zote na bado nafasi zipo, tuna uwezo wa kujilisha wenyewe bila ya kuagiza vyakula vinavyotuletea kansa na matatizo mengine.

Mhe. Spika, jengine nataka sasa nisemee Jimbo langu la Chake Chake. Mhe. Spika, mji wa Chake Chake ni mji nambari mbili ukiacha Mjini Magharibi, kule ni mji nambari mbili. Mhe. Spika, kama umeshakwenda au hujafika basi nakukaribisha sana na Waheshimiwa Wajumbe wote nawakaribisha sana. Chake Chake ina maghorofa sasa hivi na mahoteli ya hali ya juu, ni mahoteli ambayo yanakidhi hata kufanya mikutano ya kimataifa, mheshimiwa mahoteli tunayo tena mazuri sana.

Mhe. Spika, ule mji umekaa kimji mji, ni mji kwa majengo mheshimiwa ukifika asubuhi mpaka milango ya saa 8:00 mji ule una tabu kuliko Kariakoo, Mhe. Spika, mji hauna standi, hauna maegesho, wala hauna maeneo mji umeshajibana umemalizika.

Mhe. Spika, mimi ningeishauri serikali ili kuhakikisha inaipa hadhi ya mji, basi ni kuhakikisha kuna stendi ya mabasi ambayo yanatoka Mkoani, Wete, Micheweni na kila pahala, hawakikishe katika kipindi hiki cha mwaka mmoja au miwili stendi inatengenezwa haraka iwezekanavyo. Mheshimiwa mji wa Chake Chake uko katika hali mbaya kwa sababu haina nafasi hata ya kupita mtu, ajali ni nyingi, magari yote yanapakia watu njiani. Kwa hivyo, ningeshauri wahusika wakafanya kila jitihada zao, wakaondoa kila lililopo, kama tulivyonunua meli basi wakahakikisha na stendi ya Chake Chake basi inapatikana. Maana yake stendi ya Chake Chake ndio stendi ya Pemba, gari za kila pahali zipo pale.

Mhe. Spika, nataka niwape sifa ya Chake Chake. Chake Chake hasa nataka niwaambie kwamba kila mmoja *drip* anakuja kuchukulia Chake Chake, pale ndio *town*. Kwa hivyo, lazima ule mji tuuhakikishie kwamba una usafi. Lakini nimemsikia waziri wangu hapa akisema miji hasa wa Chake Chake ukiacha huu, hata punda na ng'ombe hawataonekana tena.

Mhe. Spika: Dakika tano zimebaki Mhe. Mjumbe.
Mhe. Suleiman Sarahan Said: Naam Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Dakika tano unazo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Spika. Nikiongeza utanipa zile dakika zako za ziada, lakini tuendelee kwanza. Ahsante nitaheshimu

mheshimiwa. Sasa ninachokisema Mhe. Spika, ni kweli na magari ya ng'ombe kweli yapo, lakini ningeshauri zaidi ule mji wa Chake Chake kwa hadhi yake ukatizamwa kihadhi yake, wizara zote ziko pale, mabenki yote yako pale, hospitali kubwa ya Chake Chake iko pale. Mhe. Spika, ukienda kutizama hospitali ya Chake Chake utalia na utatoka machozi ya damu hata feni hatuna.

Juzi nakwenda kukagua namkuta mtoto wa miaka 13 au 14 mwanamke, kafungwa hapa anapepewa kwa karatasi feni hakuna. Nakwenda *theatre* lile la kutoa ma- *oxygen* na kila kitu, tena naingia mule muna operesheni lilipasuka watu wanaona mama ana maliza maliza kumbe bwana *oxygen* inavuja mapira yamepasuka. Mhe. Spika, matatizo madogo madogo lazima haya yamalizwe. Hospitali ya Chake Chake iwekwe kiwango, kwa sababu ina zaidi ya watu laki moja wanaotoka Micheweni na kwengineko wote wanakuja pale, sasa hii hali Mhe. Spika, inatisha katika Hospitali ya Chake Chake, inatakiwa ipate huduma za ziada, madaktari wa ziada. Kwa hivyo, mheshimiwa ningesema lakini kwa sababu sipendelei sana kwamba najipendelea mwenyewe, lakini ule ni mji ni lazima tukubaliane nao.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza, ikibakia dakika moja niambie ili nipate kuunga mkono. Mhe. Spika, ni kwamba wizara yetu ya utalii ina jengo lile la Uwanja wa Gombani, jengo limejengwa kwa gharama kubwa liko pale, lakini ningeshauri lile jengo kwa sababu hata huo mpira wenyewe watu wanaingia na ina milango mingi huku nyuma na ubavuni, ningeshauri ikakaguliwa na ikafanywa hata ma-*store* tukapata pesa kwa wafanyabiashara angalau kwa sababu ule uwanja umekaa na tutautupa kwa hali hiyo.

Pia, Mhe. Spika, nataka niseme kwamba kwa upeo wangu hawa watu ambao wanaoshughulika na utalii hasa sehemu hizi za Mji Mkongwe. Mhe Spika, kule Pemba kuna matukio mengi ya mambo ya utalii, kuna Mkamandume hajulikani, kuna Kigomasha hakujulikani, kuna wale Masheikh waliodidimia hawajulikani, kuna pale Ngomekongwe iko pale Hospitali haijulikani. Mhe. Spika, hili suala ningewaomba hawa wahusika wangekwenda kutizama wakawapeleka watalii kuongeza angalau miradi hiyo.

Mhe. Spika, sitaki nichukuwe muda wako ninalosema ni kwamba nampongeza sana Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake, nampongeza Dkt. Khalid Salum Mohamed kwa kutuletea bajeti safi. Lakini pia naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia kwa bajeti hii ya serikali Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahani Said, sasa namwita Mhe. Rashid Makame Shamsi, atafuatiwa na Mhe. Shamata Shaame Khamis na Mhe. Abdalla Maulid Diwani ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuichangia bajeti hii ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nitangulize kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha na Alaasiri hii kuwa katika hali ya uzima na kuweza kuja kuichangia bajeti hii.

Vile vile, nichukuwe nafasi hii adhimu kuweza kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni, kwa kunipa niridhaa ya kuingia katika chombo hiki katika kuja kuwasemea na kuweza kuleta michango yangu kwa serikali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Magomeni na Zanzibar kwa jumla.

Pia, nichukuwe fursa hii ya kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuchaguliwa kwa asilimia kubwa na kuweza kuliongoza taifa letu. Vile vile nichukuwe fursa ya kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais kwa kuweza kuteuliwa na Mhe. Rais na vile vile kwa kuchaguliwa na wananchi wa jimbo lake tukufu la Mahonda. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia nichukuwe fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa na kuwa Spika wetu wa Baraza hili la Wawakilishi. Pia nichukuwe fursa ya kumpongeza kwa kuchaguliwa Katibu wetu mpya wa Baraza hili na Wajumbe kwa ujumla wa Baraza la Wawakilishi kwa kuchaguliwa katika majimbo yao na wale ambao wameteuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar, niwapongeze sana.

Mhe. Spika, sasa nielekee katika kupeleka michango yangu katika bajeti hii. Mhe. Spika, bajeti iliyowasilishwa ni bajeti ambayo naweza kusema kweli imewalenga wananchi wa Zanzibar ambao wengi hali yao ya uchumi ni duni. Bajeti hii kwa uzuri wake haikuweza kuongeza kodi katika nyanja mbali mbali, lakini vile vile ni bajeti ambayo imewatazama wananchi na wafanyakazi wa kiwango cha chini, ni bajeti ambayo imewatazama wazee wetu ambao wana hali duni na ambao wametimiza miaka ya 70 na kuendelea. Kwa ufupi vile vile imetazama miradi mbali mbali ambayo italeta tija kwa wananchi. Bajeti hii kwa kweli imewajali wananchi wa Zanzibar katika kuendeleza maendeleo mazima na mustakabali wa maisha yao.

Mhe. Spika, mimi kwa kweli katika bajeti hii nianze katika suala zima la pencheni, pencheni ambayo imetajwa humu kwa kweli kwa miaka mingi mimi sijawahi kuisikia, kwamba serikali kuweza kumudu kutoa pencheni kwa wazee waliotimiza miaka 70 na kuendelea. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuweza kufikiria suala hili la pencheni kwa wazee wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika utoaji wa pencheni hii hapa kidogo nitowe ushauri kwa sababu ya malalamiko mbali mbali na hususani mengine ambayo nimeyasikia katika jimbo langu. Baadhi ya wale ambao wamepata pencheni katika huu mkumbu wa mwanzo, inasemekana kwamba kuna wengine wako chini ya miaka 70. Hili kama kweli limetokea basi ni tatizo.

Kwa hivyo, tunaiomba wizara inayohusika au serikali kwa ujumla, kuweza kulitazama vyema suala la utoaji wa pencheni, ili kuweza kuwakinga wale ambao hawana nia njema, kwa sababu waliolengwa ni wazee zaidi ya miaka 70. Sasa kuja kumkuta mtu ana miaka 50 au 60 anakwenda kuchukua pencheni ile kwa kweli hii hatuwatendei haki Wazanzibari. Kwa hivyo, suala hili liangaliwe kwa makini ili kuona haki inatendeka kwa wale ambao wamelengwa kuipata pencheni hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nije sasa katika suala la ongezeko la mishahara kwa wafanyakazi wa kima cha chini. Nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuweza kuitikia wito kwa malalamiko ya wafanyakazi, na katika kilele cha Mei Mosi kuweza kuahidi kwamba katika bajeti hii basi ataongeza mishahara kutoka shilingi 150,000/- hadi shilingi 300,000/- kwa kweli nimpongeze sana Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufikiria hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kutokana na tamko la Rais la ongezeko la mishahara hii, wananchi na hususani wafanyakazi wa kima cha chini wana matumaini na matarajio makubwa, lakini ni ukweli usiofichika Mhe. Spika, baada ya Mhe. Waziri wa Fedha kuwasilisha suala hili kwamba ongezeko hili litaanza mwezi wa Aprili, 2016 basi kumekuwa na nong'onong'o nyingi sana, hususani baadhi ya wananchi ambao nilizungumza nao katika jimbo langu.

Nimuombe sana atakapokuja Mhe. Waziri, sisi wajumbe inawezekana tukawa tunafahamu kwa nini ongezeko hili halitoanza mapema baada ya kuwasilisha bajeti hii, sisi wengine tunaelewa, lakini wananchi huko mitaani hawaelewi. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja basi aweke

wazi kwa wananchi juu ya ongezeko hili kutolewa kuanzia mwezi wa Aprili 2016, kwa sababu matumaini ya wananchi pamoja na wafanyakazi yalikuwa yapo mapema zaidi ya hapo.

Mhe. Spika, sasa nije katika suala zima la viinua mgongo. Niipongeze sana bajeti hii kwa kuweza kuangalia suala zima la kuweza kuondosha madeni au kupunguza au kulipa madeni ya viinua mgongo kwa wastaafu wetu, nimpongeze sana ni suala zuri ambalo litakuwa linawapunguzia mzigo na makali ya maisha kwa wastaafu wetu.

Hata hivyo, katika hili Mhe. Spika, kuna suala hili la wastaafu na pencheni zao. Kwa kweli mimi sikuweza kuona ndani ya bajeti hii kama limewagusa wastaafu ambao hivi sasa wengi wao wananung'unika au kulalamika au wale wana hali ngumu kutokana na kiwango kidogo cha pencheni.

Kwa hivyo, ningeishauri sana serikali kuweza kulitazama suala la pencheni kwa wastaafu wetu, kwa sababu siku hadi siku zinavyokwenda, basi viwango vyao vinadidimia na hasa tukitizama kwamba chombo chetu cha *ZSSF* ni chombo ambacho kinawekeza na kinazalisha. Kwa hivyo, ni muafaka sana kuweza kuwatazama hawa wastaafu wetu kwa jicho la huruma ili kuweza kuwaongezea viwango vyao na kuweza kupunguza makali ya maisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nije sasa kwa msajili wa vyombo vya moto na hususani katika vyombo hivi vya maringi mawili, vikiwemo vespa na pikipiki. Mhe. Spika, kwa kweli vyombo vya maringi mawili kwa Wazanzibari wengi hivi sasa vimekuwa ni vyombo vya watu masikini, watu wengi wanaojiweza hivi sasa wananunua magari. Lakini cha kushangaza Bima za vyombo hivi zinapanda siku hadi siku.

Mtu ambaye anamiliki chombo cha moto cha maringi mawili kama mkulima, kumuwekea Bima ya shilingi 59,000/- au 60,000/- kwa kweli ni kumtoza nguvu kwa sababu hali yake ya uchumi ni duni, lakini vile vile huku unamtwika mzigo mwingine wa Bima kubwa. Kwa hivyo, ningeshauri sana kwa kupitia Mhe. Waziri wa Fedha kuweza kulitazama suala hili la ongezeko la Bima kwa vyombo vya moto vya maringi mawili, ambavyo zaidi vinaendeshwa na wanyonge ili kuweza kuwapunguzia makali yao ya maisha.

Mhe. Spika, nielekeze mchango wangu katika suala zima la ajira. Naishukuru serikali na Wizara ya Fedha katika bajeti yake imeweza kuzungumzia vizuri sana suala la kuongeza ajira hususani kwa vijana.

Mhe. Spika, suala la ajira linaweza kupungua iwapo tu vyuo vya ufundi na vyuo vya amali vitaimarishwa, na katika bajeti hii imetaja juu ya kuweza kuimarisha vyuo vya amali katika visiwa vyetu, hili ni suala zuri naliunga mkono na kwa sababu na mimi ni mjasiriamali ambaye naendesha vyuo hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ili tuweze kuwasaidia vijana hawa katika kupata ajira, mara tu wanapomaliza vyuo hivi wangestahiki kuweza kupata mikopo ambayo itawawezesha kuanza miradi yao kwa ujasiriamali kwa mujibu wa fani ambazo wamezipata katika vyuo hivyo. Mhe. Spika, la kusikitisha sana, hivi sasa mikopo inayowahusu vijana wanaomaliza vyuo vya amali, sana inaelekea katika vyuo vya serikali. Hii inadunisha na kuweza kuteremsha ile ari ya vijana ambao wanapata mafunzo ya amali katika vyuo vya binafsi.

Ningependa sana niishauri serikali kuweza kulitazama hili, kwamba vyuo vingi ambavyo vinatoa wanafunzi basi vingi vyao ni vile ambavyo vinaendeshwa na sekta binafsi. Kwa hivyo, mikopo hiyo bila shaka na wao watakuwa na haki nayo ili kuweza kuona kwamba vijana wengi wanapomaliza vyuo hivi wana uwezo wa kujiajiri kutokana na nguvu za mikopo ambayo wanaipata kupitia serikali. Tukianza kuleta ubaguzi wa mikopo kati ya vyuo vya serikali na vyuo binafsi, nafikiri lengo la serikali la vijana kuweza kujipatia ajira nyingi halitafikiwa.

Mhe. Spika, pamoja na hayo sasa nielekee katika suala zima la miradi ya serikali. Nimepata faraja sana kuweza kuona kwamba serikali imeweza kuona kwamba, kuna haja sasa ya kuweza kupunguza miradi ya maendeleo iwe kidogo lakini yenye kutekelezeka, kuliko vile ambavyo ilikuwa nyuma, tulikuwa tunatekeleza miradi mingi lakini hatimaye tunaiwacha njiani.

Ni ukweli usiofichika Mhe. Spika, kwamba unapouwacha mradi iwapo haukukamilika, unapokuja kuurejea basi gharama zake zinakuwa karibu mara mbili au tatu ya zile ambazo zilipangwa mwanzo. Hivi sasa kuna barabara nyingi sana na hususani katika eneo la Magharibi na Kati, kuna barabara karibu tatu zimelala. Barabara zile utakaporudiwa mradi wake utakuta kwamba nyingi tayari zimeshaharibika, kwa hivyo tunaanza kazi mpya. Pesa zinakuwa ni nyingi zaidi, kwa hivyo niipongeze Serikali kwa kuweza kuliona suala zima la kuweza kuwa na miradi michache, lakini yenye kutekelezeka ili kuona kwamba tunaweza kumudu kuzitumia pesa zetu ambazo ni kidogo kwa vizuri zaidi.

Katika hili vile vile ningezungumzia suala zima la mradi ule ambao unaendeshwa na kampuni ya Kichina ambayo ni ya utoaji wa maji machafu

katika maeneo mbali mbali ya Mji wa Zanzibar. Nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mhe. Rais kwa kuweza kufikiria kuweka mradi ule ambao utapunguza kero kubwa sana la utoaji wa maji machafu katika maeneo mbali mbali ya Mji wa Zanzibar na ambayo kwa kweli wakati wa mvua yanaleta usumbufu sana.

Mhe. Spika, katika suala hili mradi huu ambao unaendea hivi sasa kwa kweli unaonekana kama unasua sua na hili ningependa nitahadharishe sana serikali, kwa sababu wananchi wanatokea katika kipindi cha mvua. Wananchi wengi katika kipindi hiki walipata maafa ya mafuriko na serikali ikatumia pesa nyingi sana katika kuwafariji na kuwahudumia wananchi hawa.

Vile vile, Serikali hususan kupitia Wizara ya Elimu wanafunzi wameathirika sana kwa kukosa masomo hasa kwa kufunguliwa kwa kambi ile ya Skuli ya Mwanakwerekwe C, sasa ili matatizo haya yasije yakatokea katika msimu mwengine wa mvua basi ni vyema sana mradi huu ungeweza kusimamiwa vizuri kuona kwamba unamalizika kwa wakati. Lakini wasi wasi wangu kwamba kuna taarifa kwamba kuna baadhi ya majengo ambayo yalipaswa yaondolewe, ili kupisha mradi huu mpaka leo wenyewe hawajalipwa na hususan katika jimbo langu la Magomeni.

Kwa hivyo niiombe sana Wizara ya Fedha ambayo ndio ilitiliana sahihi mkataba na kampuni hii kuweza kuona kwamba kama ni sahihi basi wale wenye majengo ambayo wanatakiwa yapishe mradi basi yalipwe, ili kuona mradi huu unafanikiwa kutekelezwa kwa wakati, ili na wananchi wangu nao wa Jimbo la Magomeni waweze kuondokana na adha ya kutuama maji kila unapofika msimu wa mvua.

Mhe. Spika, baada ya michango hiyo niseme tu kwamba bajeti hii ni bajeti nzuri na nimshukuru sana Waziri wa Fedha na watendaji wake kwa kuweza kuiandaa bajeti hii na kuiwasilisha hapa, na mimi sina wasi wasi na utekelezaji wa bajeti hii kwa sababu imeandikwa kitaalam na imepangika vizuri. Kwa hivyo naunga mkono bajeti hii kama walivyotangulia kusema Wajumbe wenzangu asilimia mia kwa mia. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia bajeti hii ambayo imewasilishwa tokea jana na Mhe. Waziri wa Fedha.

Awali ya yote kwanza napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subuhana Wataala kwa kunijaalia siku ya leo nikaweza kupata fursa

hii. Vile vile Mungu kwa kutujaalia sote tukiwa wazima wa afya na tukiwa tunaendelea na majukumu yetu kama vile wajibu unavyotutaka tufanye.

Pia, napenda nichukue fursa hii kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa uteuzi wako, lakini vile vile napenda nichukue fursa hii adhimu na kwa moyo wangu thabiti kuwapongeza wananchi wa Jimbo langu la Micheweni. Mapenzi yao na ukarimu wao ambao waliwouonesha kwangu na leo wakanichagua mimi na kuweza kuwasemea hapa katika chombo cha kutunga sheria kwa moyo wao thabiti.

Napenda nichukue fursa hii kukipongeza Chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kupitisha jina langu na leo nikaweza kuwa Muwakilishi wa Jimbo la Micheweni. Pia napenda nichukue fursa hii kuwapongeza wale wote ambao wameteuliwa na Mhe. Rais kwa kuwachagua kumsaidia kutekeleza majukumu yake kama vile ambavyo majukumu hayo yanatakiwa yafanyike. Vile vile, napenda nichukue fursa hii ya dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha hotuba yake ambayo imeweza kwenda sambamba na hotuba ya Mhe. Rais ambayo aliizindua hapa kwenye Baraza.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika katika mazingira ya sasa ni vyema kabisa katika hali hii ambayo tunayo na twende nayo na kuweza kujikita zaidi katika kuona tunatoa mashirikiano ya dhati, kwa kuona dhamira ya Serikali yetu inafanikiwa kama vile ambavyo inataka kufanikiwa. Lakini baada ya hapo napenda nichukue fursa hii na mimi kwa jioni ya leo niweze kuchangia machache katika maeneo yafuatayo.

Kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kuyataja baadhi ya maeneo ambayo nitaweza kuyagusa kwa kuchangia laasiri hii ikiwemo muelekeo wa matumizi ya bajeti ya mwaka 2016/2017. Lakini vile vile nitagusa katika malengo makuu ya bajeti kwa mwaka 2016/2017, nitaangalia katika hatua za kuimarisha ukusanyaji wa mapato mwaka 2016/2017 na vile vile mwisho kabisa nitachangia katika hatua za kubana matumizi.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba Kamati ya wenyeviti wa kamati za kudumu za Baraza katika hotuba yao ambayo wemetoa mchango wao jana, katika ripoti yao leo imeonekana imegusa kwa kila maeneo, cha msingi zaidi ni kwamba imekidhi mahitaji na sisi tutaweza kuongezea kwa mujibu ambavyo tunaona kwamba inafaa zaidi. Kwa hivyo moja kwa moja Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuanza eneo moja baada ya jengine katika yale ambayo nimeweza kuyataja.

Kwanza kabisa katika muelekeo wa matumizi ya bajeti Mhe. Spika, naomba ninukuu.

"Kutokana na mwelekeo wa hali ya fedha sera kuu ya matumizi inahitaji kubana matumizi zaidi kulingana na vyanzo vya mapato vilivyopo kutoka mwelekeo huo mkazo katika matumizi utalenga katika mambo yafuatayo".

Kupitia hotuba ya Mhe. Waziri moja katika mkakati huo ni kupunguza madeni hasa ya kiinua mgongo, vile vile kulipa madeni ya walimu jambo hili ni ukweli usioweza kufichika katika maeneo yetu au katika nchi yetu watumishi ambao wamemaliza muda wao miongoni mwao bado wanaendelea kuidai Serikali na hadi sasa hivi hawajalipwa na wanaendelea kufuatilia hatua kwa hatua kadri wanavyoweza.

Mhe. Spika, naomba niiombe Serikali yangu ifanye juhudi za makusudi na za haraka katika kuona suala hili inalikamilisha kwa wakati, kwani baadhi ya wakati naweza kusema inasikitisha sana kwamba mfanyakazi tokea ameajiriwa anajulikana ni siku gani ambayo anastaafu au kumaliza muda wake wa utumishi Serikalini, lakini inahuzunisha sana kwamba ifike wakati mzee amemaliza kufanya kazi ya kutumikia nchi hii na hatimae tena aanze kuhangaika baada ya kutoka kazini, kile ambacho wanaahidiwa kuweza kukipata badala yake akitumie kwa ufuatiliaji katika kuona anapata stahiki yake.

Kwa kweli jambo hili ni wakati sasa ni vyema tuweze kubadilika zaidi katika kujali utumishi, kwa sababu leo wazee wetu hao nao walikuwemo humu humu na sisi ambao tunapiga kelele tunatarajia hivyo hivyo ifike siku na sisi tuje kutafuta hizo haki zetu, na sisi tusije tukapata usumbufu kama wanavyoendelea kupata wazee wetu. Kwani kuna baadhi ya watumishi ambao wamemaliza muda wao wa kazi tokea mwaka 2013 na sasa hivi bado hawajapata stahiki zao kwa mujibu wa sheria.

Ningeomba Serikali kupitia Wizara husika kwamba sasa kumekuwa na baadhi ya ushauri na malalamiko kwa baadhi ya watumishi, kwamba wao wanapomaliza muda wao wa kazi au wa utumishi walikuwa wanahitaji waende wakatekeleze wajibu, yaani waende wakahiji Makka na hatimae wanafika wakati tayari nguvu zimepungua na sehemu ya Makka au sehemu ya Ibada hii, wakati mwengine tunaona kama ni sehemu ambayo inahitaji mtu aende ambae ana nguvu kwa kiasi fulani katika mwili wake.

Hivyo basi kwa sasa ningeiomba Serikali iangalie utaratibu kwa wale ambao wanamahitaji maalum ya kutaka kwenda kutekeleza wajibu huko Makka, basi kuweko na utaratibu maalum ambao utaweza kumfanya mfanyakazi au mtumishi wetu ambae anahitaji kwenda kutekeleza wajibu huo. Basi katika lile fungu lake au makusanyo yake yale ambayo anatarajia ayapate baada ya kumaliza kazi, basi kuwe kuna utaratibu ambao utamfanya aweze kupata angalau asilimia fulani, ili aweze kwenda kutekeleza majukumu hayo au kwa mujibu wa imani inavyoelekeza.

Mhe. Spika, naomba nieleweke kwamba sizungumzii kwamba labda masuala ya udini zaidi, nimeangalia kwamba mtu yeyote ambae atakuwa na mahitaji kama hayo hata kama kwa utaratibu mwengine, au madhehebu nyengine au utaratibu wa dini nyengine. Basi ni vyema jambo hili hatuwezi tukakaa tu tusilizungumzie kwa sababu sheria au Serikali yetu inazo fursa ambazo zinashughulikia masuala ya dini. Kwa hivyo kuzungumzia suala hili hapa nadhani ni jambo la msingi kwangu na ambalo linahitaji nilisemee kama vile ambavyo naona inafaa.

Mhe. Spika, vile vile niangalie katika malengo makuu ya bajeti, Mhe. Spika, naomba kunukuu; "Kwa kuzingatia malengo makuu ya Serikali na mustakbali wa bajeti kwa mwaka ujao wa fedha 2016/2017, inatarajiwa kwamba katika kila shilingi itakayotumika katika nchi yetu katika utekelezaji wa majukumu yetu sent 58.7% ziende katika sekta tano zinazobeba malengo makuu ya Serikali zikiwemo Mawasiliano na Usafirishaji, Mafunzo ya Amali, Maji, Mifugo na Uvuvi na mambo mengineyo kama hayo".

Mhe. Spika, na mimi naomba nichukue fursa hii kugusia kidogo katika mazingira haya au kuchangia kwa mujibu ninavyohisi inaweza kusaidia. Kwa mazingira haya ya Mawasiliano na Usafirishaji ningeomba Serikali fedha hizi ambazo zimetajwa zinatarajiwa kwamba zinaweza kufika Tanzania Shs. 494.2 bilioni, kati ya shilingi 841.5 milioni za matumizi ya Serikali yote.

Mhe. Spika, ningeomba katika maeneo haya bado Mhe. Waziri wa Fedha hakuainisha hasa katika mazingira haya au katika maeneo haya au taasisi hizi kwamba ni mambo yepi zidi ambayo yanaweza yakaguswa kwa kupitia fedha hizi ambazo zitakusanywa. Hivyo basi nitoe tahadhari kwamba ni vyema tuwe makini katika makusanyo hayo lakini vile vile tuwe makini katika matumizi hayo ambayo tunalenga katika kuziboresha sekta hizi. Kwa sababu mara nyingi katika awamu zilizopita tunaweza tukashuhudia kwamba kuna mfuko unachangiwa ambao sitaki nitoe mifano, lakini hatimae ukija ukiangalia basi unakuta kwamba fedha hazikutumika vizuri.

Hivyo basi naomba Mhe. Waziri kupitia Wizara yake kwamba kuona watendaji wenzanke kuona kwamba mazingira haya au maeneo haya ambayo yamekusudiwa kutengewa fedha basi tuwe makini sana katika kuona kwamba zinatumika kama vile ambavyo Serikali imekusudia. Lakini pamoja na maelezo hayo ningeiomba Serikali yangu kuangalia katika mafunzo ya amali, vijana wengi katika nchi yetu tumeona kama suala la ajira limekuwa likilalamikiwa sana, hata hivyo ukiangalia uhalisia jambo hili lina ukweli. Hivyo basi Mhe. Waziri ningeomba kwamba aangalie zaidi katika yale maeneo ambayo yanaonekana kwamba umasikini umekuwa ukionekana una viashiria vikubwa zaidi ukilinganisha na maeneo mengine.

Kwa mfano nimekuwa nikifuatilia hata katika Baraza lililopita au hata ukiangalia sensa ya mwaka 2012 tumeshuhudia bado Micheweni inaonekana kwamba kuna viashiria vya umasikini ambavyo vimekithiri. Ni vyema sasa Serikali yangu kuona kwamba sasa iko haja ya kuangalia mazingira kama hayo na Wilaya nyengine ambazo zimetajwa zikifuatia kutoa vipaumbele, ili kuona kwamba tunaweza kutatua hili suala la mapungufu ya ajira. Ndio maana hata ukiangalia katika Jimbo langu, kwa mfano la Micheweni nikitoa mfano leo unakuta hata ukitathmini wale watu ambao hawaitakii mema nchi hii ndio maeneo waliyokimbilia kutokana na kuwatia tamaa vijana wetu katika mambo ambayo hayana msingi, hatimae kufanya mambo yanayopelekea uvunjifu wa amani. Hivyo basi tuelekeze nguvu zaidi katika maeneo yale, ili kupunguza hali hii ya kuweza kuwatia tamaa na hatimae kuwatumia vijana wetu vibaya katika kuihujumu nchi yao.

Mhe. Spika, vile vile, suala la maji naomba tuliangalie, namuomba Waziri au Wizara inayohusika basi pale atakapofika tuone kwamba tunaliangalia kwa kina, kwa sababu kwa sasa nikitoa mfano kwa Micheweni ijapokuwa na maeneo mengine yapo, lakini nazungumzia pale ambapo tunaweza kutoa mfano ambao kwa uhalisia. Mhe. Spika, katika jimbo la Micheweni mtandao wa maji umeenea takribani maeneo mengi, lakini ukija suala la upatikanaji wake hayo maji umekuwa ni dhaifu mno. Yaani kuna baadhi ya maeneo mengine maji hayafiki, hii inatokana na kwamba miundo mbinu tuliyonayo ni zamani mno ambayo haiendani na wakati wa sasa.

Hivyo basi katika maeneo mengine kama haya Serikali ni vyema kufikiria upya na kuangalia suala hili kwa sababu malalamiko ya upatikanaji wa maji kwa baadhi ya maeneo, hususan katika jimbo langu au Wilaya ya Micheweni inaonekana likishamiri zaidi ijapokuwa mtandao wa maji unaonekana upo.

Vile vile katika suala la mifugo na uvuvi Mhe. Spika, ningeomba kwa sasa tuangalie katika sekta hizi pia tuangalie ufanisi zaidi katika yale ambayo nimesema ni tahadhari ndio naendelea katika kutoa mchanganuo katika mazingira haya. Kwa mfano katika Wilaya ya Micheweni ukiangalia kwa sasa katika nchi yetu ili tuweze kupiga hatua kwa masuala mazima ya ufugaji wenye tija. Hatuna budi tuingie katika ufugaji wa kisasa, tukiingia kwenye ufugaji wa kisasa ufugaji huu ni kwamba unahitaji maeneo machache au madogo ukilinganisha na wafugaji wetu ambao tuliokuwa nao tuliorithi kwa wazazi wetu.

Hivyo basi ufugaji huu pia hatuwezi tukaufanya kama tutakuwa hatuwezi kuangalia mambo mengine ya msingi, kwa mfano upandishaji ng'ombe kwa sindano tukiweza kuzisambaza mbegu za ng'ombe wa kisasa, basi nadhani hili linaweza likafanikiwa na tukaweza kufika tukaona tunatumia maeneo madogo na makubwa yaliyobakia tukaweza kutumia kwa shughuli nyengine na ardhi yetu tukaweza kuitumia vizuri na ikaweza kuleta tija kwa kila nyanja.

Hivyo basi tuliangalieni hili kwa msingi wake lakini sambamba na hilo tuangalieni kada ya utumishi, watumishi waliopo inaonekana ni pungufu sana hususan nikitoa mfano kwa Wilaya ya Micheweni, watu ambao wana dhamana ya kulisimamia jambo hili la upandishaji wa ng'ombe kwa sindano ni wafanyakazi wawili, ambao wafanyakazi hao wawili ni watu ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu karibu wanaelekea katika miaka yao ya kustaafu. Sambamba na hilo hao wafanyakazi ukiangalia hata nyenzo za usafiri hakuna, mmoja ambae anamiliki usafiri hata wa Serikali katika kusambaza mbegu zile, na mbegu hizi huwezi kuzisambaza kwa kutumia baskeli isipokuwa unahitaji kupata chombo cha moto kama ni pikipiki ama vyenginevyo, kwa hivyo mazingira kama haya vile vile tuyaangalie.

Vile vile, tuangalie lakini ukiangalia pia na masuala ya uvuvi katika nchi yetu nadhani sasa umefika wakati, hizi fedha ambazo tunazilenga tuzitumie hapa au tusaidie hapa tuangalieni uvuvi ambao ni wa kisasa zaidi. Kwa mfano, kuna miradi chungumzima ambayo tumeweza kuishuhudia kama vile mradi wa *MACEMP* na miradi mengine yameweza kununua vifaa lakini hatimae kama vile ambavyo wengine wameweza kuchangia sina haja ya kufafanua, kwa hili lazima tuwe makini zaidi. Sambamba na hilo kama nilivyosema sifahamu kama fedha hizi zitatumika katika mazingira yepi zaidi ndio maana nikachangia kwa mujibu vile ninavyoona mimi inaniwajibikia.

Mhe. Spika, pia tuangalie katika mazingira ya nchi yetu asilimia kubwa ya wakaazi wa visiwa vya Zanzibar ni wavuvi hususan kwenye Jimbo langu la

Micheweni nathubutu kusema asilimia 90 watu wa kule ni wavuvi. Hivyo basi, ukiangalia na sasa hivi fedha tunazopata pato letu katika nchi yetu utalii ni sekta moja ambayo tunaiangalia iingize uchumi kwa kiwango kikubwa mno nchini mwetu.

Vile vile maeneo yale ambayo wavuvi wetu wangeweza kupata faraja au wakaweza kutumia na wao wakaweza kupata kuitumia kwa kuongeza kipato takriban yote unaambiwa ni hifadhi, zimetajwa hifadhi kuanzia Pemba mpaka Makunduchi. Kwa hiyo, ningeomba tuangalie utaratibu mmoja wa kuweza kuwasaidia wananchi wetu hatuwezi tukalikwepa hili kwa mazingira yetu tuweze kuacha utalii uendelee kufanya kazi, lakini na wananchi wetu wanapata tabu katika masuala mazima kwa kazi ambazo wamejiajiri kwa wingi na ambapo wanapata tija na ndio wanachotegemea katika maisha yao.

Mhe. Spika, ningeshauri utaratibu wa baharini kwa mfano mimi nilikuwa mvuvi. Leo katika mazingira ambayo yamewekea hifadhi au palipokuwa haparuhusiwi kuvuliwa, maeneo yale ni kwamba samaki huwa ni kimbilio na ni sehemu ambayo wanaweza wakazalishana kwa wingi. Kwa hivyo, mazingira mbali mbali yanaweza yakajitokeza katika maeneo yale. Kwa mfano, pale kwenye maeneo yale ambapo pana hifadhi ni kwamba samaki wakubwa nao pia huchukua fursa yakwenda kutembelea maeneo yale kuona jinsi gani wanaweza kujisaidia kwa kupata chakula chao kwa urahisi zaidi.

Mhe. Spika, kuendelea kuwepo idadi kubwa ya samaki katika eneo fulani pia ni hivyo hivyo kunaweza kukahatarisha maisha ya wageni wetu. Kuna baadhi ya samaki wameshakuwa wakubwa katika bahari wanakuwa wanafanya majaribu kuweza kukamata kitu huwa wanajilinganisha kama kile anaweza kupambana nacho. Pia baadhi ya wakati anaweza hata akapita mgeni wakaweza kumuhujumu au kuweza kumpatia maumivu makubwa ama ulemavu au kumuua kabisa.

Kwa hiyo, ningeomba kwamba sipingani na utaratibu kuwa utalii ndio sehemu ambayo inatuongezea pato, lakini yale maeneo ambayo kuwa ni tengefu katika hifadhi pamoja na masuala mazima ya utalii tungeandaa utaratibu maalum wa kuweza kuwaruhusu wavuvi wetu kila inapofika kipindi fulani wakaruhusiwa wakenda kupatumia pale kwa kuvua kwa lengo la kuongeza kipato chao wao wenyewe, pamoja na serikali yetu inaweza ikapata mapato zaidi na kuongeza idadi na kiwango cha uzalishaji mkubwa wa samaki.

Mhe. Spika, bahari yetu sasa hivi inao samaki wengi, lakini sisi bado hatujaweza kuwamudu au kuweza kuwafikia kutokana na zana zetu duni

ambazo bado tunaendelea kuzitumia. Mhe. Spika, hususan katika kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani ningeshauri wizara iandae utaratibu maalum kwenye yale maeneo, kwa mfano maeneo ya Fumba, Pungume ni sehemu nzuri ambazo wananchi wetu au wavuvi wetu wa Zanzibar wanaweza kwenda katika msimu kama huu wakaweza kupata samaki wengi na wakaweza kujisaidia katika maisha na sisi vile vile wenyewe tukaweza kutumia fursa hizo za wavuvi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba nielekee katika hatua za kuimarisha mapato. Katika hatua za kuimarisha mapato ya serikali, naomba kunukuu kifungu cha 69.

"Mhe. Spika, pamoja na kuzipongeza na kuzishukuru taasisi za ukusanyaji wa mapato, *TRA*, *ZRB* na wizara mbali mbali, serikali inaamini kuwa bado kuna fursa ya kukusanya mapato zaidi kutokana vyanzo vya ndani kuliko kiasi kinachokusanywa kwa sasa. Kwa sababu hii, kwa mwaka ujao wa fedha 2016/2017 haipendekezwi kupandisha kodi kwa yoyote katika vianzio vyake vya mapato ya ndani, zaidi ya kurekebisha viwango vya ada mbali mbali vilivyopitwa na wakati. Badala yake, inashauriwa kuendelea na hatua mahsusi za kupanua wigo wa kodi, kuimarisha ufanisi katika ukusanyaji, na kuongeza uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato".

Mhe. Spika, jambo hili na mimi nasema kwamba nafurahia sana kuwa hatua hii ya serikali ni nzuri na ina mwelekeo na inaweza kutusaidia na kutufikisha pale ambapo sasa nchi yetu inaelekea na kwa kasi hii naamini kuwa tunaweza tukafika kwa mujibu wa malengo yetu.

Mhe. Spika, katika hatua hii na mimi nasema kwamba bado naamini kama wizara ilivyosema inaamini kuwa yapo maeneo ambayo tunaweza tukayatumia yakaweza kuongeza ukusanyaji wa mapato katika nchi yetu. Kwa mfano, niangalie katika sekta ya mifugo kwenye sheria za kusimamia maliasili ya mifugo ya mwaka 1999 na mapendekezo ya malipo na ada za huduma za mifugo. Kwa mfano, ukiangalia katika suala zima la usafirishaji wa mifugo ndani ya nchi kutoka eneo moja kwenda eneo jengine vile vile kusafirisha mifugo kutoka Tanzania Bara kuja nchini.

Mhe. Spika, kwa mfano naomba nianze kwa kuchambua kwa kiasi kidogo, nitoe mfano ng'ombe mmoja ambaye anaingizwa nchini. Ukiangalia Tanzania Bara ng'ombe mmoja anaweza akafika kwa thamani ya kati ya shilingi 900,000 mpaka 1,200,000 ng'ombe wa kisasa, lakini ukija katika ada za kumuingiza nchini tozo yake ni shilingi 1000.

Sasa Mhe. Spika katika kodi hii kwa kiasi fulani unahisi inaweza ukaona kwamba bado tunaweza tukafanya vyenginevyo katika maeneo haya kuweza kutanua kidogo ukusanyaji na tukaweza kupata zaidi. Nadhani tusiwe na hofu katika mazingira haya kwa sababu mara nyingi mtu ambaye anachukua nafasi ya kuleta mifugo hapa nchini si mfugaji wa kawaida au si mwananchi wa kawaida. Badala yake ni watu ambao wana uwezo au ni wafanyabiashara ndio ambao wanaweza kufanya kazi hiyo.

Kwa maana hiyo kuendelea kubakia na shilingi 1000 kwa kuingiza mnyama mmoja kwa mfano ng'ombe kumleta nchini kwa shilingi 1000 bado makusanyo haya hayaendani na wakati wa sasa. Lakini kwa mfano sasa hivi nchi yetu imekuwa ikitoa vibali vya kuingiza ngamia, shughuli nyingi zinafanywa kwa kutumia nyama ya ngamia. Lakini ngamia mpaka sasa hivi katika sheria hii ambayo nimeitaja ya mwaka 1999 bado haijaweka bayana kwamba ngamia akiingizwa hapa nchini atozwe tozo kiwango gani, hii bado ukiangalia kuna jambo la kufanya.

Mhe. Spika, nikiachana na hatua hiyo ukija katika ukaguzi wa nyama, kwa mfano ng'ombe mmoja aliyechinjwa kwa kawaida ada ya sasa ambayo imepitishwa mwaka 2011, unakuta ng'ombe mmoja ambaye amechinjwa na kukaguliwa nyama yake haizidi shilingi 2800. Hivi sasa thamani ya mnyama mwenyewe na ile tozo inayotolewa bado haiendi kuona kwamba kuna mazingira ya jambo tunaloweza kulifanya.

Mhe. Spika, tukiachana na hayo sheria yetu tumesema ni msumeno, lakini vile vile katika jambo hili bado hatujawa makini. Kwa mfano, leo unakuta katika wananchi wa kawaida ambao ni walaji wao wanalazimika kuweza kutii sheria hii na badala yake kutozwa tozo fulani kwa mujibu wa kazi au uchinjaji wa mifugo ambayo wameifanya. Lakini bado kuna taasisi za serikali sheria hii imepitishwa na serikali ukiangalia kuna taasisi za serikali hazijaona umuhimu wa kulipa kodi au kukaguliwa na badala yake kuweza kulipa ada. Taasisi mbali mbali zipo hususan kipindi cha msimu wa sikukuu tumekuwa tukishuhudia taasisi mbali mbali za serikali ambazo zinaweza kujichinjia mifugo kiholela na badala yake hawatowi chochote wanapofanya kazi hiyo.

Mhe. Spika, naomba tukubali kupitia Baraza letu hili kwamba sasa muda umefika wa kubadilika kwa yale ambayo tunayoyasema, isiwe leo sisi tunawahimiza wananchi walipe kodi lakini bado kukawa kuna taasisi wao sheria wanazivunja na badala yake hakuna chochote kinachoendelea.

Mhe. Spika, nitoe tahadhari kwa sasa niwanasihi sana waheshimiwa wenzangu katika utaratibu wa sasa sheria yetu ya kuingiza mifugo nchini, inakuwa ni sheria ambayo inatoa fursa na tukubali moja katika ukaguzi wa nyama unafanywa kwa malengo tofauti. Moja ni makusanyo na pili ni kulinda afya za watumiaji wa nyama zile ambazo wanataka kula.

Tuamini kwa sasa Tanzania Bara huwa kunaripotiwa baadhi ya magonjwa ambayo ni hatari kwa binadamu, hivyo kuendelea na mazoea ambayo tunayo ya kuweza kutumia pasi na kuangalia na kulipa umuhimu jambo hili ni kujiweka katika mazingira hatarishi na hatimae tunaweza tukaja tukawakosa watu wetu ambao ni watumishi tulikuwa tunawapenda sana na ni mahodari katika utumishi wao serikalini.

Mhe. Spika, tuangalie kwa mfano kama ambavyo tumeona katika masuala ya kipindupindu ambayo sasa hivi nchi yetu tunaendelea kupata tabu. Nadhani tahadhari za usafi zilikuwa zikizungumzwa sana na tulikuwa tunaona labda mambo yako mbali lakini sasa tumelazimika kufunga migahawa na mahoteli kwa ajili ya kupambana na kuondoa tatizo la kipindupindu. Naomba nitoe tahadhari kwenye mifugo watumizi ambao tunatumia matumizi ya nyama, tukumbuke kwamba kuna magonjwa mbali mbali ambayo unaweza ukashtuka kuwa umeondoka na ugonjwa na hatimae kifo pasi na kutambua wapi ulianzia.

Mhe. Spika, vile vile, kuna ugonjwa wa *TB* hii inaweza ikatoka kwenye ng'ombe na hatimae unaweza ukaipata wewe binadamu ama kwa kunywa maziwa yaliyokuwa ya mnyama ambaye ana *TB* na vitu vyengine kama hivi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ambayo kwa ufupi na mimi napenda kusema kwamba hotuba hii ya bajeti ambayo imewasilishwa kwetu hapa Barazani. Niseme ni nzuri na imekidhi vigezo na masharti yote ya kupitishwa katika Baraza hili tukufu, na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Micheweni niseme kwamba naunga mkono asilimia mia moja hotuba hii kwa kadri ilivyoonekana katika uwasilishwaji wake. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima wa afya na nguvu kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu ikawa miongoni mwa wachangiaji kwa siku ya leo. Vile vile Mhe. Spika, sina budi kukupongeza wewe binafsi yangu kwa kuchaguliwa kuwa kiongozi wa Baraza hili kwa nafasi ya Uspika. Pia nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa ushindi wa kishindo alioupata kuongoza katika visiwa vyetu hivi.

Mhe. Spika, vile vile nawapongeza Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi waliotoka katika majimbo yao, viti maalum na waliopata uteuzi wa Mhe. Rais. Pia nachukua fursa hii adhimu kuwapongeza wateule wote katika nafasi za uwaziri na naibu waziri ili kumsaidia Rais wetu kazi ya kutusogeza mbele katika Serikali yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, shukurani zangu nyengine za dhati napenda kuzitoa kwa wapiga kura wangu wananchi wapendwa wa Jimbo la Jang'ombe kunichagua kuwa mwakilishii wao na leo hii nafanya kazi moja ambayo wamenituma kuja kuwaletea mapendekezo yao katika Baraza hili. Baada ya kutoa shukurani za dhati moja kwa moja mimi nitakwenda katika hotuba ya Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 12 katika *infrastructure* ambapo imeonesha hapa kuna vipengele mbali mbali vya ukusanyaji kodi.

Mhe. Spika, lakini tukiangalia kwa dhati kabisa tunakuta mengine imekuwa kidogo ni tofauti wameongeza mzigo kidogo kwa wananchi wetu wa hali ya chini. Nitazungumza kwa haraka haraka juu ya suala la asilimia 2 ya ununuzi wa umeme. Hii asilimia 2 ya ununuzi wa umeme ni pesa nyingi sana wakati hata kabla haijaongezwa kodi hiyo tayari umeme ulikuwa ni mzigo kwa watu wetu kutokana na matumizi na gharama ya uendeshaji na pesa nyingi kwa kununua umeme huo.

Kwa hiyo, tayari tumeingiza kodi asilimia 2 tayari tunamuongezea mzigo mtu wa chini katika matumizi ya umeme huo. Vile vile wakati tungeenda vizuri tungeweza kuongeza pato letu zaidi sehemu ya wasafiri wanaotumia viwanja vya ndege na bandari, lazima kungekuwa na tofauti katika hivyo viwili baina ya bandari na uwanja wa ndege.

Mhe. Spika, tunajua kwamba mtu yeyote ambaye imani yetu inatupa kwamba anayesafiri kwa ndege anakuwa tofauti kipato na yule ambaye anasafiri kwa boti. Kwa hiyo, basi ile tofauti kidogo ionekane iwepo baina ya anayesafiri kwa ndege na boti angalau iongezeke hapa kidogo ili kuzibaziba mapengo kwenye mambo ambayo tunaona haya tunamkamua mtu wa chini. Leo hii mtu wa kijijini anaweza kwenda kununua *unit* zake za shilingi 5000 kuna asilimia 2 ambayo inambinya huo ni mzigo mkubwa kwa kweli.

Mhe. Spika, vile vile katika hayo tunakuta katika ukusanyaji wa kodi hiyo ni nani hasa ambaye anapaswa kulipa kodi ya miundombinu, mlaji au ni

mfanyabiashara? Sasa tukitazama ni kawaida kwamba kodi ile inakusanywa na *ZRB* na *ZRB* kawaida hukusanya kodi za mlaji. Kwa hiyo, tunawapa mizigo mikubwa watumiaji hawa ambao wanalipa kodi hizi, kama mfano kodi tuliyozungumza ya asilimia 2 ya umeme na vile vile suala la usafiri ambapo mtu anakwenda Pemba anatozwa shilingi 2000. Kwa hiyo, inawezekana ikawa inatozwa lakini mtu ambaye anatumia uwanja wa ndege kwa kusafiri kwenda Pemba au nje ya Tanzania basi ingezidi kidogo kungekuwepo tofauti ingeweza kusaidia ku-*push* mapato yetu.

Mhe. Spika, pia ningependa kuzungumzia suala zima la ulipaji wa dola 1 kwa mgeni, ambayo inaingia katika kodi hii ya *infrastructure* ambayo tunamwambia mgeni anapokuja hapa awe tayari kutuchangia kwa ajili ya kujenga barabara, shule zetu, kutafuta maji wakati tayari kuna kodi ameshailipa au anaendelea kuilipa. Sasa basi ingekuwa ni busara zaidi tungetafuta njia mbadala ya kuongeza kodi katika nchi yetu ili tukapata kipato zaidi kuweza ku-*cover* sehemu ambayo iliyobakia ya milioni 349,000,0000 ambayo tunategemea ruzuku na mikopo ukilinganisha na 450 ambayo ni ya ndani.

Katika hilo basi nafikiri tungeenda moja kwa moja *proper tax* ambapo kuna nafasi kubwa sana ya kukusanya kodi, majengo yako mengi yenye kulingana kwa utofauti wa uhali wake, nafikiri ingekwenda pale basi tungewapangia sheria tukaangalia je tukusanye kodi kwa kiwango gani au kwa mwenendo gani ingetusaidia kuongeza mapato katika nchi yetu, tofauti na kuweka hizi kodi ndogo ndogo ambazo tunamuonea mtu wa kijijini kule ambapo maisha yao tunajua kwamba hayako mazuri hata hivyo.

Mhe. Spika, katika hilo tunapokwenda katika *proper tax* itasaidia kuondoka hata malalamiko ya kusema miji yetu michafu, barabara za ndani hazipo kodi hii ingekuwa itakusanywa ingeweza kukidhi katika utengenezaji wa miundombinu yetu mizuri. Hata maskuli yetu ingekuwa inachangia katika kodi hii ya *proper tax.*

Mhe. Spika, vile vile ningependa kuzungumzia juu ya suala zima la *temporary transportation*. Hii imekuja baada ya kwamba upande wa Zanzibar hatuwezi kutumia fursa hii kama wana Jumuiya wa Afrika Mashariki. Wenzetu wana jumuiya wana nafasi nzuri sana ya kutumia *transportation,* nazungumza juu ya masuala yao pengine vipando vyao vya magari. Wanapokwenda sehemu moja ya *East Africa* wanapata fursa hiyo kwenda *border* au sehemu yoyote kuwasilisha nyaraka halisi na kupata *release* pengine ya kulipa Dola 100

wakatembea na magari yao katika sehemu zile, japo hili suala lilizungumzwa na Mjumbe aliyepita, lakini mimi nalikazia kamba kwa nini kwa Zanzibar hatupati fursa hiyo.

Halafu nasema sisi pengine kama viongozi tunaweza tukapata tukatumia barua tukaombana, tulikwenda Dodoma tukaruhusiwa kwenda na magari yetu, lakini wale wapiga kura wetu ambao na wao wanataka kutumia fursa hii kama ambavyo wanatumia watu kutoka *South Africa*. Mfano wanatoka watu Jumuiya ya *SADC* au *South Africa* huko au tuseme katika *East Africa* Burundi, Rwanda kuja na magari yao Zanzibar inakuwaje Zanzibar hatuwezi kutumia?

Ni kero ya muda mrefu sana. Zimeundwa kamati mbali mbali lakini bado inakuwa pengine mtu kwa utashi wake kwamba lazima anazuwia kuwa Zanzibar isitumie fursa hii basi imekuwa limenyamaziwa, lakini ni sababu ambayo inakera na inatukandamiza kabisa sisi Wanzanzibari na itabidi lazima tulizungumze, hatutaweza kunyamaza mpaka tuhakikishe tunatumia fursa hii. Mtu anapojisikia *weekend* au *holiday* na familia yako unatanguliza gari yako unapita pale Tanganyika unafuata taratibu husika siku ya pili unapanda gari yako unakwenda Ngorongoro, Serengeti.

Unakwenda na usafiri wako, kama wao wanavyokuja hapa wakatembea katika *beach* zetu wanakuja na gari hapa za (T**)**, wanakuja pale wanakamilisha taratibu kidogo wanaingia nchini wanazunguka baadae wanakwenda zao. Sasa kuna uharamu gani kwa Zanzibar kutumia gari zetu kwa ajili ya kwenda kwenye matembezi yetu ya kawaida ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa kama sisi ni wenzao au ndugu zao katika Muungano huo.

Mhe. Spika, lakini hapo hapo nimeona kwamba kuna baadhi ya watu ambao wanatumia hii vizuri tu, kuna mfanyabiashara anashughulika na masuala ya *transport* anatumia pande zote za Muungano katika kupitisha magari yake. Sasa sijui yule kachukuliwa vipi hata hawa wengine iwe shida kupata fursa ile.

Mhe. Spika, nafikiri hilo waziri atuweke wazi katika suala hilo, inakuwaje tushindwe kutumia *temporary transportation* kwa ajili ya sisi Wazanzibari kwenda kutumia vipando vyetu upande wa pili wa Muungano au vile vile kwa *East Africa*.

Vile vile napenda kuzungumza suala zima la bandari, kama tunavyofahamu kuwa bandari ni uti wa mgongo tunategemea bandari kwa ajili ya kukusanya *import tax*. Bandari imekuwa kilio cha muda mrefu sasa hivi kwamba *congestion* imekuwa kubwa sana katika Bandari yetu ya Zanzibar mpaka

kufikia baadhi ya kampuni za meli au wasafirishaji kuongeza *sircharges* ambapo walikaa wakafikiria kuongeza 250 *dollar* kwa kontena la 20 *feet* na 450 kwa kontena la 40 *feet*.

Hii haiishii pale inaishia kumpa mzigo mtu wa chini. Kwa sababu kama mfanya biashara kanunua mzigo wake kaleta hapa kwa dola 2000 anaambiwa sasa hivi imeongezeka dola 400, ina maana tayari kuna dola 400 imeongezeka karibuni dola laki nane. Kwa hivyo, hatokubali ipotee ile na yeye ataongeza gharama kwa watumiaji wa chini, huoni kwamba anatupa wakati mgumu wakati ukiangalia kwamba kipato chetu hakiendani na maisha yalivyo.

Sasa kupatikana hiyo imesababishwa na bandari kukosa sehemu mbadala ya ku-*shift* zile kontena zao tupu mle ndani. Kwa sababu bandari yetu ina uwezo wa kuchukua kontena 2,000 tumejibana hapo hatuna uwezo huo lakini ilikuwa mwanzo 1,500 mpaka sasa hivi ni 2,000; inafika wakati mpaka makontena 2,800 inashindikana hata ile *lift stacker* kutembea katika bandari yetu na kuipa wakati mgumu meli kukaa nje kwa muda mrefu mpaka ikafikia kuongezwa gharama hiyo.

Sasa nini njia mbadala, hapo nyuma ilikuwa kuna eneo ambalo wanatumia kuwekea *empty container* katika eneo la Bwawani na siku hizi eneo hilo bahati nzuri tumepata mwekezaji ambaye kapewa anataka kuja kuwekeza, lakini nafikiri bado hajawa tayari angeturuhusu tu Mhe. Spika, akawapa bandari wakaendelea ili kuondoa lile tatizo lililokuwepo ndani ya bandari. Leo hii unasafirisha mzigo kutoka Dubai mpaka Zanzibar kwa wiki mbili, lakini kupata kontena lako ambalo limo ndani ya bandari ya Zanzibar unachukua mwezi mzima au wiki tatu.

Nini tunafanya halafu tunasema kwamba tunataka kupeleka uchumi tupate pesa, mtu mzigo umeshafika pale umesafiri siku 14 kutoka Dubai lakini linakaa pale siku 21 ndio ifike hatua ya kupata mali yako kuingiza dukani. Nafikiri ni tatizo kubwa na vile vile nahakikisha pengine hata baadhi ya meli kutishia kupunguza *route* zake kuja Zanzibar, nafikiri utakuwa wakati mgumu.

Hapo siku za nyuma ilifika muda ilitu-*cost* katika gharama hii mfuko wa saruji ulifika shilingi 2,000 kwa sababu saruji iliadimika, lakini meli zipo nafasi ya kutoa kontena hazipatikani kwa siku nzima bandari ya Zanzibar ilikuwa na uwezo wa kushusha kontena 15 mpaka 20 wakati nyuma ilikuwa na uwezo wa kushusha mpaka *shift* moja zaidi ya kontena 100 inashusha. Hii ilikuja baada ya *congestion* vyombo havizunguki ndani ya bandari kutokana na wingi wa kontena zile.

Sasa basi tungeomba kupitia fursa hii kama Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango tunahitaji mapato ya dhati kabisa tutoe angalau msamaha au tumuombe mwekezaji yule kama hajawa tayari, kama tulivyothubutu kuwapa wengine ambapo kuna wengine kawaongezea miezi sita waendelee na shughuli zao basi na bandari nao awaongezee angalau muda wakati wanatafuta njia mbadala ya kuweza kujitatua katika tatizo hilo.

Vile vile, bado kuna tatizo pengine la vyombo, pia bandari kuna tatizo kubwa sana la *port gear***.** Imefika muda mpaka sasa hivi shirika lile limekodi vyombo kutoka Tanzania Bara baada ya kushindwa kuvikarabati vile vya kwao pengine gharama imekuwa kubwa, lakini la kushangaza kwamba wameweza kukodi chombo ambacho kinatembezwa kwa masaa manane kwa siku tofauti na vyombo tulivyokuwa navyo sisi wenyewe ndani ya bandari ile vinakwenda muda wowote, *more than 24 hours* zinaendeshwa tu, lakini kile kilichokodiwa shirika hili limepewa masharti kwamba wasiendeshe zaidi ya masaa manane lakini *cost* imekuwa ni kubwa.

Mhe. Spika, vile vile kuhusu suala la bandari bado wapo watu ambao ndani ya bandari ile hawaitakii mema nchi yetu katika kutupatia mapato. Kuna mianya mingi sana nathubutu kusema katika bandari ile, nafikiri Mhe. Waziri wa Fedha kuna haja ya kuweka mkakati maalum kutegemea kwamba bandari ituingizie pato basi iangaliwe kwa jicho kali sana katika vitengo vyake vile. *Loophole* nyingi sana za uvujaji wa mapato katika sehemu mbali mbali ikiwa ndani ya bandari hata katika taasisi nyengine za fedha katika bandari ile.

Mhe. Spika, pia ningependa kuzungumzia juu ya suala zima la Mhe. Rais la kutoa pencheni ya shilingi 20,000 kwa wazee wetu waliostaafu. Ni vizuri sana anapaswa kushukuriwa kuwaza wazo hilo, nafikiri katika Afrika Zanzibar itakuwa nchi ya nne kuweza kutoa shilingi 20,000 kwa wazee wetu ambao wamechoka. Lakini baadae pengine tungetoa rai kwamba wazee wale hawana nguvu na mzee yule unampa shilingi 20,000 ambayo anajikimu katika mwezi au miezi miwili.

Kuna mambo mengi sana yamemzunguka mzee yule anaonaje basi kupitia kauli hii kuongeza pato kwamba baada ya kutoa ile pesa tukaenda katika kumpatia bima ya afya ambapo wazee wale wengi tunaweza kuwatibu kwa mwaka mzima kwa shilingi 76,800 badala ya 20,000. Hii ni karibu shilingi 120,000 kwa mwaka, tungekuwa tunalipa shilingi 76,800 unamsaidia mzee yule pindi akipata matatizo ya afya anatibiwa katika hospitali zaidi ya 600. Sina nia ya kupiga debe kwa baadhi ya kampuni za bima hapana, lakini unaangalia ile hali halisi ambayo ipo.

Mhe. Spika, nimezungumza hivyo kwa sababu jambo hilo nimelifanya katika jimbo langu nimeweza kuwatolea wazee bima karibu wazee 270 ambapo wanafaidika na bima ya afya, kulikoni kusema nawapa shilingi 10,000 au 20,000 kidogo ingenipa matatizo makubwa kwa wazee wetu walioko sasa hivi. Kama tunavyojua matatizo yako mengi sana ukiangalia sukari, matatizo ya mikojo, mara hivi, nafikiri ingelikuwa tunawapatia bima za afya ingekuwa tunawapenda zaidi na bado tunahitaji kuwapa. Lakini nafikiri mwenyewe aliamua akaona hilo ndilo, basi tunamshukuru pia, lakini kuna haja ya kuliangalia hilo jengine pia ili wazee wetu hawa wakawa katika mustakabali mzuri baada ya kutumikia nchi yetu kwa muda wote.

Vile vile, mimi ningependa kuzungumza suala jengine juu ya tafauti. Nafikiri pato letu la ndani tulilokusudia kupata pale ni shilingi 450.5 bilioni, kuna tafauti karibuni ya shilingi 349.9 bilioni ni pesa nyingi sana. Tumesema tumekusudia kupata ruzuku, mikopo ikiwa kama tutaipata, sasa kama mfano hatukuipata hatuoni kwamba mzigo utakuwa bado ni mkubwa katika serikali yetu tutashindwa kutekeleza bajeti hii.

Mhe. Spika, nafikiri tutafute njia mbadala ya kuweza kuongeza vyanzo vyetu vya mapato ili hii bajeti tuweze kuikidhi isiwe kutegemea ruzuku zaidi angalau asilimia 50 au 60 ya bajeti hii iwe mapato yetu ya ndani na hii iliyobakia kidogo iwe katika suala la ruzuku.

Mhe. Spika, nafikiri kwa leo acha nichangie haya machache bado tunaendelea kujifunza katika Baraza lako hili, nathubutu kusema kwamba naunga mkono hoja kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na vile vile naunga mkono asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Spika ahsante sana, kwanza kwa ruhusa yako kwa kuweza kunipa fursa hii adhimu ya jioni ya leo nami kupata kuchangia hotuba hii ya serikali iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango kwa dhamira ya kutoa michango hasa katika taifa letu la Zanzibar.

Pili, naomba nitumie fursa hii rasmi sasa kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwera nami kumpongeza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za ndio na kupewa dhamana hasa katika awamu yake hii ya pili. Lakini pia nitoe pongezi kwa wale wote waliopata teuzi kutoka kwa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar hasa kwa dhamira ya kutaka kumsaidia kazi na kutaka kuwaletea maendeleo wananchi

wote wa Zanzibar pamoja na taasisi zake kwa ujumla. Nami naomba niende moja kwa moja katika hotuba hii ya Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Spika, kwanza nianze na suala zima la bandari. Mhe. Spika, nchi yetu ama taifa letu limezungukwa na kisiwa asilimia kubwa ya mapato yetu tunategemea kutoka katika tasnia ya utalii sambamba na bandari, lakini bado kuna mianya mingi hasa ya watu kuweza kukwepa kulipa kodi na kutokuweka miundombinu mizuri hasa katika maeneo yote yale yaliyokuwa na bandari bubu.

Mhe. Spika, ni muda muwafaka sasa umefika kwa wizara na taasisi husika kuweka mkazo hasa katika yale maeneo yote ambayo tumekuwa tunaingiza bidhaa kiholela pasina kulipiwa kodi na ushuru wa aina yoyote, maana kwa kufanya hivyo tunapata na kupunguza sana pato la taifa lakini pia tunapunguza sana zile pesa ambazo zingeweza kusaidia wananchi wengi katika taifa hili katika masuala ya maendeleo.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika suala zima la uwanja wa ndege hasa pale *Terminal II*. Tangu kuanza kujengwa kwa uwanja huu ni kipindi kirefu sasa, muda mrefu umepita lakini bado mradi huu umekuwa ukisuasua. Sasa ni muda muwafaka kwa dhamira ya dhati serikali hii iliyokuwepo chini ya mikono salama ya Chama cha Mapinduzi kuweza kutia nguvu za kutosha hasa kuimarisha na kutoa fungu madhubuti kwa kuweza kukamilika uwanja huu wa ndege.

Maana ya kukamilika kwa uwanja huu wa ndege wa kisasa kabisa kutaweza kutoa fursa nyingi hasa za ajira lakini pia utaruhusu kwa mashirika mbali mbali ya ndege ya kimataifa kuweza kufika katika kiwanja chetu cha ndege jambo ambalo litaweza kuiongezea serikali mapato; lakini pili tutaweza kupata *foreign currency* ambayo inaweza kuweka uchumi wetu kuwa katika hali nzuri.

Mhe. Spika, niungane sambamba kabisa na wazungumzaji wote waliopita hasa Mhe. Mohammedraza Hassanaali alianza kuwa na hoja ya kutumia shilingi bilioni takriban 18 kwa ajili ya kuweka mradi wa *CCTV Camera* hasa katika maeneo yetu. Mhe. Spika, kweli maendeleo katika taifa hili tunayataka sote na sote tunaumwa sana na maendeleo, lakini bado kutenga kiasi kikubwa cha fedha hiki takriban shilingi 18 bilioni kwa dhamira ya kuweka *CCTV Camera* katika taifa letu hali ya kuwa bado watoto wanakaa chini katika skuli zetu, hali ya kuwa bado hatuna matundu ya kutosha ya vyoo katika skuli zetu jambo ambalo linaendelea kuzua magonjwa tofauti. *(Makofi)*

Vile vile kutenga kiasi kikubwa hiki cha pesa hatuna dhamira ya kusema kwamba hatutaki kuweka taifa letu katika mikono salama ya ulinzi hapana, lakini bado taifa letu haliko vizuri katika tasnia kubwa ya miundombinu. Bado tuna barabara mbaya lakini bado tuna mambo mengi ya kufanya jambo ambalo lingechukua kiwango hiki cha pesa kupeleka katika miradi mingine.

Mhe. Spika, nitoe mfano kidogo, katika bajeti hii iliyowasilishwa nitoe mfano katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambayo wizara hii imekuwa na changamoto lukuki niweze kunukuu kidogo miongoni mwa changamoto zake wamekuwa wakisema kwamba wana uhaba wa vifaa vya maabara, kuna uhaba wa walimu hawa wa hesabati na sayansi, kuna uhaba wa mambo ya miundombinu hasa katika teknolojia ya TEHAMA vifaa kama kompyuta, umeme na kadhalika. Lakini pia kuna uhama wa vifaa vya samani vikalio haya madeski katika skuli zetu na tuna takriban vitu vingi ambavyo tungeweza kutoa angalau kiasi cha shilingi bilioni mbili katika hizi shilingi 18 bilioni, tukawa katika skuli zetu kwa dhamira ya kupunguza matatizo haya.

Leo Ofisi ya Bunge ya SMT wameweza kuchukua takriban zile shilingi bilioni sita wakaweza kutengeneza madawati na yanatarajiwa kusambazwa katika skuli zote katika taifa hili. Sasa kwa nini na sisi angalau katika shilingi 18 bilioni zilizotengwa kwa ajili ya mradi wa *CCTV Camera* tukachukua angalau shilingi bilioni mbili tukapeleka katika mirad ya skuli zetu hasa katika kutatua matatizo haya ya vikalio, lakini pili kuweza kutoa nafasi za ajira kwa walimu wetu na tatu hata kupunguza madeni yanayostahiki kwa watendaji wetu jambo ambalo litatoa motisha la wao kuweza kutoa elimu bora, jambo ambalo litaweza kutoa motisha hata wao kupata moyo wa kufanya kazi na kutoa elimu bora kwa wanafunzi wetu.

Mhe. Spika, sambamba na hilo kwangu mimi bado mradi huu umekuwa na thamani lakini bado nasema muda wake haujafika sana, kwa sababu leo vijana wengi katika taifa hili wanakosa mikopo ya serikali na vijana wengi hasa wale ambao wana dhamira ya kutaka kusoma elimu ya sheria wamekuwa wakinyimwa kabisa mikopo kutoka katika serikali yao.

Hili ni jambo ambalo linawanyima fursa ya kufanya *selection* bora katika zile tasnia zao wanazotaka kwenda kusoma hasa katika elimu ya juu na ukizingatia elimu hii ya sheria katika taifa letu la Zanzibar inatoka katika Chuo Kikuu kimoja tu na chuo chenyewe ni cha *private* sio chuo cha serikali. Sasa ni muda umefika ni vyema angalau pia tukatoa fungu katika mradi huu tukaweza

kuwapa vijana wetu ambao wangeweza kuongeza elimu na ambao watakuja kuisaidia fika serikali katika mambo ya kisheria na tasnia nyengine katika taifa letu hili la Zanziabr.

Mhe. Spika, bado naendelea kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha kwamba kiwango hiki cha mradi wa *CCTV* bado una dhamira njema, ina nia stahiki kabisa ya kuweka *security*, lakini tunasema huduma hizi za maendeleo katika jamii bado zina ubora wa hali ya juu sana na bado zina uhitaji mkubwa kuliko huu mradi wa *CCTV* ambao utatugharimu pesa nyingi, lakini marejesho yake yakawa kidogo ama yasionekane kabisa katika taifa hili.

Kwa kuzingatia tuna takriban mwaka mmoja tangu ule mradi wa awamu ya mwanzo wa kuwekwa kwa *CCTV Camera* katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi umewekwa lakini bado kumekuwa na changamoto nyingi. Sasa ni vyema kwa sababu mrejesho na pesa hizi ni nyingi ni vyema tukazichukua na kuziwasilisha katika maeneo mengine kwa dhamira ya kutaka kutatua changamoto tofauti za ajira na kutatua changamoto tafauti kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Pia nimefuatilia kwa makini sana hotuba hii ya Mhe. Waziri, tunajua yeye ni mtu mweledi sana kwa mambo haya ya mipango na uchumi, pia tunatambua sana mchango wake.

La pili, tunaweza kusema kwamba bado taifa hili linahati miliki kubwa sana ya vijana, bado tunasema taifa hili linahitaji mshikamano mkubwa sana kutoka katika kundi kubwa sana la vijana. Hivyo, ni muda sasa umefika kwa sababu suala la ajira limekuwa ni tatizo na bado tumekuwa tunasema kwamba hata wale watu ambao wamefika *stage* ya kustaafu wamekuwa na msamaha ya kuongezewa miaka miwili katika mikataba yao kwa dhamira ya kwamba ya kuendelea.

Lakini kunapokuwa na utaratibu wa kuendeleza watu hali ya kuwa tuna benki kubwa ya watu ambao hawajaingia katika nafasi hizo bado tunatoa hasira kubwa kwa watu ambao wameshanufaika vya kutosha na elimu waliyopewa na Serikali yao hii ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia tunawanyima vijana wengi fursa ya kuitendea haki na kulitendea haki taifa lao la Zanzibar kwa kushindwa kupata nafasi za ajira hasa katika muda unaostahiki kwa dhamira ya kuwaongezea watu muda katika maeneo yao ya kazi.

Nalisema hili Mhe. Spika, ni vyema sasa na muda ukafika kwamba wenzetu wa Wizara ya Fedha wakaweza kuweka fungu maalum kwa ajili ya vijana hasa

kwa dhamira ya kuwapa mikopo nafuu na iliyokuwa na masharti kidogo maana kwa kufanya hivi tutawaweza kuwa-*motivate* hasa kwa wale watakaokuwa na *fields* zao kama ni za *technical* au nyengine kuweza kutoka na kwenda kuzifanyia kazi nje ya kutegemea ajira hizi za serikali.

Tunafahamu sana na vijana wengi wanafahamu fika kwamba bado tatizo la ajira ni tatizo la dunia kwa ujumla. Lakini nasi kama serikali tuna kila sababu ya kutenga fungu maalum ambalo litaweza kwenda kuwasaidia vijana ambao wanapambana na changamoto kubwa sana za ajira katika taifa hili.

Kwa kufanya hivi Mhe. Spika, tutaweza kupunguza viguvugu kubwa katika taifa letu kwa kuweza kuwalinda vijana ambao na kuweza kupunguza matatizo yao. Maana kama ambavyo Mhe. Waziri alipokuwa akiwasilisha bajeti hii kwamba pato la taifa limeongezeka. Lakini kuongezeka kwa pato la taifa linaonekana *normal in document* lakini ukija *in reality* pato hili huwezi kuliona maana siku baada ya siku tunaambiwa uchumi umepanda lakini ukitizama mzunguko wa pesa katika *society* inakuwa ni adimu kuona.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohd Shein kwa kuanza kwa vitendo kutekeleza ahadi zake na ilani la Chama cha Mapinduzi 2015/2020. Alianza kusema katika kampeni zake aliendelea kusema katika mikutano yake na hakusita kusema hata siku ya wafanyakazi kwamba atahakikisha kima cha chini cha wafanyakazi katika taifa hili kinapanda kwa zaidi ya asilimia mia. Tunamshukuru sana na nawafanyakazi wengi sana wamefarajika sana kwa kuongezewa kiasi kikubwa hichi cha pesa kwa takribani asilimia mia. Lakini suala linakuja kweli wanafarajika sana kwa kuongezewa pesa hizi na wanashukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuongeza mishahara kwa kiwango hiki.

Wafanyakazi wengi wameanza pia kusema angalau basi kiwango hiki cha fedha kingeanza kulipwa mnamo mwezi wa Januari kuliko kwenda katika mwezi wa April. Kwa kufanya hivi angalau utaweza kupunguza machungu ya watu wengi ambao wanategemea kupata fedha hizi, lakini kwa kutamkwa kwa kupandishwa mishahara katika taifa hili tayari kumeshaanza dalili za wafanyabiashara hasa wale biashara ndogo ndogo za vyakula kuanza kupandisha bidhaa zao kwa kigenzo kwamba tayari serikali imeshapandisha mishahara kwa wafanyakazi wao.

Sasa tuwaombe sana na kuna haja ya kuendelea kutoa elimu sana na taasisi zetu na idara zetu ambazo zinahusika na uthibiti wa upandishwaji holela wa bidhaa ikachukuwa jukumu stahiki hasa kwa maeneo yote ambayo watu wataweza na

watakuwa na utaratibu wa kupandisha kiholela bidhaa hizi. Kwa kufanya hivyo tutaendelea kuwasaidia watu wetu lakini kwa kufanya hivyo tutaendelea angalau ku-*maintain* kule kupandishwa kiholela kwa bidhaa maana tayari jamii yote ya nje imefarajika kwa kuongezeka kwa kima cha chini cha mishahara lakini haliyakuwa mishahara hii itaanza kulipwa kuanzia mwezi wa April 2017.

Mhe. Spika, sambamba na hilo baada ya kutizama hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha pia tunaomba sana imeshindwa au haikuwezekana ku-*specify* moja kwa moja ni lini sasa punguzo hili la *paye* litaweza kupunguza kutoka kwa asilimia 13 mpaka asilimia 9.

Sasa ni vyema tukaiomba ama tukamshauri Waziri wa Fedha ni vyema punguzo hili likaanza wa uchache kuanzia mara tu pale bajeti hii itakapopitishwa mwezi wa Julai watu hawa waanze kukatwa kwa kima hiki na sio tukasubiri kwamba mpaka pale tutakapoanza kuwalipa pale mshahara mipya ndio tuanze kupunguza kiwango hiki.

Mhe. Spika, tuwapongeze sana watendaji wetu wa *ZRB* kwa kujitahidi sana kukusanya mapato katika taifa hili maana wanafanyakazi kubwa, stahiki lakini bado tunasema bado kuna mianya mingi sana ya ukwepaji ambayo watendaji hawa wa *ZRB* kwa namna mmoja au nyengine wamekuwa wanahusika.

Niungane na Kamati wa Wenyeviti wakati wa uwasilishaji wao wa hotuba yao asubuhi hii ya leo na Mwenyekiti aliyeweza kuwasilisha kwamba ni muda sasa umefika tukatafuta *external auditing* akaweza kufanya *auditing* katika taasisi yetu hii ya *ZRB* ili kuweza kutambua kama kweli kima hichi cha pesa ambacho taasisi hii inakusanya kama ni sahihi au si sahihi maana bado watu wanasema bado kuna mianya mingi sana ya ukwepaji wa kodi ambayo taasisi hii inahusika.

Sambamba na hilo niseme hata kwa mfano ukirudi pale Bandarini Zanzibar ni miongoni mwa maeneo yanayonufaika na bandari lakini Zanzibar ni miongoni mwa nchi ambazo zina kampuni nyingi za *clearing and forwarding* jambo ambalo kunakuwa na *competition* katika kuweza kutafuta mianya ya ukwepaji wa kodi ili kuweza kufanya kazi zao. Ni vyema sasa tukaifanyia *auditing* idara hii kwa dhamira ya kuja kuisaidia na kuongeza mapato hasa katika taifa letu.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri wa fedha sambamba na kumpongeza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa kuendelea kuwathamini wazee katika taifa hili maana wazee hawa wametoka mbali, wazee hawa wamefanya mengi na makubwa katika taifa hili, wazee hawa wamelitumikia vyema taifa hili.

Pia nitoe pongezi zangu hizi za dhati kabisa baada ya maamuzi ya Rais wetu wa Zanzibar kuaza kuwapa pencheni wazee wetu hawa ya kima hichi cha elfu ishirini kwa kila baada ya mwezi. Dhamira hii ni njema, zamira hii inaonesha kuenzi na kuwathamini wazee wetu katika taifa letu. Lakini pia bado idara hii ina changamoto zake tunasema pia tunajukumu na bado kuna wazee wengi ambao wana sifa za kupata pencheni hii na wamenyimwa fursa hii ya kupata.

Ni vyema sasa tuende kukafanye upembuzi yakinifu katika maeneo yale kwa dhamira kwamba kila anaestahiki kupata fungu lile basi alipate pale muda unapofika na alipate pale ambapo wakati wa kupata fungu lile utakuwa umefika kwa kuweza kupunguza minongono na kupunguza lawama zote kutoka kwa wazee wetu hawa maana wazee hawa ni tumzo na rasilimali njema katika taifa letu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nasema bado hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha na Bajeti hii ya Serikali ni bajeti nzuri na bejeti ambayo imeakisi kutaka kutoa taifa letu kutoka katika uchumi wa chini kwenda katika uchumi wa kati. Sasa ni muda muafaka umefika sasa ni vyema tukaanzisha sasa miundo mbinu yetu madhubuti kwa ajili ya kufua umeme. Kwa sababu umeme huu tunaopata lakini kwa maendeleo haya ambayo tunakwenda nayo baada ya miaka mitano itapelekea umeme wetu huu ambao tunaupokea kutoka Tanzania Bara, usiweze ukawa na mahitaji madogo usiweze kukidhi hasa ukilinganisha na maendeleo ambayo yanapatikana katika taifa letu la Zanzibar.

Hivyo, ni vyema sasa serikali ikaandaa mpango madhubuti kwa dhamira ya kutafuta na kuanzisha mradi ambao utakuwa mbadala wa kufua umeme jambo ambalo litaweza kusaidia taifa hili katika kutuletea maendeleo.

Mhe. Spika, nizungumzie suala zima la uvuvi, bado serikali hii haijaweka nguvu ya kutosha katika suala zima la uvuvi maana bado wavuvi wetu wadogo wadogo wanashindwa kwenda katika bahari kuu kuweza kuvua na kuwa na uvuvi wenye tija hasa wenye kuwanufaisha wananchi wetu. Leo wavuvi wetu hawa wanapata tabu sana, wanahangaika sana kutokana kwamba kutumia miundombinu midogo, lakini kutumia miundombinu ambayo inashindwa kuwafikisha baadhi ya maeneo jambo ambalo lingeweza kuwasaidia kuweza kuvua samaki wa kutosha tukaweza kutumia Zanzibar. Pia tukaweza kuzalisha samaki wa kutosha jambo ambalo tungeweza kuuza Tanzania Bara pamoja na dunia na nchi tofauti kama ambavyo baadhi ya nchi nyingi za visiwa zinafanya.

Tukitizama nchi kama zile za Malasia, Indonesia wale wenzetu wa China na Korea ingawa wao wamefika mbali sana kiteknolojia lakini bado na wao

walianza hivi hivi ni vyema tukatumia kipindi hiki na ni vyema Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara hii ya Uvuvi ikaweka miundombinu ya kutosha kwa dhamira ya kutaka kufungua fursa nyingi za ajira katika taifa letu.

Pili, nizungumzie hasa katika kilimo cha Mwani. Mhe. Spika, bado wananchi wa Zanzibar hasa wale ambao wanahusika na kilimo cha Mwani wanahangaika sana. Ukizungumzia wakulima wote kwa kuanzia Jambiani kule maeneo ya Chwaka na maeneo yote kwa ujumla wanateseka sana kutokana na kwamba kilimo hichi cha mwani wamekuwa wakitumia nguvu kubwa wakitumia jitihada kubwa na wamekuwa wakitumia pesa za kutosha lakini bado kumekosekana kuwa na *rate* ya kuweza kuuza mwani ule.

Bado kumekuwa na bei ya ulanguzi jambo ambalo kuwafanya wakulima washindwe kujipatia na washindwe kuendesha maisha yao kutokana na kwamba serikali kushindwa kupanga bei stahiki hasa ya kilimo hichi cha mwani. Leo wenzetu wa Brazil wameendelea sana na kilimo hiki na bado zipo nchi ambazo zimeendelea sana na kilimo cha Mwani.

Ni vyema sana Mhe. Spika, kwa kipindi hiki serikali hii ikaendelea kuweka mkazo hasa katika kilimo hichi cha mwani, kilimo ambacho kitaendelea kuongeza pato la taifa lakini kilimo ambacho kinaendelea kuajiri watu wengi katika tasnia hii jambo ambalo linaipunguzia serikali mzingo wa kutafuta nafasi nyengine za ajira.

Mhe. Spika, nizungumzie katika vikosi vyetu hivi vya Ulinzi na Usalama. Hapa nizungumzie hasa katika ile *station* ya KMKM iliyopo katika eneo ya masingi ndani ya jimbo la Mwera. Mhe. Spika, katika kambi ile kulikuwa na kitu pale ni muhimu sana katika taifa letu. Tulikuwa na rada yetu pale ilikuwa ikisaidia sana ulinzi na usalama katika taifa letu. Lakini kwa muda mrefu wetu rada ile imekuwa haifanyi kazi na kwa kipindi kirefu sana watu wale wamekuwa wakihangaika angalau kuweza rada ile kufanya kazi jambo ambalo lingeweza kusaidia usalama katika taifa letu hasa ukitizama *jiografia* ya kambi ile pale ilipo.

Sasa ni vyema sasa serikali hii kwa kuzingatia tuna bilioni zile takribani kumi nane ambazo tulikuwa tumeziweka kwa ajili ya mradi wa *CCTV*, ni vyema tukatenga takribani kiasi cha bilioni moja kuweza kwenda kurekebisha ile rada pale maana kwa mujibu wa taarifa stahiki mitambo yote iko sawa lakini bado kuna vitu vidogo vinavyohitaji kurekebishwa ili mitambo ile iweze kufanyakazi.

Kwa kufanya hivyo tutaweza kupunguza hata ile *coast* kubwa ambazo tungeziweka kwenye *CCTV* rada hizi zina nguvu za kutosha kuweza ku-*maintain* usalama katika taifa letu hasa kwa kuzingatia taifa letu hilo lote limezungukwa na maji ama ni miongoni mwa taifa la visiwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, narudia kusema kwamba niipongeze sana hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha bado ina dhamira ya dhati kuweza kuwakomboa Watanzania. Lakini bado kina mama katika taifa hili wamekuwa wakipata mikopo kidogo sana kutoka katika serikali yao pendwa SMZ. Sasa ni vyema kina mama hawa ambao wamekuwa ni mahodari katika kuanzisha *SACCOS* tafauti katika maeneo yao. Ni vyema sasa serikali hii ikatoa kipaumbele maana taifa hili bila ya kina mama na vijana haliwezi kusonga mbele. Taifa hili bila maamuzi ya kina mama na vijana haiwezi kuwa chachu ya mafanikio katika taifa hili.

Sasa ni vyema serikali ikaendela kuipa nguvu wizara hii stahiki kwa kuweza kuanzisha angalau Benki ya wanawake katika taifa hili, kuweza kutoa fursa mpya kwa kina mama ambao wataweza kuanzisha miradi yao na ambao wataweza kwenda katika Benki ile kukopa na kuweza kujiendeshea maisha yao, maana mitaji hii ya kina mama wanaopata fursa hizi wananufaisha mengi, wananufaisha akina baba ambao wako majumbani; vijana ambao wanawalea. Pia wanaweza kunufaisha watoto ambao tunagemea tutakavyoweza kuwatunza bora na kuweza kuwaekea mazingira mazuri wanaweza wakaja kuwa kigezo chema hasa katika taifa linalokuja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimalizie katika sekta hii ya afya. Sekta hii ni sekta nyeti sana katika taifa letu. Sekta hii ni miongoni mwa taasisi muhimu sana hasa kwa kuzingatia kwamba bado tuna hospitali yetu kubwa ya Mnazi mmoja, lakini bado tuna hospitali zetu nyingi ambazo zimekuwa zikikosa vifaa stahiki kwa dhamira ya kwamba kuiongezea mzigo hospitali yetu ya Mnazi mmoja.

Leo tuna hospitali kubwa sana iko Makunduchii, leo tuna hospitali kubwa sana iko Kaskazini ya Kivunge ni muda sasa muafaka wa kuweza kuziboresha hospitali zetu hizi ili kuweza kupunguza msongamano unaoikabili hospitali yetu ya Mnazi mmoja kwa dhamira kwamba kuweza kutafuta madaktari bora ambao wana sifa za kutosha. Lakini pili kuweza kupeleka vifaa stahiki ambavyo vinakosekana katika hospitali hizi ambazo wananchi wengi wanapata tabu ya kwenda kufatilia katika hospitali yetu ya Mnazi mmoja.

Kwa kuzisaidia hospitali zetu hizi kubwa tutaweza kuisaidia na kupunguza hasa matatizo mengi ambayo yanawasibu Wazanzibari kwa ujumla ambao wanakimbilia katika hospitali ya Mnazi mmoja. Maana dhamira

tunapowasaidia wananchi katika maeneo yao tutaweza kusaidia sana kuweza kuwapunguzia usumbufu lakini tutaweza kuwasaidia sana kwenda kupunguza zile kero ambazo kila kukicha kero katika hospitali ya Mnazi mmoja zinazidi kuongezeka. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini pia serikali hii ya SMZ bado ina kila sababu ya kuweza kutoa motisha kwa wahudumu hawa wa sekta ya afya. Wahudumu hawa wanafanya kazi kubwa, wanafanyakazi ngumu na wanatumia muda mrefu katika kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata huduma stahiki kwa mujibu ambavyo serikali hii inawajibika ipasavyo. Sasa ni vyema sasa kwa watendaji wetu hawa katika sekta zetu za afya tukaweza angalau kuwapa motisha ya baadhi ya malipo yao maana wapo wahudumu wengi, ambao bado wanaendelea kuidai serikali jambo ambalo linawapungizia motisha wa kuweza kufanya kazi hii, hasa pale ambapo wanatakiwa kufanya kama inavyotakiwa.

Kwa kufanya hivi Mhe. Spika, tutaweza kurekebisha lakini tutaweza kwa kuwapa wananchi wetu huduma stahiki ya afya tutaweza kuwa na nguvu kazi kubwa sana ya taifa hili. Taifa ambalo lina wananchi wagonjwa wagonjwa haliwezi kuwa na maendelea maana kazi nyingi za taifa zinashindwa kuendelea. Sambamba na hilo Mhe. Spika, nimepitia sana hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha nimepitia sana katika masuala haya ya miundo mbinu.

Mhe. Spika, taifa ambalo halina mbinu ni vigumu sana kuweza kufikia katika uchumi wa kati sana vile ambavyo taifa hili linategemea kufikiwa. Tunapozungumzia leo miundo mbinu tuzungumzie katika mambo yote ya barabara za ndani na barabara za nje, barabara ndogo na barabara kuu. Ni vyema sasa Mhe. Spika, njia hizi ambazo zimekuwa zikijengwa kwa kipindi kirefu hasa hii njia ya kuelekea Kaskazini Chaani na kwengineko. Njia hii Mhe. Spika, imekuwa ni kero na usumbufu sana kwa watalii wetu, watu wanakuja hapa kupumzika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tunapokea watalii wengi sana ambao wanakuja kupumzika. Lakini mazingira hayawi bora kwao hasa ya mindombinu hii, jambo ambalo linarudisha nyuma pale wanapotoka wanatoka na *message* ambayo inakuwa si mzuri katika taifa letu. Ni vyema sasa serikali kuliko kuanzisha miradi mipya ambayo imekuwa si endelevu, kila siku ni wakati sasa ikafika tukasema kwa kipindi cha miaka miwili hii serikali iwekeze katika suala zima la miundo mbinu angalau ipungue kwa asilimia kubwa ili tuendelee katika sekta nyengine.

Mhe. Spika, serikli imekuwa ikitumia pesa nyingi sana kwa ajili ya kugharamikia miundombinu hii. Lakini bado miundombinu hii hasa ya

barabara imekuwa ikijengwa katika kiwango kidogo sana. Jambo ambalo barabara nyingi zimekuwa hazifiki hata miaka miwili zimekuwa zikiharibika.

Mhe. Spika, nasikitika sana kwa gharama kubwa iliyotumika na serikali yangu ya Mapinduzi kwa kujenga barabara ya Amani-Dunga. Serikali imetumia gharama kubwa sana kujenga barabara hiii. Lakini takribani miaka miwili tu tangu barabara hii ifunguliwe rasmi, barabara hii Mhe. Spika, kwa kumpa taarifa Mhe. Waziri kwamba hata wakitoka leo kwenda kuikagua basi barabara hii haitakuwa na uwezo wa kufika mwaka mmoja mwengine mbele, kutokana na kwamba barabara yote imeshakuwa ikikatika maeneo ya pembembeni.

Hii inakuja kutokana na kwamba kunakuwa na miradi mikubwa katika taifa letu, lakini hatukuwa na hatuna usimamizi bora yakinifu katika miradi hii. Jambo ambalo tutakuwa tukitumia pesa nyingi lakini kwa muda mfupi miradi hii imekuwa ikiharibika tutakuja kutizama baada ya miaka mitano barabara, hizi ambazo tunahangaika kuzijenga leo kesho zitakuwa tena zitaharibika na zitahitaji maboresho makubwa sana.

Kitu ambacho kama tutakuwa hatuna usimamizi uliokuwa mzuri na tutakapokuwa na usimamizi bora, tutakapoweza kutumia kodi stahiki za wanyonge katika taifa hili kwa kutengeneza miundo mbinu hii ni vyema sasa watu wanakapokuwa wanapata fursa za dhamana ya kusimamia wasimamie stahiki na kuweza kuhakikisha kodi za wanyonge katika taifa hili zinatumika ipasavyo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa muda.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Nimalizie katika suala zima la maji.

Mhe. Spika: Basi Mheshimiwa muda wako ushakwisha.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Ahsante Mhe. Spika, kwa sababu muda wangu haujatosha lakini naweza kumaliza kwamba naunga...

Mhe. Spika: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha kwa asilimia mia. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mihayo Juma N'hunga kwa mchango wako, mchango wako ulikuwa mzuri tu. Lakini muda hauko rafiki sana nasi.

Waheshimiwa Wajumbe nimeombwa niwatangazie kwamba wale Waheshimiwa ambao bado hawajarejesha vitabu vya Bajeti kwamba wanaombwa wavirejeshwe na wawape wahudumu ili waweze kuzikusanya.

Baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe naomba niwatangazie pia kwamba kesho nikutajieni majina ya wachangiaji wanne wa mwanzo kesho kwanza kabisa atakuwa Mhe. Said Omar Said Mwakilishi wa Wingwi, atafuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid ambaye afuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh pamoja na Mhe. Dkt Makame Ali Ussi.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya matangazo hayo na kwa kuwa muda wetu utakuwa umekwisha napenda sasa niakhirishe shughuli za Baraza mpaka kesho tarehe 24 siku ya Jumanne saa 3:00 barabara za asubuhi. (*Makofi*)

(Saa 1:46 usiku Baraza kiliakhirishwa hadi tarehe 23/05/2016 saa 3:00 asubuhi)